

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao Cha Nne – Tarehe 11 Juni, 2010

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 na Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Uchumi, juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 26

Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu-CDA

MHE. EPHRAIM N. MADEJE aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya makazi holela katika maeneo ya Manispaa ya Dodoma, Chinyoya, Ipagala, Chadulu na kadhalika yamekuwepo kwa zaidi ya miaka ishirini iliyopita kutokana na *CDA* kutopanga maeneo mbadala ya kuhamishia watu; licha ya vitisho vya *CDA* vya kuvunja makazi hayo:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuyahalalisha na kuyaboresha makazi hayo kama vile ilivyofanya kule Manzese Dar es Salaam?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kubuni mradi mahsusui wa kuboresha makazi haya ili kupata ufadhili wa Mashirika ya Kimataifa kama *HABITAT* badala ya kuitegemea CDA ambayo bajeti yake haikidhi mahitaji?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wananchi wachache ambao itabidi wapishe ujenzi wa barabara katika eneo la Chang'ombe ambalo limekwisha halalishwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Dodoma, ambao ni Makao Makuu ya Tanzania umeandaliwa Mpango Kabambe ambao ndiyo dira kuu katika ujenzi na uendelezaji wa Makao Makuu. Mpango kabambe huu unatoa mwongozo wa uendelezaji wa matumizi mbalimbali ya ardhi.

Utekelezaji wa Mpango Kabambe umekuwa na matatizo mbalimbali katika utekelezaji wake.

Matatizo hayo ni pamoja na uvamizi wa maeneo ya wazi na hifadhi ya misitu, uvamizi wa maeneo ya barabara na huduma nyingine za msingi, ujenzi holela, uchimbaji mchanga, na kadhalika shughuli ambazo hazizingatii kabisa mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka imelazimika kufanyia uboreshaji maeneo yalikuwa yamevamiwa na wananchi wengi na ubomoaji kuonekana kama siyo suluhu mwafaka. Katika kuboresha maeneo hayo, wananchi hulazimika kuchangia gharama za upimaji na wale wanaoathiriwa na zoezi hilo, hupewa viwanja mbadala badala ya kulipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baada ya maelezo hayo, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Madeje yenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (*CDA*) imeshafanya maboresho katika Maeneo mbalimbali ya Mji wa Dodoma ambayo ni Chadulu, Ipagala, Chang'ombe, Kizota, *Osterbay*, Maili Mbili, Mlimwa Kusini na Kinyambwa.

Aidha Serikali iliama tangu mwaka 2003 kuwa uboreshaji wa eneo la Chinyoya hauwezi kufanywa kwa kuwa eneo hilo lilitengwa maalum kwa ajili ya matumuzi ya Taasisi za Serikali, hifadhi ya maji safi, misitu pamoja na Barabara Kuu ya Dodoma-Iringa (*processional way*). Kutokana na uamuzi huo, wakazi wa eneo la Chinyoya waliovamia eneo hilo, walikwishapewa viwanja mbadala katika maeneo ya Chidachi Mashariki na Kisasa Magharibi.

Hivyo, wananchi hao wanatakiwa hao kuondoka na kuhamia kwenye viwanja vyao walivyopewa. Waziri mwenye dhamana ya Ustawishaji Makao Makuu alikwishatoa maelezo ya kina kuhusu uboreshaji wa eneo hili mnamo tarehe 30 Machi, 2007 kupitia barua kumb. Na. FC 122/590/01/59.

Aidha, uboreshaji uliofanywa na *CDA* ulikuwa wa makazi kwa ujumla wake wakati ule wa Manzese (Dar es Salaam) ulihusu zaidi uboreshaji wa miundombinu (*Community Infrastructure Upgrading Programme (CIUP)*). Hivyo ni miradi miwili tofauti.

(b) Tangu awali Serikali iliishaona umuhimu wa kubuni miradi mahsus ya kuboresha makazi kwa kupitia ufadhili kutoka Mashirika mbalimbali ya kimataifa.

Mfano, Mradi wa Nyumba za gharama Nafuu katika eneo la Chidachi ulifanywa na Shirika lisilo la Kiserikali la *HABITAT for Humanity* na pia katika eneo la Nkuhungu Magharibi palifanyika mradi wa Uboreshaji uliofanywa na NGO moja iitwayo *Women Advancement Trust (WAT)*. Hali kadhalika, katika eneo la uboreshaji la Chang'ombe, upo mradi wa ujenzi wa barabara unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

(c) Mradi wa uboreshaji wa eneo la Chang'ombe ni mradi ambao ulikuwa na makubaliano maalum na wananchi kabla ya utekelezaji wake. Baadhi ya makubaliano hayo ni pamoja na wananchi kuchangia gharama za upimaji viwanja na kutokuwepo kwa fidia ya aina yoyote kwa wale watakaoathiriwa, badala yake watapewa viwanja mbadala, jambo ambalo *CDA* iliishatimiza ahadi yake.

(d) Kwa mantiki hiyo, suala la fidia katika mradi huo halipo. Wananchi waliopo kwenye eneo hilo la barabara tayari wamekwishapewa viwanja mbadala kama makubaliano halali yalivyokuwa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali limekuwa na jibu refu kwa sababu ya hali halisi.

MHE. EPHRAIM N. MADEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la makazi holela katika Miji yetu linatambulika katika sheria ya ardhi, na ninavyoju mimi ni kwamba kama mwananchi akijenga mahali ambapo hatakiwi ajenge lakini makazi hayo yakadumu kwa zaidi ya miaka miwili au mitatu basi ana haki zake katika fidia chini ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ametueleza hapa kwamba wananchi wa Dodoma wanapotolewa kwenye makazi ambayo ni holela wao wanapewa viwanja mbadala badala ya kulipwa fidia.

Je, hii ni sahihi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kuwa suala la ujenzi holela katika Miji yetu ni jambo la kawaida lakini kwa Dodoma hali ni tofauti kwa sababu toka mwaka 1974 wananchi wengi kwenye maeneo haya walikwishafidiwa, na wananchi wa Dodoma wale wa asili wa wakati ule walikuwa watifu, bahati mbaya wavamizi hawa wengi wao ni watu wapya waliokalia maeneo haya baada ya wale wa awali kupewa fidia.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali ilishakiri kwamba Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya *CDA* ina mapungufu, na kwa kuwa Waziri aliahidi kuleta Muswada ili kurekebisha sheria hiyo.

Je, Waziri utakubaliana nami kwamba sheria hii ikifanyiwa marekebisho itapunguza migongano kati ya *CDA* na *Manispaa* ya Dodoma?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu spika, japokuwa swalii la msingi halifanani na swalii la nyongeza la Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma, nitamjibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna mapungufu katika sheria ambayo inasimamia ujenzi wa Makao Makuu, lakini tukumbuke ujenzi wa Makao Makuu ni mchakato unaoendelea kwa muda mrefu na hivyo sheria ambayo inatarajiwa kutungwa inazingatia michakato mbali mbali inayoendelea katika Mji huu kwa sasa, hivyo wananchi wote pamoja na Waheshimiwa Wabunge tuwe na subira. (*Makofi*)

Na. 27

Nafasi Maalum za Ubunge kwa Wazee

MHE. ZAYNAB M. VULU (K.n.y. ENG. STELLA M. MANYANYA)
aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni Wazee wetu waliotumikia nyadhifa mbalimbali za juu katika kuisaidia Serikali pamoja na Bunge katika mambo mbalimbali kama vile Madini na Miswada wamehamasika kuingia katika siasa lakini wanapogombea Ubunge hukumbana na vikwazo vikubwa kutoka kwa vijana wenye nguvu na kasi mpya hata kama hawana ari mpya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga nafasi chache kwa ajili ya Wazee hao kama ilivyo kwa Wabunge wa Viti Maalum?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua nafasi na umuhimu wa michango ya wazee katika maendeleo na ustawi wa Taifa letu kwa kupitia nyanja mbalimbali za kisasa, kiuchumi na kijamii. Serikali inawatambua na kuwaenzi wazee kama nguzo muhimu katika kudumisha maadili, mila na desturi, utamaduni, amani, umoja na mshikamano katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imelipokea wazo la Mheshimiwa Mbunge kama ushauri kwa ajili ya kulifanyia kazi kutokana na ukweli kwamba utekelezaji wa suala hilo unahitaji mashauriano au majadiliano ya kina katika kubaini iwapo kuwapatia wazee nafasi za uwakilishi Bungeni hawatakuwa na fursa ya kuendelea kutoa michango yao muhimu katika jamii. Aidha ni vema ikumbukwe pia kwamba uamuzi kama huo ambao utahusu vyama vyote utahitaji kufanya mabadiliko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo kwa utaratibu wa kidemokrasia yatapaswa kuhusisha mchakato wa ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mwelekeo huo natambua zaidi kwamba wazee ni rasilimali na nguvu muhimu katika maendeleo ye yote. Napenda kulihakikishia Bunge hili Tukufu kuwa, kwa kuzingatia sera ya Taifa ya wazee ya mwaka 2003 kila jitihada itawekwa kuhakikisha kwamba Wazee wanapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na maamuzi katika nchi yetu kwani hekima, busara na uzoefu wao unahitajika sana. (*Makofii*)

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Waziri naomba kuuliza swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa sote tunatambua na ni utamaduni wetu Watanzania kuthamini wazee. Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwa na wazee ndani ya Bunge iwe kama *thinking tank*?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania sote tunatambua busara za wazee na

ndiyo maana Watanzania wamewachagua Wabunge ambao wanawakilisha wananchi wengi hapa Bungeni.

MHE. DR. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza,

Je, wakati haujafika wa kuwa na vigezo vyta Wabunge *specifically* kuliko umri, kwa sababu katika Katiba mwisho wa umri wa mwakilishi ni umri gani?

Je, inakuwaje kama hatuna *definition* hatujui mpaka wa vijana na vijana wengine wanafikiria ni wazee na wazee wengine wanafikiria ni vijana hivi vyote havihitaji *definition*?

NAIBU SPIKA: Je mbili zitaunganishwa ziwe Je moja. (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika Mheshimiwa Getrude Mongella anafahamu fika kwamba yeche ni pamoja na wale wazee ambao tunawataja sasa hivi, kwa sababu sheria za Tanzania zinatambua kwamba Mzee ni mtu mwenye umri wa zaidi ya miaka 60 na tupo wengi humu. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na definition zaidi ya hiyo nadhani siyo suala la msingi tena kwa sababu tuna sheria ambayo kwa sasa ipo na inatambulika. Kwa madhumuni ya wawakilishi hakuna umri uliowekwa. Mbunge anaweza kuwa mtu yeoyote kati ya umri wa miaka 21 na kuendelea.

Na. 28

**Masharti ya Ukopeshaji kwa Wakulima katika Benki
ya Rasilimali ya Taifa.**

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

Katika Mkutano wa 18 wa Bunge, Bunge lilikubali kuongeza shilingi bilioni 19 kutoka akaunti ya *EPA* kwenda Benki ya Rasilimali ya Taifa (*TIB*) upande wa kilimo kwa ajili ya kuwakopesha wakulima, na kwa kuwa mikopo ilikuwa haijaanza kutolewa kwa kuwa masharti ya ukopeshaji yalikuwa hayajakamilika:-

- (a) Je, masharti hayo sasa yamekamilika; na kama jibu ni ndiyo ni yapi?
- (b) Je, kati ya shilingi bilioni 22 zilizotengwa kwa ajili ya wakulima ni kiasi gani kimekopeshwa na ni wakulima wangapi wa Mbozi wamepata mikopo hiyo?

MHE. OMAR YUSSUF MZEE (NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Jimbo la Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Rasilimali ya Tanzania (*TIB*) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na Benki Kuu, imeandaa mwongozo wa ukopeshaji (*lending framework*) na kuitishwa na Serikali mnamo mwezi wa Disemba 2009. Aidha masharti ya ukopeshaji yalikubalika na kuitishwa kama ifuatavyo:-

- (i) Mikopo itatolewa kwa riba isiyozidi asilimia 8 kwa mwaka
- (ii) Mikopo italipwa kwa kipindi cha miezi 6 hadi miaka 15, kutegemea na mahitaji ya mradi na ukubwa wa mkopo.
- (iii) Marejesho yatapangwa kuendana na msimu wa kilimo au mavuno.
- (iv) Dhamana zilizokubalika ni pamoja na ardhi, nyumba, mashine na kadhalika, Hati za Makazi zinazotolewa na MKURABITA zitakubalika kama dhamana ili mradi mkopaji awe ndiye mmiliki wa Hati husika.
- (v) Mkopaji atatakiwa kuandaa mchanganuo wa mradi (*Business Plan*) kabla ya kupatiwa mkopo.
- (vi) Wakopaji wadogo watalazimika kuitisha maombi yao kwenye *SACCOS*, *VICOBA* au Taasisi za Kifedha.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kufikia mwezi Mei, 2010, jumla ya shilingi 2.5 bilioni tayari zimeshaidhinishwa kwa ajili ya kukopeshwa wakulima kutoka katika maeneo mbalimbali.

Aidha, kwa upande wa Wilaya ya Mbozi, takwimu zinaonyesha kuwa hadi sasa ni wakulima watatu (3) tu ndiyo walioomba. Mmoja kati yao ameshindwa kupata mkopo kwa sababu ya ya kutorejesha mkopo mwingine aliopewa na Serikali kuititia mfuko wa pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wawili, wamepatiwa maelekezo na ushauri wa ziada kwa lengo la kuandaa maombi yao kwa uzuri na baadaye kuyawasilisha tena kwa ajili ya uchambuzi.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni kwa sababu gani pamoja na masharti mengine yanayoonekana kuwa mazuri lakini kuweka sharti la kwamba mwombaji lazima apitishe maombi yake kwenye *SACCOS* au *VICOBA*:-

(a) Je, pale ambapo hakuna *SACCOS* au *VICOBA* huyu mkulima atalazimika kufanya nini?

(b) Je, ni lini sasa huduma hii badala ya kuwa Dar es Salaam na kuwagharimu wananchi gharama kubwa kuomba mikopo hiyo kutoka maeneo mbalimbali ya nchi ni lini taasisi hii itapeleka au itakuwa na vituo huko Mikoani ili waombaji wasipate gharama nyingi zaidi kufuata mikopo hiyo Dar es Salaam? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Naibu Spika, kama eneo halina SACCOS au VICOBA mwombaji anaweza kuomba kutumia taasisi nyingine za fedha kama vile community banks. Kama vyote hivyo havipo mwombaji atalazimika kuifuata taasisi ya *TIB* ilipo. Hii ni kwa taratibu za kiusalama wa mfuko huu. Hatuna vinginevyo mpaka sasa hivi.

La pili, Mheshimiwa Zambi ametaka kujua ni lini vituo vitafika Mikoani? Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Zambi kwamba *TIB* sasa hivi ina mpango mzuri katika mwaka wa 2010 itafungua vituo vinne zaidi ili kuweza kuwafikia karibu wanachama / wakulima wote lakini kama nilivyoeleza mkulima anaweza vile vile kutumia Community Banks ambazo katika Wilaya nyingi tayari tunazo *Community Banks*.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masharti hayo ambayo ameyaeleza dhamira ya kuanzishwa kwa dirisha hilo katika *TIB* kwa ajili ya wakulima Serikali hii imewalenga wakulima wakubwa au ilikuwa inafikiria mkulima mdogo mdogo alioko kule Mpanda? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. YUSSUF O. MZEE): Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kuwa-cover wakulima wa aina zote pamoja na wale wadogo na kwa maana hiyo asilimia 30 ya fedha zote zilizoko katika dirisha hili la kilimo ni kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo. (*Makofi*)

Na. 29

Fedha zinazotolewa na Msamaha wa Deni la Taifa

MHE. PAUL P. KIMITI aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi nyingi zimesamehe madeni yetu ambayo tulipaswa kuyalipa kwa miaka mingi ijayo:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichosamehewa wakati wa Serikali ya awamu ya Nne?

(b) Je, matumizi ya Fedha hizo za msamaha yamejenga na kusaidia maendeleo katika nyanja zipi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa nchi yetu imepata msamaha wa madeni tuliyokuwa tukidaiwa miaka mingi iliyopita. Jumla ya dola za Kimarekani bilioni 4.14 tumesamehewa na nchi mbalimbali katika kipindi cha cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi misamaha tunayoipata huwa inalenga katika kutoa nafasi kwa Bajeti ya Serikali kuweza kugharamia sekta ya Maendeleo. Fedha za msamaha hutumika kusaidia miradi ya maendeleo katika nyanja zilizoainishwa ndani ya MKUKUTA kama vile Elimu, Maji, Afya, Kilimo, Nishati na Miundombinu.

MHE. PAUL P.KIMITI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kwa ufupi kabisa.

(a) Kwa kuwa fedha bilioni 4 ni sawa na nusu ya Bajeti ya mwaka mzima huu ingeweza kusaidia mipango mingi sana ya maendeleo. Je, Waziri anaweza kunisaidia kwa nini kipindi hiki kilichopita tumekuwa na tatizo la baadhi ya makandarasi kuacha kuendelea na kazi zao kwa kukosa kulipwa madeni ya shilingi bilioni 305. Serikali inasema nini ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zinalipwa na kama hazilipwi ina mpango gani?

(b) Kwa kuwa sehemu nyingi zimepata misamaha na tunaelewa kwamba misamaha hiyo imesaidia sana katika suala la elimu, Afya, Maji pamoja na Miundombinu. Mheshimiwa Waziri anaweza kunisaidia mgao wa fedha hizo kama hana hata baada ya kipindi hiki akanipa kwa maandishi? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Paul Kimiti kwamba lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba wakandarasi hawa wanalipwa fedha zao.

Lakini tunachokifanya katika kipindi hiki ambacho kimetokana na maelekezo ya Bunge letu Tukufu ni kulipa kwa kutumia ile sera yetu *value for money*.

Kwa maana hiyo kwanza tunathibitisha na tunahakikisha kwamba kazi ambayo imefanywa na wakandarasi hao kuititia ile *certificate* ambayo wamei-*raise* ya malipo tunaiangalia ni sahihi na ndio tunalipa. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba hawa makandarasi ambao hatujawalipa tutawalipa baada ya kukamilisha *value for money exercise*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Paul Kimiti kwamba huo mgao ambao uliotaka kwa sasa sitakuwa nao lakini nitampatia tutakapomaliza.

Fursa Zilizotolewa na Matumizi ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi

MHE. BAKARI SHAMIS FAKI aliuliza:-

Je, Serikali inazitumiaje fursa zinaotokana na matumizi ya maji ya Bonde la Mto Zambezi katika kutekeleza dhana ya Taifa ya Kilimo Kwanza?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kueleza kwamba Kilimo Kwanza ni suala mtambuka kwa sababu ufanisi wake unategemea mchango wa sekta mbalimbali na unaongozwa na nguzo 10 ikiwa ni pamoja na utashi wa kisiasa, kugharamia kilimo, mfumo wa kilimo, upatikanaji wa ardhi ya kilimo, vivutio vya uwekezaji, viwanda, maendeleo ya teknolojia, miundombinu na ushiriki wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji shirikishi tuliyonayo, kwa madhumuni ya kuboresha uhusiano uliopo na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi, kijamii na kisiasa baina ya nchi wanachama, wakuu wa nchi wanachama wa *SADC* walisaini Itifaki ya Maji Shirikishi ya (*Revised Protocol on Shared Water Courses*), Mjini Windhoek, Namibia na kukubaliana kuundwa kwa Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (*The Zambezi Water Course Commission (ZAMCOM)*).

Mkataba huu uliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 8 Februari, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kumjibu Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya fursa zilizopo katika ushiriki wa Tanzania katika Kamisheni ya Mto Zambezi imo katika utekelezaji wa programu na Miradi ya pamoja. Mara nyingi washiriki wetu katika maendeleo wanapenda kufadhili miradi yenyе muundo wa ushirikiano kama huo wa *ZAMCOM* kwa sababu pamoja na kuleta maendeleo, programu hizo zinatuunganisha pamoja.

Kwa mfano, katika Bonde la Mto Zambezi, Tanzania na Malawi zinatekeleza Programu ndogo ya Mto Songwe ambayo itahusu ujenzi wa mabwawa makubwa, kuendeleza heta 6,000 za kilimo cha umwagiliaji katika nchi zote mbili, udhibiti wa mafuriko, miradi ya umeme, uvuvi, utalii na ujenzi wa miundombinu.

Mfano mwingine ni mradi wa pamoja wa umwagiliaji wa *upper Zambezi/Shire* ambao benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) imeonesha nia ya kusaidia. Mradi huu unaohusisha nchi za Msumbiji, Malawi na Tanzania. Aidha, ziko fursa nyingine za kuendeleza umwagiliaji katika Bonde la Ziwa Nyasa ambalo nalo ni sehemu ya Bonde la Mto Zambezi. Miradi tayari imekwishaainishwa katika Bonde la Ziwa Nyasa ni pamoja na Ngana, Kasiabone, Kisegese, Kifunda, Manda, Lifua na Mkiu.

Mheshimiwa Spika, hizo ni baadhi tu ya fursa zilizopo lakini zitakuwapo nyingine kama vile ajira na hifadhi ya vyanzo vya maji na mazingira ambazo zote zinachangia kuendeleza Kilimo Kwanza. Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara nyingine na sekta binafsi kuibua miradi mingine hususan itakavyowashirikisha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa ili wawekeze katika kilimo cha umwagiliaji.

MHE. BAKARI SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna ushauri kwamba katika kutumia fursa zinazotokana na matumizi ya Mto Zambezi Serikali iandae mipango mahususi ambayo itaweza kuinua uchumi wa Mikoa iliyomo katika Bonde la Mto Zambezi.

- (a) Je, Serikali inasemaje kuhusu kutekeleza ushauri huu?
- (b) Kwa kuwa ni hivi karibuni tu Bunge liliridhia Azimio la kuanzisha Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi. Je, kuna changamoto zipi ambazo zinaikabili Serikali katika kupata na kutumia fursa zinazotarajiwaa baada ya kuridhia Azimio hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu mipango mahususi kama nilivyosema katika majibu ya msingi tayari ipo miradi hiyo, program ndogo ya Mto Songwe ni mpango mahususi ambaa unalenga kutumia fursa zilizopo. Nimetaja miradi ya umwagiliaji ambayo tutashirikiana na wenzetu na tunatarajia pia kupata misaada kutoka *ADB* kwa kushirikiana na zile nchi tatu nilizozitaja. Hiyo ni mipango mahususi. Lakini pia nimesema Serikali inaendelea kupanga mipango jinsi muda unavyokwenda maana yake maendeleo ni *process* siyo kwamba tayari sasa tumefika mwisho. Tunataka tutekeleze haya ambayo tayari tumepanga wakati tunapanga mipango mingine. Kwa hiyo, ni *process* ambayo inaendelea.

Kuhusu changamoto mimi ningesema hakujawa na matatizo makubwa kwa sababu sisi wenyewe bado hatujakamilisha kila kinachotakiwa ili kupata misaada hii. Labda changamoto moja tu ambayo ningesema ipo na wenyewe sioni kama ni tatizo kubwa ni kwamba katika nchi 8 ambazo zinatarajiwaa kukamilisha kusaini mkataba huu nchi tano nimesema zimekwisha saini mkataba huo ambazoni Namibia, Tanzania, Angola, Mozambique na Botswana. Nchi za Zambia, Zimbabwe na Malawi bado nazo kutokana na utaratibu wao wa ndani wanajipanga ili waweze kusaini mkataba huu. Kwa hiyo, hiyo ndiyo changamoto ambayo bado tunayo.

Mpango wa Kuepeleka Maji kwa Wananchi wa Masasi

MHE. RAYNALD A. MROPE aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna shida kubwa ya maji safi na salama kwenye Wilaya ya Masasi hususan, Masasi Mjini na Masasi Magharibi; na kwa kuwa, Serikali katika mipango yake ina malengo ya kuapelekeea maji wananchi wake:-

- (a) Je, Mpango mkubwa wa kutoa maji kwenye chemchem ya Mbwinji kuapeleka Masasi Mjini kwa kuititia vijiji vya njiani utakamilika lini?
- (b) Kama hatua ya kuongeza uwezo. Je, Serikali haifikirii pia kupata maji mengi kuititia vyanzo vya chemchem ya Liputu, Mwena, Mwiti pamoja na kufufua Bwawa la Mcchemwa ili kuhakikisha Masasi inapata maji ya kutosha?
- (c) Kwa upande wa Masasi Magharibi; hasa kwenye Vijiji vya Mpanyani, Nambawala, Chikoweti na kadhalika. Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo kubwa la maji kwenye eneo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Wilaya ya Masasi kama zilivyo Wilaya nyingi inakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa maji. Ili kuona ukubwa wa tatizo hili mwezi Novemba 2009 mimi mwenyewe nilifuatana na Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu katika ziara yake Mkoani Mtwara ilijojumuisha pia Wilaya za Masasi.

Katika ziara hiyo Mheshimiwa Mrope, Mbunge wa Masasi alitumia muda mrefu sana kuelezea ukubwa wa tatizo na vyanzo vya maji vilivyopo ambavyo vikitumiwa vizuri vitapunguza tatizo la maji lililopo. Ili kutatua tatizo hili, Wizara yangu imepanga kuendeleza chemchem ya Mbwinji na kujenga mfumo wa usambazaji maji hadi katika Miji ya Masasi na Nachingwea pamoja na Vijiji vilivyoko kando kando ya njia ya bomba kuu.

Mradi huu ambaa ulifanyiwa usanifu mwaka 2005 lakini ukakosa fedha za utekelezaji kutohana na ukubwa wake sasa unatekelezwa katika Programu ya kuendeleza Sekta ya Maji. Hatua iliyofikiwa ni kwamba tathmini ya zabuni ya ujenzi imekamilika na matarajio yetu ni kwamba mkataba wa ujenzi kutiwa saini mwezi Agosti, 2011.

Katika kuharakisha utekelezaji, Wizara yangu imeamua kumtumia Mhandisi Mshauri anayesimamia mradi wa jamii wa Mtwara ili asimamie pia mradi wa Mbwinji.

Matarajio yangu ni kwamba ujenzi wa mradi huu sasa utakamilika mwezi Desemba, 2011.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tangu mradi wa maji wa Masasi- Nachingwea ufanyiwe utafiti mwaka 2005 kumekuwa na ongezeko kubwa la watu katika Miji hiyo na vijiji vilivyo kando ya njia ya bomba kuu. Kwa sababu hii, Wizara inafanya uchunguzi wa vyanzo vingine ikiwa ni pamoja na chemchem za Liputu, Mwena, Mwiti na kuchunguza uwezekano wa kukarabati na kuboresha bwawa la Mchemwa ambalo limechakaa. Namshukuru tena Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Wizara katika kuanisha vyanzo hivi.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, ni moja kati ya Halmashauri 91 zilizokamilisha taratibu za kuajiri mtaalam mshauri na kupata kibali cha Benki ya Dunia kusaini mkataba. Vijiji vya Mraushi, Lilala, Mihina, Nambawala na Mtakuwa ni mionganini wa Vijiji 10 ambavyo sasa vinafanyiwa usanifu.

Ujenzi wa miundombinu ya maji unatarajiwa kuanza mwaka 2010 /2011. Nampongeza Mheshimiwa Raynald Mrope na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa hatua iliyofikiwa na ninaomba Halmashauri kuviveka vijiji vya Mpanyani na Chikowetu katika mpango wake wa maendeleo ya mji ili navyo vifikiriwe kupata huduma hiyo.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa majibu mazuri kwa swali langu ambalo limeleta matumaini makubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Masasi.

(a) Kwa upande wa Massasi Magharibi Waziri amevitaja vijiji vitano kwamba vitasaidiwa na mpango wa Benki ya Dunia je, kuna mpango gani wa kuvihudumia pia vijiji vilivyobaki ambavyo ni vingi zaidi?

(b)Mpango wa kuleta maji Masasi kwa bahati mbaya umechelewa kwa muda mrefu sasa.

Kwa kuwa mwaka huu ni wa Uchaguzi, tayari wapita njia wanajinadi kwamba wataleta maji ya kutosha Masasi.

Sasa Mheshimiwa Waziri naomba uliahidi Bunge hili pamoja na wananchi wa Masasi kwamba danganya toto ya namna hiyo haitaweza hata kidogo kuleta maji Masasi na kwamba nje ya mpango huu mambo mengine yote ni geresha tu. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mrope kama ifutavyo.

Kuhusu vijiji vile ambavyo sikuvitaja hapa chini ya mpango wa vijiji kumi. Naomba nimhakikishie kwamba haya ni maendeleo na maendeleo ni *process* ni mchakato sio matukio.

Kwa hiyo, sasa tumeanza na vijiji hivyo vitano katika Jimbo lake lakini kuna awamu nyingine itakayofuata . Kwa hiyo, naendelea kuiomba Halmashauri hiyo hivyo vijiji vingine ambavyo havimo katika utaratibu wa vijiji kumi viwekwe katika mipango yao ya maendeleo ya maji.

Lakini pia naomba nishauri kwamba wanayo nafasi kutumia fursa zingine za vyanzo vya fedha zilizopo kwa kutumia vyanzo kama mashirika ya dini, *NGO's* na wengine na kule Wilayani Masasi mimi nina hakika kabisa najua kanisa la Anglikana tayari linasaidia kutekeleza baadhi ya miradi hususani katika kijiji kimoja kinaitwa Mkwapo.

Kwa hiyo, hizo ni fursa ambazo pia zinaweza zikatumika kuweza kuendeleza hivyo vijiji vingine ambavyo bado havijaendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili kuhusu hii aliyosema danganya toto ya hawa wengine wanaopitapita mimi nataka nimhakikishie kwamba kama nilivyosema maendeleo ni *process* na mipango hii ni mikubwa, mradi huu wenyewe unatarajia kutumia kama bilioni zaidi ya thelathini na moja, hizi ni fedha nyingi hakuna mtu mmoja kati yetu anaweza kwenda akasema mimi napeleka bilioni thelathini na moja kwenda kuendeleza mradi wa Nachingwea na Masasi.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba Serikali imeshaweka utaratibu huu na tunaendelea kutekeleza ilani hii kama tulivyojiwekea wenyewe na hii ni *process*, ni mchakato endelevu. Naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Spika wa Maji.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji na tatizo la maji au changamoto ya maji hakika ni kero namba moja, naomba kutumia nafasi hii kuwahakikishia wananchi wa Tanzania kwamba kwa uzoefu wangu katika Wizara hii Wabunge wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania hawa niliofanya kazi pamoja nao kila mmoja wao amefanya kazi kubwa kweli katika kuendeleza shughuli zinazohusiana na maji, hilo naweza kudhibitisha.

Kuhusu mradi ya Mbwinji, Masasi na Nachingwea hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa wananchi wa Masasi na wananchi wa Nachingwea, tunaitekeleza na kama alivyojibu vizuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri, matarajio yetu ni kwamba mwezi Agosti tutatia saini mkataba wa ujenzi, hata kama tutakuwa katika shughuli zetu za uchaguzi. Mimi nina uhakika kwamba sherehe hiyo itahudhuriwa pia na Waheshimiwa Wabunge wa Masasi na Nachingwea na mimi nitatoka Rungwe Mashariki kushuhudia.

Elimu Juu ya Soko la Afrika MasharikiI

MHE. JACKSON M. MAKWETTA (K.n.y. MHE. YONO STANLEY KEVELA) aliuliza:-

Kwa kuwa, Soko la Pamoja la Afrika Mashariki bado halijaeleweka vizuri kwa wananchi hasa upande wa Tanzania.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaelimisha wananchi juu ya soko hilo la pamoja na Tanzania itafaidika vipi na soko hilo la Afrika Mashariki?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa ikitoa elimu kwa umma kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na vipindi vyta redio, runinga, makala, vipeperushi, majarida, semina, mikutano, maonyesho ya nane nane na makongamano.

Vile vile, Wizara imeyapatia elimu makundi mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Makatibu wakuu na Makatibu Tawala wa Mikoa, Wafanyabiashara, Wahariri wa Habari, Wanafunzi wa Vyuo Vikuu na wananchi kwa kutumia vyombo vyta habari. Aidha ziara mbalimbali zenye lengo la kutoa elimu kwa Umma zimefanya katika maeneo ya Kigoma, Mwanza, Bukoba, Dodoma, Shinyanga, Tabora, Kilimanjaro, Iringa, Morogoro, Rukwa, Singida, Mbeya, Ruvuma, Arusha, pamoja na Zanzibar na ziara katika mipaka ya Namanga, Sirari, Holili na Mtukula kwa lengo la kuwaelimisha wananchi na watendaji kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wizara kuweka juhudini za wazi kabisa katika kuhakikisha kuwa elimu kuhusu Soko la Pamoja na Hatua zingine za Mtangamano inawafikia wananchi kwa kiwango cha kuridhisha inaonyesha kuwa elimu hiyo haijawafikia wananchi wengi kufikia kiwango kinachohitajika.

Hivyo basi, Wizara kwa kutambua hilo imejipanga vyema kuhakikisha kuwa elimu kuhusu Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Hatua zingine za Mtangamano zinawafikia wananchi kwa kiwango kinachotakiwa kwa kufanya yafuatayo:-

1. Wizara imeandaa Mpango kabambe wa kutoa Elimu kwa Umma ambao ulizinduliwa rasmi mwezi Mei, 2010. Lengo la mpango huu ni kuhakikisha

wananchi wengi wanapata elimu kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutumia njia mbalimbali kama vipindi vya redio, runinga, nyimbo, maigizo, michezo ya redio, matamasha, vipeperushi, semina, mabango, makongamano, mikutano, makala na majarida.

2. Wizara imefanya mazungumzo ya awali na TAMISEMI kwa ajili ya kuweka mfumo wa ushirikiano utakowezesha Wizara kuzitumia Halmashauri katika kutoa elimu kwa umma katika maeneo yao.
Aidha utaratibu huu utajenga mfumo endelevu wa kutoa elimu kwa Umma ambapo wataalam mahususi watakaoeuliwa katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa watakuwa viungo baina ya Wizara na maeneo yao.
3. Kuimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano kwa kuongeza idadi ya watumishi pamoja na kukipatia kitengo vitendea kazi kwa ajili ya kukijengea uwezo kitengo ili kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi katika kuhakikisha taarifa mbalimbali zinawafikia wananchi wa Tanzania ili waweze kutumia vyema fursa zitokanazo na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutekeleza Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, Tanzania itanufaika zaidi na fursa zitokanazo na ushirikano wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo soko kubwa la bidhaa, mitaji, huduma na ajira. Vile vile kutoa fursa zaidi za uwekezaji pamoja na ushirikiano katika nyanja za kiuchumi na kijamii.

Na. 33

Matukio ya Ubakaji na Mauaji ya Watoto Mbeya

MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI aliuliza:-

Siku za hivi karibuni kumekuwa na matukio ya ubakaji na mauaji ya watoto wadogo katika Wilaya ya Rungwe na maeneo mengine Mkoani Mbeya, uhalifu amabo unakiuka haki za watoto na za binadamu.

Je, ni wahalifu wangapi wamekamatwa kuhusiana na uhalifu huo na ni hukumu gani imetolewa juu yao ili kukomesha kabisa vitendo hivyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kati ya tarehe 14 Mei, 2010 katika Wilaya ya Rungwe Mkoa wa Mbeya kumejitokeza matukio sita (6) ya mauaji ya kikatili ya watoto wa kike wenye umri kati ya miaka miwili hadi mitano.

Matukio hayo sita ya mauaji yamekuwa yakifanyika kwa mbinu (*modus operandi*) ya aina moja kwani kabla ya watoto hao kuuawa wote walibakwa na kunyongwa shingo. Upelelezi wa awali umeonyesha kwamba mauaji hayo yanahusiana na imani za kishirikina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 31 Mei, 2010 jumla ya watuhumiwa 21 walishakamatwa na kufikishwa mahakamani kuhusiana na mauaji hayo. Hadi sasa hajitatolewa hukumu yoyote.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini kwa masikitiko makubwa sana naomba kulaani mauaji hayo na ubakwaji kwa watoto wasio na hatia. Naamini Wabunge wenzangu wote wataungana na mimi kulaani kitendo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba upelelezi wa awali umeonesha kwamba mauaji haya yanahusiana na imani za kishirukina na kwa kuwa mauaji hayo ya watoto wasio na hatia yametuathiri sana sisi wazazi.

Je, Serikali itakubalina na mimi kwamba kesi hii iendeshwe haraka haraka ili wauaji hawa waweze kupatiwa hukumu inayo stahili ili kukomesha ukatili huu usitokee tena sehemu nyingine?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, hakika naungana na Mheshimiwa Mbunge Faida Mohamed Bakari kwamba Serikali kwa kauli moja ina laani vitendo kama hivi. Ni vitendo vya kizalimu ni vitendo ambavyo vinaipaka nchi yetu au Taifa letu matope na kutudhalilisha kwa kweli mbele ya umma uliokuwa mkubwa na mbele ya ulimwengu kwa sababu ni vitendo si vya utu hata kidogo. Na tunafanya kila jitihada katika kufanya upelelezi na kuhakikisha kwamba hizi kesi zinifikishwa mahakamani na mahakama ichukue mkondo wake kuhusu wadhalimu hawa.

MHE. FLORENCE E. KYENDESYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona ili na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa suala hili la hawa wanaume kuwabaka watoto wadogo kikatili na kinyama kwa kuwanyonga shingo, imeleta simanzi sana kwa wananchi wa Wilaya ya Rungwe Mkoa wa Mbeya na Taifa kwa jumla.

Kwa kuwa hawa watu waliofanya vitendo hivi baadhi yao wameshakamatwa, kwa nini upelelezi unasuasua. Kwa nini usifanyike haraka ili hawa wapate hukumu

inayostahili na liwe fundicho kwa watu wengine na hii inaweza ikarudisha angalau imani ya wananchi kwa Serikali yao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kutuhukumu kwamba Serikali katika upelelezi wake inasuasua niseme kwamba Mheshimiwa Mbunge inaonekana hivyo katika dhana ya mtizamo lakini kiuhakika ni kwamba suala la mauaji ni suala la mauaji, ni suala ambalo linaenda *High Court*, Mahakama Kuu.

Lakini kabla halijafika kule inabidi lipite katika taratibu lianzie katika mahakama ya Wilaya na mpaka tupate ushaidi wa kutosha kwa maana ya kusema kwamba yule mtu kweli sisi katika macho yetu anaweza kuwa ametenda kosa na kweli tunaona kwamba ni kosa lakini kwa muujibu wa sheria tulizojiwekea sisi inabidi tufuate taratibu zile za sheria kwa maana ya kusema kwamba tuanzie katika mahakama ya kwanza mpaka tuje kufika katika mahakama ambayo ndio itastahili kusikiliza masuala ya mauaji.

Ningeomba tu kwamba ieleweke kwamba hapa hakuna dhana yejote ya kusema kwamba tuna sua sua lakini tunakwenda kwa mujibu wa sheria ambazo tumejiwekea sisi lakini bado nitarejea kusema kwamba Serikali ina laani vitendo hivi ambavyo vinafanyika kwa wananchi wetu.

Na. 34

Kenya Kufunga Mapito ya Wanyama Katika Hifadhi zao za Taifa

MHE. MICHAEL L. LAIZER aliuliza:-

Kwa kuwa maji na wanyama katika Hifadhi ya Taifa ya Amboseli (*Amboseli National Park*) ya Kenya vinatoka katika Mlima Kilimanjaro na kwa kuwa Kenya wamefunga mapito yote ya wanyama kutoka nchini kwao na hivyo kubaki na mapito ya *Kitenden Corridor* na *Arusha National Park Corridor*:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzieleza nchi jirani amabzo zimeharibu mazingira yao na kutegemea mapito ya wanyama ya Tanzania tu?

(b) Kwa kuwa wanyama wanaopita mapito hayo wanaharibu mashamba kwenye Wilaya ya Longido na Rombo. Je Serikali ya Tanzania na ile ya Kenya ziko tayari kuwalipa fidia wananchi waliopata hasara?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILII NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, mbunge wa Longido, naomba kutoa maelezo mafupi ya awali kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna taarifa zinazotokana na utafiti katika mfumo wa Ikolojia wa Amboseli nchini Kenya na Kilimanjaro, Tanzania unaonesha kuwepo na ongezeko kubwa la idadi ya watu na matumizi ya Ardhi kwa shughuli za kilimo na makazi. (*Makofii*)

Aidha,kwa upande wa Kenya mashamba yanayomilikiwa na watu binafsi yana uzio jambo ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza mapito ya wanyama.

Kwa kawaida katika maeneo hayo, wanyamapori huvuka mipaka ya Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro na Amboseli kwenda na kutoka Hifadhi ya Taifa ya Arusha kuitia vishoroba vya Kitendeni, Enduimet WMA, *West Kilimanjaro Ranch/Mkuu Estates* na vijiji vya Kisimiri Juu na Kisimiri Chini.

Tafiti za karibuni zinaonesha kuwa Kishoroba cha Kitendeni ndicho pekee kilichobakia katika mfumo wa Ikolojia wa Amboseli na Kilimanjaro kinachoruhusu wanyamapori kutoka upande mmoja kwenda mwingine. Aidha, upana wa kishoroba hicho nao umepungua kutoka upana wa kilomita 21 mwaka 1952 hadi kilomita 5 kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa mapito ya wanyamapori imeyatambua na kuyaingiza katika sheria mpya ya wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009 ili kuyalinda kisheria.

Aidha, kwa kushirikiana na wananchi na wadau wengine imewezesha kuanzishwa *Worldlife Management Area (WMA)* ya Enduimet amabyo itasaidia kuboresha mapito ya wanyamapori. (*Makofii*)

Serikali pia imewahamisha wananchi na viongozi wa Wilaya ya Arumeru hususan vijiji vya Kisimiri juu na Kisimiri Chini kutengeneza mipango bora ya matumizi ya Ardhi (*Land Use Plan*) ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo ya ardhi ili kufungua mapito ya wanayamapori na kupunguza migongano kati ya binadamu na wanyamapori. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ya Tanzania hutumia vikao na mikutano kati yake na nchi jirani hususan Kenya kuelezea athari za kuharibu mapito ya wanyamapori. Katika mkutano uliofanyika Narok nchini Kenya tarehe 1Julai, 2009 mpaka tarehe 5 Julai, 2009 ilikubaliwa kuwa Serikali ya Kenya ifanye jitihada kufufua mapito ya wanyamapori ikiwemo kununua ardhi iliyokwisha kukaliwa na wananchi.

Vile vile, Serikali za Tanzania na Kenya zinashirikiana kwa pamoja katika suala zima la uhifadhi wa mfumo wa ikolojia wa Amboseli na Kilimanjaro kupitia mpango wa UNESCO unaoitwa *Biosphere as a learning laboratory for sustainable development in Africa*. Kupitia mpango huu, Mikutano mbalimbali ya wadau inafanyika pamoja na elimu kwa uma kutolewa.

(b) Serikali ya Tanzania inao utaratibu wa kulipa kifuta jasho kwa wananchi ambao mashamba yao yameharibiwa na wanyamapori. Kwa utaratibu huu, kiasi cha shilingi 100,000 hulipwa kwa muathirika ambaye shamba lake linazidi eka moja.

Kwa mfano Seriakli kwa mwaka huu wa fedha 2009/2010 imeshalipa jumla ya Tshs 109,100,000 kama kifuta jasho katika maeneo mbalimbali nchini na mchakato wa kulipa wananchi katika maeneo mengine yanayozidi kuharibika kila siku unaendelea.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa *Nationla Park* ya Amboseli iliyoko Kenya wenye wamefunga mipaka. Kwa hiyo, *Nationla Park* hiyo inategemea mapito yanayotoka Kenya ndio wanafaidi *National Park* yao.

Je, Serikali inaonaje ikiwa wao Wakenya wameiu *Nationla Park* yao, sisi tuihifadhi *Nationla Park* ya nchi nyingine. Je Serikali inaona hali hiyo ni haki?

(b) Kwa Kuwa wenzetu wamefunga mipaka yao na kuongeza wingi wa wanyama kupita katika mapito yaliyoko Tanzania, na kusababisha uharibifu wa mashamba mwaka huu mashamba yote yaliyolimwa yameliwa na wanyama.

Je, Serikali itachukua hatua gani kwa sasa kuwanusuru maisha ya hao wananchi ambao mashamba yao yote yameliwa? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, ambaye mimi namwona ni Mbunge Mhifadhi, kwa sababu kwa kiasi kikubwa maoni yake yamekuwa yakitusaidia sana katika kujadiliana na wenzetu hasa nchi jirani. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba, ushauri wake daima tutakuwa tukiufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pendekemo lake la swali la kwanza kwamba kwa kuwa wenzetu wameshafunga mipaka, wameshafunga njia za mapito ya wanyama na kwa maana hiyo uwepo wa Hifadhi ya Mboseli unatutegemea sisi, kwa nini sisi tunawasaidia. Niseme tu kwamba, hawa wanyama hawana mipaka. Wanyama wanakuwa Mboseli kwa wakati fulani, wanakuwa *Kilimanjaro National Park* kwa wakati

mwingine. Kwa maana hiyo si rahisi kusema kwamba, wanyama hawa ni wa Kenya kwa maana hiyo tukifunga na sisi tutaathirika kwa sababu *eco-system* ni ile ile. Kwa hiyo, tunafikiri njia nzuri zaidi ni kuendelea kuwa na jitihada za pamoja kuhakikisha kwamba, wanyama na *eco-system* nzima inalindwa kwa sababu faida si kwa wanyama peke yake lakini pia kuna viumbe vingine hai vingi tu ambavyo vinategemea uwepo wa misitu na uwepo wa Shoroba kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, tunafikiri ni vizuri tuendelee kuzungumza na wenzetu kuliko kufanya *retaliative actions* kwa upande wa kwetu, kwa kufunga njia au kufanya kingine cha kufanana na hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swal lake la pili kwamba, maeneo mbalimbali ya wananchi makubwa sana yameharibiwa na kwa maana hiyo Serikali inafanya nini. Kama nilivyosema kwenye jibu letu kwamba, Serikali daima imekuwa ikishirikiana na wananchi na tuna mwongozo ambao tunatumia kwa sasa hivi kwamba, pale ambapo uharibifu umetokea kwa shamba linalozidi ekari moja, tunatoa kifuta machozi na nimesema pia kwamba, tayari tumekwishatoa zaidi ya milioni 109 kwa mwaka huu wa fedha tulionao na bado tunaendelea ku-*process* maombi mengine au tuseme *claims* nyingine ambazo ziko kwenye maeneo ambayo yameharibiwa siku za karibuni. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo, ingawa mzigo unakuwa mkubwa. Ndiyo maana kwenye Sheria mpya ya mwaka 2009, Sheria Namba 5, tunesema tutajaribu kuwa na mpango mzuri zaidi wa kubainisha *corridor, dispersal areas* ili *conflict* kati ya binadamu na wanyama ziweze kupungua.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, tunatumia muda wa mwanzo kufidia.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana majibu mazuri na maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba niulize swal la nyongeza.

Kwa kuwa kuna *guidelines* au utaratibu wa kuendeleza rasilimali zilizo mpakani mwa Nchi za Afrika Mashariki hususan Kenya, Uganda na Tanzania, yaani *guidelines for development of trans-boundary resources*; kwa nini tatizo linalojitokeza kwenye eneo hilo lisizingatie au kutumia utaratibu wa *guidelines* hizo ambazo ziliandaliwa na ninaamini zimepitishwa na Nchi za Afrika Mashariki kwa ajili ya kulinda na kutumia kwa utaratibu endelevu rasilimali zilizo mpakani mwa nchi zetu? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia Sekta ya Wanyamapori, miongozo mingi iliyopo inatumika ikiwa ni pamoja na suala hili. Tatizo ambalo lipo ni Sheria inayotawala eneo ambalo liko nje ya hifadhi ambalo ni pamoja na Shoroba. Hapo ndiyo tunapokuwa na tatizo, kwa sababu mara nyingi Sheria zinazotawala maeneo hayo zinakuwa ni nyingine. Kwa ujumla ni kwamba, Sheria, *Guidelines*, pamoja na miongozo mbalimbali zinatumika. Ninafikiri ni vizuri nikamhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika miongozo ambayo tunaitumia ni pamoja na *guidelines for development of trans-boundary resources* kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda pia umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na shughuli, tunao wageni ambao wamelitembea Bunge hili asubuhi hii. Kwanza kabisa ni mgeni wa Mheshimiwa Shah, ambaye ni Sheikh Ally Mwabaku, Imamu Mkuu wa Msikihi Mkuu Mafia. Sheikh yuko wapi? Nadhani atakuja kesho sijamwona. (*Makofi*)

Haya, tunaendelea. Aah Sheikh yuko pale, karibu sana. Yuko Sheikh na wageni wengine wa Mheshimiwa Shah.

Vilevile tuna wageni wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni, ambao ni mtoto wake, Majid Hamad Rashid Mohamed na rafiki yake. Huyu Majid anasoma Chuo Kikuu cha Monash, kilichoko Afrika Kusini. Yuko wapi, aah yuko pale, karibu sana. Yupo na rafiki yake anayeitwa Adil Ebrahim Ponnurangam kutoka Chuo Kikuu cha J.A.M.K. kilichoko Finland. Karibuni sana, someni kwa bidii sana na bila elimu hakuna maendeleo.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, wao ni wanafunzi wa tano kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha IMF Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Amiri Madega. Wanafunzi wa Chuo cha IMF, karibuni sana. Tunashukuru sana kwa kuweza kupata nafasi hii.

Halafu pia tuna wanafunzi 12 kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi, Dar es Salaam. Wako wapi wanafunzi wa Ardhi? Aaah tunashukuru sana, mnahitajika sana kuipima nchi yetu kusudi watu waweze kuitumia kwa faida yao. Ahsanteni sana.

Hatuna orodha nyingine ya wageni, kwa hiyo, matangazo ya kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Alhaj Mohammed Missanga, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa, watakutana leo tarehe 11 saa tano asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa ili kukamilisha shughuli za kujadili Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Miundombinu. Kwa hiyo, Wajumbe wote waende saa tano katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Cheyo, anaomba niwajulishe Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa, kuna Kikao cha Kamati leo kuanzia saa 7.30 mchana katika Ukumbi Na. 231, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala. Kwa hiyo, hawa ni saa 7.30, ile Kamati nyingine ni saa 5.00.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo ya kazi. Tunaendelea na shughuli nyingine.

Kama mliviyotangaziwa jana na Mheshimiwa Naibu Spika kwamba, nitawaita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Bajeti na Hotuba ya Mipango, atawasilisha kwa dakika 30, halafu tutamwita Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani, naye atapewa

dakika 30 kutokana na mabadiliko tuliyoyafanya. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika na mambo haya ya Mipango, Mheshimiwa Dr. Kigoda.

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2009 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi, ilipokea na kujadili Taarifa za Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2009, Mwelekeo katika kipindi cha Muda wa Kati (2010/2011 - 2012/2013), ikifuatiwa na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2010/2011. Kamati imezipokea taarifa hizi kama mkakati wa Serikali wa kuinua Uchumi, wapi itapata mapato na matumizi yatakuwaje, pamoja na changamoto zilizojitokeza na zile ambazo zinatarajiwu kujitokeza. Kamati inampungeza Mheshimiwa Mustafa Mkulo (MB), kwa umakini na usikivu wake, pamoja na watendaji wake wa Wizara kwa kuandaa Taarifa ya Hali ya Uchumi na Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa limepita katika kipindi kigumu kilichoambatana na mtikisiko mkubwa wa uchumi Duniani, ambao uliathiri kwa kuporomoka bei za mazao yetu ya biashara, kupungua kwa uwekezaji wa mitaji, kupunguzwa kazi kwa wafanyakazi Sekta ya Utalii, kuongezeka kwa riba za mikopo kutoka nje na kupungua kwa mapato ya kodi. Hali hii iliifanya Serikali iandae mkakati wa kunusuru Uchumi uliokadirwa kugharimu shilingi 1.7 trilioni na hadi Machi 2010, shilingi 1.2 trilioni sawa na asilimia 71.3 ya fedha zimekwishatolewa. Kamati inampungeza Serikali kwa hatua iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, bado Uchumi wetu unatakiwa kukua kwa viwango vya juu asilimia 8 na zaidi ili kupunguza umaskini wa wananchi. Pato la Taifa lilikuwa kwa asilimia 6 mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 7.4 mwaka 2008. Ukuaji wa shughuli za kilimo ulishuka toka asilimia 4.4 mwaka 2008 hadi asilimia 3.2 mwaka 2009. Mfumko wa bei ulifikia asilimia 9.4 Aprili 2010 ukilinganishwa na asilimia 10.3 mwaka 2008. Chakula bado kiliendelea kutoa mchango mkubwa katika mfumko wa bei ikimaanisha tuendeleze juhudzi za uzalishaji wa chakula. Kwa upande wa Sekta ya Fedha, viwango vya riba bado viko juu hivyo kuendeleza tatizo la ughali wa mikopo kwa wananchi wanaotaka kutumia vyombo na taasisi zetu za fedha. Hadi kufikia Machi, 2010, Serikali ilikusanya mapato ya ndani kiasi cha shilingi trilioni 3,4 au asilimia 91.3 ya lengo. Makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi yalifikia kiasi cha shilingi bilioni 160, sawa na asilimia 80 ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010, misaada na mikopo ya Bajeti (*GBS*) iliyopokelewa ilikuwa kiasi cha shilingi. 999,676

milioni, sawa na asilimia 84 ya misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilifikia shilingi trillioni 1.3, sawa na asilimia 93 ya lengo. Kwa upande wa matumizi, kuanzia Julai, 2009 hadi Machi, 2010 matumizi yalifikia kiasi cha shilingi trillioni 6 ikiwa ni asilimia 91 chini ya makisio. Kati ya fedha hizi, kiasi cha shilingi trillioni 4 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trillioni 1.9 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuongezeka kutoka Dola za Kimarekani trillioni 2 mwaka 2008 hadi kufikia Dola za Kimarekani trillioni 3.5 Desemba 2009. Ongezeko hili ni asilimia 23.6. Akiba hii inatosheleza kuagiza bidhaa na huduma nje kwa muda wa miezi 5.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009, Benki ya Rasilimali Tanzania imeanza kutoa mikopo ya muda mrefu; *Tanzania Mortgage Refinance Company* imeanzishwa; Serikali inaendelea na mchakato wa *Credit Reference Bank* na kuanzisha ofisi itakayoshughulika na masuala ya taarifa za mikopo; Serikali imekamilisha maandalizi ya sheria na kanuni za kuboresha mifuko ya jamii; serikali pia inajiandaa kutumia mfumo wa malipo ya TISS. Haya ni mafanikio katika maboresho ya Sekta ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunaendelea na upungufu wa nakisi ya urari wa bidhaa, huduma na uzalishaji mali toka Dola za Kimarekani milioni 2883 mwaka 2008 hadi Dola za Kimarekani milioni 2,208 mwaka 2009. Thamani ya bidhaa na huduma tulizoagiza kutoka nchi za nje zililipungua kwa asilimia 7.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mipango ya Muda wa Kati na Mrefu umeendelea na tathmini kufanyika, Dira ya Taifa ya Maendeleo, MKUKUTA na Malengo mengine yamekuwa yakitekelezwa kama Hotuba ya Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi ilivyoelezea. Hata hivyo, bado Tanzania hatujapiga hatua kubwa katika uendelezaji wa Sekta Binafsi. Uamuzi wa Serikali kuandaa Sera, Sheria na hatimaye Kanuni za *Public Private Partnership (PPP)*, pamoja na Programu za Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara (MKURABITA) na Mkakati wa Kuendeleza Sekta Binafsi (*PSDS*) zinatarajiwu, ikiwa umakini utazingatiwa, utaendeleza sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo moja muhimu ambalo limekuwa likifuatiliwa mwaka 2009, lakini bado halijapewa umakini ni lile la uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Eneo hili limekosa uratibu na usimamizi mahiri. Baraza la Taifa la Uwezeshaji (*NEC*) halijapewa nguvu kisheria (halina meno). Matokeo yake programu hii haijaonesha mafanikio makubwa hasa ikizingatiwa kuwa idadi kubwa ya wananchi wanahitaji kuwezeshwa kiuchumi. Aidha, zipo baadhi ya sera, sera za kifedha na zile za ardhi ambazo zinahitaji kuhuishwa ili kuingia kusaidia eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukijiwekea misingi na malengo ya uchumi na maendeleo ya jamii kwa kipindi cha miaka mitatu pamoja na malengo ya uchumi jumla na maendeleo ya jamii. Kamati inaendelea kuishauri Serikali maoni yanayotolewa

na Kamati yazingatiwe na yatasaidia katika kufikia malengo tuliyojiwekea, pamoja na wananchi kushiriki katika kujenga uchumi wetu na huduma za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imejadili na kutathmini Taarifa ya Hali ya Uchumi, utekelezaji wa Serikali kwa mwaka 2009/2010 na mchanganuo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/2011. Maoni na ushauri wa ziada wa Kamati kwa Serikali ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeendelea kutafakari kwa kina kwa nini Serikali bado hajawenza kujikusanya mapato yake kikamilifu yanayotegemewa katika Bajeti ya Serikali. Mfumo iliyojiwekea Serikali unaweza kuwa ni sababu ya uwezo mdogo wa Serikali wa kudhibiti vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni dhahiri vingeboresha Bajeti ya Nchi. Wakati wa mchakato wa Bajeti, inaonekana Serikali bado hajawenza kuyafikia maeneo mengine ambayo yanaweza kuwa vyanzo muhimu vya kugharimia (*finance*) Bajeti yake.

Matokeo ya hali hii ni uwezekano wa kung'ang'ania (*concentrate*) vyanzo vichache vya kila siku/mwaka na baadae kujenga kero kwa wananchi. Kwa mfano, wafanyabiashara, wafanyakazi na hata wakulima kulipia viwango vya juu vya kodi. Hali hii itaongeza gharama ya kufanya biashara nchini (*high cost of doing business*) kwa sababu ya viwango vya juu vya kodi. Aidha, itachochea ubadhirifu (*resorting to secondary incomes*), kuongeza tatizo la kuepuka kulipa kodi (*tax avoidance*), kukwepa kulipa kodi (*tax evasion*) na hata rushwa. Hii ni changamoto kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya Serikali ni zaidi ya mapato inayokusanya. Hali hiyo inajionesa katika bajeti iliyopita 2009/2010. Katika bajeti iliyopita, mapato ya Serikali yalikuwa kiasi cha shilingi trilioni 3.4 (asilimia 91.3 ya lengo) na matumizi yalikuwa shilingi trilioni 6.1 (sawa na asilimia 91.4 ya makadirio). Katika Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2010/2011, Sera za Mapato zinalenga kukusanya kiasi cha shilingi trilioni 11.1; kati ya hizo, shilingi trilioni 6 ni mapato ya ndani na matumizi ya kawaida yatakuwa shilingi trilioni 7.8 na matumizi ya maendeleo yatakuwa trilioni 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Kibajeti unakuwa ni wa Serikali kutumia zaidi badala ya kuzalisha. Uwiano wa mapato na matumizi katika Mwaka 2007/08 na Pato la Taifa ulikuwa mapato asilimia 15.9 wakati matumizi yalikuwa asilimia 22. Mwaka 2008/09 hali ilikuwa mapato asilimia 16 ikilinganishwa na asilimia 25.

Mwaka 2009/10 ilikuwa asilimia 16 ikilinganishwa na asilimia 24 na mwaka 2010/11 hali hii inatarajiwu kuwa asilimia 17 ikilinganishwa na matumizi asilimia 26. Uchumi wetu unaashiria utumiaji mkubwa ikilinganishwa na tunavyozalisha (*net consumer nation*). Jitihada kubwa ziongezwe katika kuboresha maeneo ya uzalishaji mali moja kwa moja, kwa maana ya *directly productive sectors*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuainisha matumizi ya Serikali na uwezo wa kuamsha mapato. Serikali ichunguze matumizi yake na kuhakikisha kuwa, yanakuwa ni matumizi ya kimkakati. Uzoefu tulioupata katika kipindi cha

2009/2010 na picha inayojionesha tunapoelekea 2010/11 ili tutekeleze vyema malengo yetu ya mpango na kujenga uchumi. Kamati inashauri Serikali kuja na mkakati wa makusudi wa kupunguza matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima (*cost cutting measures – expenditure cuts*). Ni changamoto kwa serikali sasa kuona mikutano, warsha na semina gani zinazoweza kufanyika, matumizi ya magari, mafuta, samani na posho.

Katika bajeti ya mwaka 2010/11, vipo viashiria vinavyoonesha upungufu wa mapato, upungufu wa misaada na malipo kutoka nje. Hatua hii itasaidia Bajeti ya Serikali kuwa endelevu na vile vile kuepuka *deficit financing* ambayo inaweza kuongeza athari za mfumko wa bei katika uchumi wetu. Eneo hili likidhibitiwa, litaleta tija (*efficient expenditure cuts*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeona kuwa, mapato yetu ya ndani yanaweza kuongezeka ikiwa hatua mbalimbali zifuatazo zitachukuliwa:-

Upo umuhimu mkubwa wa kuangalia eneo la sera na uendeshaji wa taratibu za kukusanya kodi. Ni matumaini yetu kuwa, *TRA* itaimarisha jitihada zake za kuendeleza mpango wake mkakati wa kuboresha ukusanyaji wa kodi. Kwa mfano, tunapoangalia makadirio ya mapato ya mwaka 2010/11, ongezeko la ushuru wa bidhaa utakuwa ni mdogo kutoka shilingi 978,025.9 billioni hadi kufikia trilioni 1.1, ongezeko dogo la shilingi 84,969.9 bilioni. Ushuru wa bidhaa unatokana na uzalishaji wa viwanda. Viwango hivi vidogo vinaashiria vile vile uzalishaji mdogo katika viwanda vyetu au makusanyo dhaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imegundua kuwa, kuna ongezeko kubwa la uanzishwaji wa Mashirika ya Umma kuititia kivuli cha Mamlaka (*Agencies*). Hadi sasa Mashirika chini ya *Public Corporation Act* na *Authorities* hivi sasa idadi yake ni takriban 193 kabla ya kuongeza idadi ya Wakala wa Serikali. Kamati inaona tunarudi kule tulikotoka licha ya mageuzi tuliyofanyia kazi ya kupunguza Mashirika ya Umma ili Serikali ibakie na kazi yake ya Utawala wa Sheria (*The Rule of Law*). Kamati inaamini kuwa, fedha za Mashirika ya Umma, Mawakala na Mamlaka kama zingekuwa zinaingia Serikalini, Bajeti ya Serikali isingekuwa trillion.11.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kufikiria (*to rethink*), juu ya utaratibu wa kurekebisha kasoro hii ya kutokupata mapato kutoka kwa baadhi ya Mashirika ya Umma, Mawakala (*Executive Agencies*), Hifadhi za Pensheni za Taifa (*Pension Fund Houses*) na hata baadhi ya Mamlaka. Uanzishwaji wa Wakala wa Serikali, Mamlaka na Mashirika ya Umma, umesababisha Serikali kupoteza vyanzo muhimu vyta mapato ambayo yaningeingia Serikalini kama masurufu.

Fedha hizo zinazobaki kwenye taasisi hizo siyo tu hazina udhibiti wa fedha, bali vile vile yanaondoa uhalali (*legitimacy*) wake kwa kuwajibika katika kuwaendeleza wananchi. Taasisi hizi nyingi zina fedha za kutosha, wakati huo huo zinatoza kodi kwa wananchi kulipia miradi yake, uendeshaji wake na gharama za matumizi yao. Kuna wakala nyingine zimeingia hata kwenye shughuli za uwekezaji, kwa mfano wa majengo

na hivyo kuacha kufanya kazi za msingi (*Core Business*) kama sheria zinavyowaelekeza na hatimaye kuingiliana na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipoangalia mfumo wa Bajeti kwa mwaka 2010/11, ilitaka kujua mikopo ya biashara inayofikia shilingi. 0.9 trilioni itapatikana kutoka wapi, kwani kama Serikali itakopa kwa kiasi hicho, upo uwezekano wa kuiengua Sekta Binafsi (*crowd out*) katika kupata huduma hiyo na hivyo kupunguza viwango vya uwekezaji. Vile vile Kamati ilipenda kujua kama mikopo hiyo itatolewa kama zoezi la Benki Kuu kuondoa ukwasi wa ziada katika uchumi (*mop out excess liquidity*) au ni utaratibu wa kutumia *Government Bonds au Treasury Bills*.

Kwenye eneo la mikopo ya kawaida, kama asilimia ya Pato la Taifa, inaashiria kuwa Benki Kuu inaweza kugharimia Bajeti ya Serikali kwa kuchapisha fedha, athari yake fedha hii inaweza kuongeza mfumko wa bei (*fiat money*). Kamati imetoa angalizo katika maeneo haya ili Serikali isije ikaingia kwenye madeni makubwa ya ndani na kuongeza mfumko wa bei, pamoja na athari za gharama kubwa za riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna udhaifu katika udhibiti na uwajibikaji katika eneo zima la manunuvi. Karibu asilimia 70 ya Bajeti ya Maendeleo (shilingi. 7.7 trilioni) ya kipindi kijacho itatumika kwa manunuvi wakati asilimia 90 ya Bajeti yote ya Serikali itatumika kwa manunuvi. Fedha nyingi za Serikali zinapotea katika manunuvi. Hatua ya Serikali kuifanya marekebisho Sheria ya Manunuvi inapongezwa. Eneo hili lisipodhibitiwa, litaendelea kuingizia Serikali hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna gharama kubwa za ufanyaji wa biashara na uwekezaji hapa nchini. Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia ya Mwaka 2009 inaonesha nafasi ya Tanzania katika vigezo vya urahisi wa kufanya biashara imeshuka kutoka nafasi ya 126 kati ya nchi 183 mwaka 2008 na kuwa ya 131 mwaka 2009. Wakati huo huo thamani ya mitaji ya kigeni (*FDI*) ilikuwa US\$ 744 millioni mwaka 2008 (upungufu wa asilimia 14.5). Katika eneo hili, Tanzania tunashika nafasi ya tatu katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa, pamoja na kuwa na kigezo kikubwa nchini petu cha amani na utulivu, maeneo yafuatayo yarekebishwe haraka ili kuijengea Sekta Binafsi mazingira bora ya uwekezaji:-

- (a) Kupunguza urasimu kwa kiwango kikubwa;
- (b) Kuharakisha mchakato wa utoaji wa maamuzi ya kiutendaji hata ya kimahakama (*Decision Making Process*);
- (c) Utaratibu wa utoaji wa leseni uboreshwe (*Licensing Procedures*);
- (d) Mfumo wetu wa kodi uvutie wawekezaji na wafanyabiashara walipe kodi badala ya kuziepuka na kuzikwepa. Kodi zikiwa nyingi ukusanyaji wake hauwezi kuwa tija;

(e) Hifadhi za *Pension* ni nyingi, karibu tano; Kenya ni moja tu. Mkakati wa Serikali wa kuziweka hifadhi zote chini ya mwamvuli mmoja liharakishwe;

(f) Mamlaka za udhibiti ni nyingi mno pamoja na *road blocks* ambazo zinaondoa tija hasa katika biashara ya usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya yarekebishwe ili tuweze kuvuta zaidi wawekezaji wa ndani na wale wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la upatikanaji wa umeme nchini limekuwa tatizo kubwa kwa uwekezaji wa viwanda na biashara. Kwa kuwa katika kipindi hiki cha bajeti, Serikali imetenga kiasi cha shilingi 270.9 bilioni kwa ajili ya shughuli za umeme, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inasimamia kikamilifu matumizi ya fedha hizo na yalingane na huduma ya umeme itakayotolewa (*value for money*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Tanzania kufanyiwa tathmini ya uwezo wake Kukopa na Kulipa Madeni kwa kutumia Dhamana ya Kimataifa (*Sovereign Credit Rating and Bond Issurance*) ili fedha hizo zisimamie katika kundeleza miundombinu haraka hasa ya reli, bandari, usafiri wa anga na barabara. Aidha, Serikali itimize ahadi yake iliyojiwekea kama shabaha na msingi wa bajeti yake kwa mwaka 2010/2011 ya kuboresha, kupanua na kukarabati miundombinu ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na miradi ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, utegemezi wa misaada unaunganishwa pia na utegemezi mwingine unaonyemelea Taifa letu kwa kasi. Kamati imeona sasa tunaingia katika utegemezi wa kidemografia. Watu wengi ni tegemezi kutokana na idadi ya watoto na vijana kuwa wengi zaidi kwa asilimia 70 ya idadi ya Watanzania wote. Ukosefu wa ajira kwa vijana ni eneo la kulipa msukumo maalumu, ipo haja ya kutumia zaidi ubunifu na nguvu za vijana katika kuchangia kujenga uchumi kwa kupewa fursa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la MKUKUTA lilikuwa ni kupunguza idadi ya wasiokuwa na kazi toka asilimia 13 mwaka 2002/2001 hadi asilimia 6.9 mwaka 2010, hali hii bado haijafikiwa katika awamu hii ya kwanza ya MKUKUTA, hivi sasa tumefikia asilimia 11. Katika Awamu ya Pili ya MKUKUTA, tathmini ya kina ifanywe kwa kipindi chote ili tujue wapi tulipokuwa, tupo wapi na tunaelekea wapi. Hii itasaidia katika kuijiandaa na utekelezaji wa awamu nyingine.

Kimsingi, changamoto zilizojitokeza katika MKUKUTA - I; zikatumike kurekebisha utekelezaji wa MKUKUTA - II. Hali hii itasaidia kuandaa ajira za vijana, akina mama na kutoa elimu ya ujasiriamali, mikopo ya bei nafuu, pamoja na kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na sensa ya idadi ya watu na makazi nchini (2002), nchi yetu inakadirisha kuwa na watu milioni 34.5 na kasi ya ongezeko la idadi ya watu ni asilimia 2.9, hivyo kwa mwaka huu 2010 idadi ya watu inakadirisha kuwa milioni

40.7. Idadi ya watu nchini inakua kwa haraka mno kuliko uwezo wa kiuchumi unaohitajika ili kuwapatia maendeleo endelevu, ikiwa ni pamoja na huduma muhimu za jamii kama vile elimu na afya. Fedha zinazotengwa kwenye miradi ya maendeleo ni tegemezi na haziwiani na ongezeko la watu; hali hii inatishia uwezekano wa kupunguza umaskini, uwezekano wa kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (*MDGs*). Hali kadhalika, rasilimali hii ya watu haitumiki ipasavyo katika kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa utaratibu wake wa kutoa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG Report*), ambayo inaelekeza maeneo ya kuyafanya katika kuzingatia matumizi bora ya rasilimali chache za Taifa. Kamati inashauri maeneo yote yenyе upungufu yafanyiwe kazi, hasa yale yanayohusisha upotevu wa fedha na rasilimali. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuona jinsi itakavyoziimarisha Halmashauri za Wilaya katika kuongeza mapato kupitia vyanzo vya kodi. Ipo haja kuanzisha vyanzo vipya vya mapato vyenye tija na kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati imebaini kuwa, eneo moja muhimu linalohitaji kuendeleza nchi yetu ni lile la uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Pamoja na jitihada zinazoendelea hivi sasa, Serikali ichukue jukumu la kuwawezesha wananchi moja kwa moja au kwa utaratibu maalum kufuatilia ngazi tatu zifuatazo: Wananchi wa kipato cha chini; wale wenye kipato cha kati; na wale wenye kipato cha juu, hasa tukizingatia kuwa tunaingia kibiashara na kiuchumi katika Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ijiingize katika maeneo ya uwezeshaji yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara ili kupunguza gharama za kufanya biashara na uwekezaji katika nchi yetu. Serikali irekebishe maeneo ya Sheria za Ardhi, upatikanaji wa leseni na kadhalika. Aidha, ipo haja ya kupunguza kero za uendeshaji wa Serikali kwa kupunguza urasimu, kutoa maamuzi kwa wakati na kufanya kazi kwa tija.

(b) Serikali iweke umuhimu mkubwa katika kuendeleza siyo tu elimu ya sayansi na teknolojia, bali vile vile elimu ya biashara na wajasiriamali.

(c) Kuwawezesha wananchi kupata mitaji. Ziwapo jitihada za makusudi za kuvifanya vyombo na taasisi zilizopo zinazokopesh, kuwafikia na kuwahudumia wale wenye vipato vya chini. Serikali ibuni mikakati na taratibu za kuwasaidia kubuni miradi yenye hadhi ya kupata mikopo kutoka Benki (*Bank-able Projects*), iwe bure au kwa malipo kidogo.

(d) Kuwatafutia wajasiriamali maeneo ya kufanya kazi zao (*premises*) na kuwawekea vivutio vya makusudi ili kuwawezesha. Nchi nyingi duniani zimetenga maeneo mahususi kwa ajili ya wajasiriamali wadogo katika miji yao.

(e) Iendelezwe teknolojia hasa ya kutumia nguvu kazi (*labour based technology*), pamoja na uendelezaji wa ufanisi na tija; na

(f) Eneo lingine ni lile la kuboresha masoko ya bidhaa za wajasiriamali hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa uwezeshaji ni lazima ujumuise vikundi vitakavyotegemea teknolojia ya nguvu kazi. Maendeleo ya TEKNOHAMA katika nchi yetu kutokana na kuboreshwa kwa mitandao kadhaa ya simu za mikononi na huduma zinazoambatana nazo; pamoja na vituo vya simu (*tele - centres*), vitumike kuendeleza biashara, pamoja na kuzingatia maeneo ya kijiografia nchini (*geographical location*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko makubwa ya uchumi hivi sasa duniani yanalazimisha kufuata mkondo unaotawaliwa na nguvu za soko. Nguvu za soko ni lazima ziwajumuise wananchi wenye vipato vya chini vijijini. Serikali haina budi kukuza masoko kulingana na bidhaa za wazalishaji wadogo. Mfano mzuri ni ule wa mifumo ya uwekezaji wa pamoja ambao utaruhusu ushiriki katika masoko ya mitaji na hisa (*Collective investments to participate in the capital markets*) na eneo lingine ni lile la kuendeleza *SACCOS*. Pia, Serikali haina budi kulenga asasi za kijamii (*Community Based Organizations*) kwa kuwa na mkakati au mwongozo wa jinsi ya kujipanga na kuimarisha organization za ngazi za chini. Kwa maana nyingine, uwezeshaji wa wananchi wadogo kiuchumi uwe ni sehemu ya sera moja kwa moja. Aidha, ipo haja ya kutengeneza utaratibu huu uwe wa kitaasisi (*Institutional Arrangement*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ipo haja ya kuwaunganisha wawekezaji wakubwa na wadogo katika kuendeleza shughuli za kiuchumi nchini. Kwa mfano, makampuni makubwa ya madini yafanye biashara moja kwa moja na wadogo hasa katika upatikanaji wa bidhaa muhimu kama vile mboga mboga, nyama na kadhalika. Hali hii itaunganisha (*linkages*), masoko baina ya makundi haya na itasaidia sana kupunguza umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, picha inayojitokeza, Kamati imebaini kuwa ipo haja ya kujifunza tufanye nini katika kipindi kijacho na vinavyokuja ili kuibua rasilimali zetu na kukuza uchumi wetu na hatimaye kuongeza mapato ya nchi. Tunachojifunza ni kwamba:-

(i) Serikali haina budi kuchukua hatua zaidi katika eneo la kuongeza mapato katika uchumi; ni dhahiri kuwa jitihada za kukusanya mapato zinahitaji ziimarishwe.

(ii) Utetemezi wa misaada na mikopo kutoka nje siyo mkakati endelevu wa kukuza uchumi na kuleta maendeleo. Kwa mfano, katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, katika Bajeti ya 2020/11 inaonesha kuwa kati ya jumla ya shilingi 3,236,041 milioni; shilingi 1,280,272 milioni zitakuwa fedha za ndani au asilimia 39.6 na shilingi 1,955,769 milioni au asilimia 60.4 zinategemewa kutoka nje. Hali hii ni changamoto kubwa si kwa Serikali, bali kwa Uchumi wetu. Upo umuhimu mkubwa wa kuongeza uzalishaji.

(iii) Kutoptaka na kutoptaka viwango vya malengo vinavyowekwa katika mipango na Makadirio ya Bajeti, wataalamu watafifi, kama lipo tatizo la kupanga malengo makubwa ya mipango na makadirio ya mapato yasiyotekelozeka (*overly optimistic revenue projections*), tatizo hili linaweza kuwa ndiyo sababu ya upungufu unaojitokeza katika utekelezaji na hatimaye serikali kulazimika kufanya makato na kupunguza makadirio ya fedha za matumizi yanayoidhinishwa (*In year cuts of approved expenditures*). Hali hii inaleta utekelezaji dhaifu wa Bajeti (*poor budget execution*).

(iv) Malengo na mikakati yote ya mipango na kibajeti tuliyojiwekea vizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano wao walionipa katika kujadili na kupitia Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011. Naomba nitumie fursa hii, kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dokta Abdallah O. Kigoda, Mbunge – Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mbunge – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mbunge, Mheshimiwa Dokta Anthony M. Diallo, Mbunge, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mbunge, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mbunge, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mbunge, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mbunge, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mbunge, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge, Mheshimiwa Dokta Binilith S. Mahenge, Mbunge, Mheshimiwa Monica Ngenzi Mbega, Mbunge, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mbunge, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mbunge, Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge, Mheshimiwa Dokta Omar Mzeru Nibuka, Mbunge, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mbunge, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mbunge, Mheshimiwa Martha Jacchi Umbulla, Mbunge na Mheshimiwa Charles Kajege, Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Hamza Mwenegoha – Makamu Mwenyekiti, kwa kunisaidia kuiongoza Kamati. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Mawaziri wa Wizara ya Fedha na Uchumi, pamoja na Watendaji wao wote na Taasisi mbalimbali, kwa kuandaa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu, ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge, Dokta Thomas D. Kashililah, Makatibu wa Kamati; Ndugu Michael Kadebe na Ndugu Lawrence Makigi, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa Hotuba yako. Sasa nitamwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, yeye ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii, ingawa leo afya yake siyo nzuri sana, tutaangalia pale atakaposhindwa atasaidiwa; karibu.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivytangulia kusema kwamba, kifua changu siyo kizuri, *inshallah* Mwenyezi Mungu, anisaidie. Baada ya kumshukuru Mola Mtukufu, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mipango 2010/2013 na Hotuba ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2010/2011, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 96(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia kuufikia wakati wa bajeti hii tukiwa katika hali ya amani na utulivu nchini kwetu. Mola azidi kutupa amani, umoja na kuvumiliana hasa katika kipindi hiki cha kutafuta wagombea kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu, tunapoelekea kwenye uchaguzi na wakati wa uchaguzi wenyewe.

Aidha, nawaomba Watanzania wenzangu, waitumie fursa hii kwa kuchagua viongozi watakaoliongoza Taifa letu kwa uangalifu mkubwa sana ili tupate viongozi waadilifu, wabunifu na wenye moyo wa kuwatumikia watu na siyo nafsi zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi za dhati na kuwashukuru Wabunge wa Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano wao walionipa wakati wote wa kipindi changu cha uongozi wakiongozwa na Dr. Willibrod Slaa, Mbunge wa Karatu na Naibu Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Naomba niwashukuru Mawaziri Vivuli na wasaidizi wao kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kutoa maoni mbadala katika sekta zao. Naamini kutokana na kazi nzuri tulioifanya, Watanzania watatuzawadia kwa kuongeza idadi ya wabunge wa Upinzani katika Bunge lijalo na hata kutupa nafasi ya kuliongoza Taifa ili yale tuliyokuwa tukiyasema tupate fursa ya kuyatekeleza kwa vitendo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukurani na pongezi za dhati kwa Chama changu cha *The Civic United Front (CUF)*, Chama cha Wananchi, kwa kuanzisha utaratibu wa kupanua demokrasia zaidi ndani ya chama, unaowapa fursa wanachama kutoa maoni yao juu ya viongozi ambao wanaamini kuwa watawawakilisha katika nafasi za uongozi wa Taifa letu. Katika mchakato huu, wapo waliopita vizuri na wapo waliopata mikwaruzo; wote nawapongeza kwani mamlaka ya uongozi yanatoka kwa wanachama na hatimaye kwa Watanzania wote, hakuna mwenye hati miliki kwa nafasi aliyonayo.

Suala la msingi ni kujenga mshikamano zaidi ili chama chetu kijipatie ushindi mkubwa katika uchaguzi ujao. Naomba niitumie fursa hii, kuwashukuru sana Wanachama wa Chama changu wa Jimbo la Wawi, kwa kunipa heshima ya kupata kura

za kishindo katika hatua hii ya kura za maoni. Nawaahidi kuongeza bidii ya kuwatumikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi, kwa kuliongoza Bunge letu katika kipindi hiki kwa viwango vinavyotakiwa kimataifa na kulijengea Bunge letu heshima katika Mabunge ya Dunia na hasa yale ya Jumuiya ya Madola. Aidha, naomba niwapongeze wasaidizi wako, Ofisi ya Katibu wa Bunge, kwa kujitahidi kutoa utumishi ulio bora kwa wafanyakazi na wabunge, huku tukielewa kuwa siyo rahisi kumridhisha kila mtu, lakini Kambi ya Upinzani inashukuru huku ikiamini kuwa, maboresho yatafanywa ili kujenga Kambi ya Upinzani iliyo imara zaidi, ambayo naamini katika Bunge lijalo itaundwa na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mbunge wa Kilosa na wasaidizi wake, kwa ushirikiano wao walionipa kama Waziri Kivuli wa Fedha na Uchumi. Ahsanteni sana. Ni imani yetu kuwa, Watanzania watatupa fursa ya kuongoza nchi ili na wenzetu wapate fursa ya kuwa Mawaziri Vivuli na kuendeleza pale tulipoachia.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za pekee nawapa Bw. Oliver Mwikila, Bw. Frank Mbumi, Mama Salvina Mahundu na Bi. Grace Samwel, kwa msaada mkubwa walionipa katika kufanikisha majukumu yangu kama Kiongozi wa Upinzani Bungeni na pia kufanikisha maandalizi ya Hotuba hii. Nawashukuru sana kwa moyo wao wa kujituma, wakielewa uchache wetu na wingi wa majukumu tuliyonayo ya kuwatumikia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitangulie kwa kuwakumbusha Watanzania wenzangu kuwa, nchi yetu toka tupate Uhuru imeongozwa na CCM na vyama vilivyoitangulia. Hivyo ni dhahiri kuwa, mafanikio na upungufu wote wa maendeleo ya nchi yetu, umetokana na Uongozi na Sera za CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu sote kujiuliza; katika kipindi chote cha uongozi wa chama kimoja; je, kwa sera zilizokuwepo na zilizopo Mtanzania wa kawaida maisha yake yameboreka kwamba sasa anaweza akapata angalau milo miwili bila wasiwasi na anaweza akasomesha watoto wake na watoto hao wakasoma vizuri na hatimaye wakapata ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mtanzania wa kawaida anaweza kujiajiri kwa kupata mikopo kwa urahisi yenye riba nafuu? Kwamba, anaweza kupata huduma ya kijamii iliyotukuka bila ya kulipia kwa gharama kubwa? Kwamba anaweza kupata bei muafaka ya mazao yake kwa kuuza anakotaka kama ilivyokuwa kabla ya Uhuru na Mapinduzi? Je, hata anayefanya kazi amepata mshahara unaokidhi muda wake wa kazi na mahitaji yake? Kwamba ukipenda kufanya biashara, unaweza ukasajiliwa na kupata mtaji wa kuanzishia bishara zako bila ya kuchelewa au usumbufu au kwa ufupi kwamba anayo matumaini ya kufikia Maisha Bora kwa Kila Mtanzania ikiwa kilo moja ya sukari ni shilingi 2000 wakati pato lake kwa siku ni chini ya dola moja ya kimarekani (shilingi 1,400)?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelazimika kuuliza maswali haya ili tupate fursa ya kupima mafanikio na upungufu uliojitekeza katika kipindi hiki cha Uongozi wa chama kimoja ili Watanzania wapate fursa ya kufanya maamuzi yanayotokana na uthibitisho badala ya hisia au ushabiki.

Tathmini sahihi tunaipata katika utekelezaji wa Ilani ya CCM, ambayo ilii taka Wizara ya Fedha na Uchumi, ijikite katika maeneo na Programu mbalimbali za Serikali zinatokana na Mpango wa Taifa wa *Vision 2025*, MKUKUTA, MKURABITA, MDGS na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya CCM inalenga kukuza uchumi kwa kiwango cha 10% ifikapo mwaka 2010 kutoka 6.7% mwaka 2005 na kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. Ukweli ni kuwa, lengo hili limeshindwa kufikiwa na tumekuwa Taifa la kupokea misaada na kukopa kopa kila pahali. Aidha, Ilani ya CCM pia ilijigamba kuimarisha au kubinafsisha Mashirika ya Umma, lakini ukweli leo Serikali ya CCM ya Awamu ya Nne, inamaliza miaka yake mitano ikishindwa kutekeleza lolote katika hayo. Hili linathibitishwa na Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, inayoonesha kuwa ni 44% tu ya mashirika hayo ndiyo yanayofanya biashara na 37% yamefungwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wetu wa Maendeleo ultokana na mpango wa muda mrefu (*Vision 2025*) au Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, ambao ulilenga kuhakikisha kuwa, ifikapo 2025, Watanzania watakuwa na maisha bora na mazuri, kuwa na uongozi bora na utawala wa kisheria na kujenga uchumi imara wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani. Tuliambiwa Tanzania itakuwa na uchumi unaotegemea sekta nyingi na ulioendelea kwa kuwa na wastani wa viwanda vingi, uchumi mpana ulio tulivu (*macroeconomic stability*), miundombinu imara na Pato la Taifa litakua kwa asilimia 8 au zaidi.

Tuliambiwa Tanzania ya 2025 itakuwa inamudu ushindani wa kikanda na kimataifa kwa kuwa na nguvu kazi yenye elimu na ujuzi. Hata hivyo, dira hii hajatafsiriwa na kuwekwa katika mpango mkakati wa utekelezaji. Wananchi wengi hawajui malengo ya dira ya maendeleo. Viongozi wa juu wa nchi hawaielezi na kuifafanua dira hii, huu ni upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya, tena kwa Watanzania walioiamini CCM ambayo imeendelea kuwaangusha kila mwaka, hakuna dalili zozote za kufikiwa malengo hayo. Kibaya zaidi ni kwamba, Mpango huu haueleweki kwa umma kama vile lilivyoweza kueleweka Azimio la Arusha. Hii ni kasoro ya kwanza kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utamaduni uliokuwepo wakati wa Mwalimu wa kuwaeleza na kuwahamasisha wananchi waelewe dira na mipango ya nchi; kwa mfano, mpango wa kwanza wa maendeleo ya miaka mitano, mwaka 1994/1999, ulikuwa na kibawagizo, “*It can be done, play your part,*” ulipigiwa debe na wananchi wakaelewa madhumuni yake. Azimio la Arusha la Ujamaa, lilielezwa na kusambazwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Mkapa aliandika dibaji nzuri ya dira, lakini hakuisimamia kuifafanua kwa wananchi. Serikali ya Awamu ya Nne haina habari kabisa na suala la Dira ya Maendeleo; hii ni kasoro kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, MKUKUTA ambao ni sehemu ya Dira ya Taifa lengo lake kuu ni katika makundi matatu; kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; kuimarisha ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukadiriaji wa gharama za MKUKUTA katika baadhi ya sekta muhimu ulikamilika mwisho wa 2006 na gharama zake zikabainika kuwa ni kubwa mno kuliko uwezo wa Serikali; kwa hiyo, MKUKUTA umeshindwa kutekelezeka. Kwa mfano, gharama za kutekeleza MKUKUTA katika Sekta ya Nishati ilikadiriwa wastani wa Dola za Kimarekani 911 kwa mwaka. Sekta ya Kilimo inahitaji wastani wa Dola za Kimarekani milioni 300 kwa mwaka, Sekta ya Afya dola milioni 476 na barabara wastani wa dola 922.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya sekta nne tu ni zaidi ya asilimia 70 ya matumizi yote ya Serikali ya 2006/2007. MKUKUTA haukutelezwa ipasavyo kwani gharama zake hazikukadiriwa mapema na ukadiriaji ulipokamilika, gharama zilikuwa kubwa mno hata lengo la kupunguza umaskini kwa asilimia 50 ifikapo 2010 halikufikiwa. Tathmini ya bajeti ya kaya ya kupunguza umaskini inaonesha umaskini umepungua toka asilimia 34.5 mwaka 1990 kufikia asilimia 35 mwaka 2000 na asilimia 33.6 mwaka 2007. Pamoja na kutokufikia lengo hili, MKUKUTA II umeweka lengo la kupunguza umaskini kutoka asilimia 33.6 ya mwaka 2007 na kufikia asilimia 19.3 ya mwaka 2015.

MKUKUTA II hauelezi mkakati gani ambao haukutekelezwa miaka 20 iliyopita na sasa itaweza kufanikisha kupunguza umaskini kwa kiwango cha asilimia 19.3; hii nayo ni kasoro nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasoro ya tatu kubwa ni kuwa bajeti ya 2009/2010, ilikuwa ni ya mwisho ya utekelezaji wa MKUKUTA I. Vilevile ya 2010 ni ya kwanza kwa utekelezaji wa MKUKUTA II. Hadi leo hakuna tathmini rasmi ya MKUKUTA I; hivyo tunaingia katika MKUKUTA wa II na kasoro zilezile za MKUKUTA I; hii nayo ni kasoro nyingine kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika MKUKUTA I, ukuaji wa Sekta ya Kilimo ulikadiriwa kutoa asilimia 5 hadi asilimia 10 mwaka 2009/2010, katika Ilani ya CCM ilikuwa ni asilimia 20. Mwaka 2009/2010, mifugo ilitegemewa kutoka asilimia 2.7, uzalishaji wa chakula uwe kutoka tani milioni 9 hadi tani milioni 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha leo hata chakula cha akiba nacho kina tatizo, bajeti ya kilimo ilitakiwa iwe na ongezeko la asilimia 23.1 kutoka Dola za Kimarekani 269.3 milioni mwaka 2005/2006 ifikie dola milioni 331.4 mwaka 2010.

Kwa kifupi, ili MKUKUTA huu wa kwanza ufanikiwe katika Sekta ya Kilimo ultakiwa uwe na wastani wa bajeti ya Dola za Kimarekani 275 kila mwaka, lakini kwa miaka mitano kuna pengo la wastani wa dola wa asilimia 42.2; hii nayo ni kasoro nyingine ya kutekeleza MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu ambao ni mwaka wa kwanza wa kutekeleza MKUKUTA II, kilimo pamoja na sera mpya ya Kilimo Kwanza kimetengewa shilingi milioni 903 bilioni, ambazo ni asilimia 7.8 tu ya bajeti nzima, wakati kwa mujibu wa makubalino ya Nchi za SADC ilitakiwa isipungue asilimia 10. Je, maisha bora kwa kila Mtanzania yatafikiwa?

Tatizo moja kubwa la mfumko wa bei ni uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula? Tumeshindwa hata kutumia soko la mchele la Kenya, ambalo huagizo mchele wastani 170,000 kutoka Pakistan, sisi tumeshindwa kuwauzia; je, tutalitumia Soko la Afrika Mashariki au sisi ndiyo tutakuwa wanunuaji tu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya tani moja ya mchele kwa mujibu wa *Regional Agriculture Trade Intelligence Network (RATIN)*, Mjini Kigali ni wastani wa USD 952, sawa na Tshs. 1,400,000 na kwa mahindi ni USD 223 sawa na Tshs. 349,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kungekuwa na umakini wa utekelezaji wa MKUKUTA wa kwanza kwa sekta ya uzalishaji wa mpunga na mahindi tu na kwa kutumia vizuri Soko la Afrika Mashariki, leo tusingezungumzia nakisi katika bajeti zetu na hivyo uhaba wa chakula na mfumko wa bei ingelikuwa ni hadithi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo (pamoja na mifugo na uvuvi na kadhalika), ndiyo sekta iliyotegemewa sana kuongeza uzalishaji wa bidhaa, kupunguza mfumko wa bei na kuongeza kipato cha watu wetu, kwani ndiyo sekta pekee inayoajiri asilimia isiyopungua 65 ya Watanzania wote. Tumeshindwa kufikia malengo ya uzalishaji wa tani 12 milioni. Hii ni kasoro ya tano kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Uganda, uzalishaji wa mpunga katika *upland rice* bila kutumia mbolea wala umwagiliaji lakini kwa kutumia mbegu bora, wanazalisha wastani wa tani 2 - 3 kwa hekta, wakati sisi katika skimu 16 za umwagiliaji maji tunazalisha wastani wa tani 1 - 2 kwa hekta. Je, katika hali hii upo ufanisi wa utekelezaji wa MKUKUTA na kwamba lengo la kupunguza umaskini wa kipato litafikiwa? Hii nayo ni kasoro nyingine ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili ni kwa Serikali kuiwezesha jamii kuwa na uwezo wa kufanya manunuzi (*improve people's purchasing power*). Uwezo wa jamii kufanya manunuzi ndiyo njia pekee itakayoongeza ukubwa wa uchumi wetu katika ngazi zote za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Watu iliyotolewa mwaka huu inaonesha kuwa, kwa mwaka 2007 idadi ya Watanzania

waliokuwa wanakadiriwa kuwa ni maskini ni milioni 12.9 kati ya Watanzania milioni 38.3. Kati ya Watanzania hao milioni 12.9; watu milioni 10.7 sawa na asilimia 83% wanaishi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo kilichokubaliwa kimataifa kuwa matumizi ya chini kabisa kwa mtu mzima ahesabiwe kuwa ni maskini wa kutupwa ni dola moja kwa siku. Benki ya Dunia inakadiria kwa kutumia kipimo hiki, umaskini Tanzania umeongezeka toka asilimia 73 ya Watanzania wote mwaka 1990 mpaka kufikia asilimia 89 mwaka 2000. Kwa kutumia kigezo hiki cha kimataifa na takwimu za uchunguzi wa bajeti ya kaya wa 2007, zaidi ya asilimia 90 ya kila Watanzania 100 ni maskini wa kutupwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tafiti hizi zinapelekea kutolewa kwa taarifa hii zilifanywa mwaka 2007, hivyo ni ukweli ulio wazi kuwa, kuna uwezekano mkubwa kuwa idadi ya Watanzania maskini wanaoishi mijini na vijijini imeongezeka maradufu kutohana na hali halisi ilivyo kwa sasa. Hatuwezi kuwa na mshikamano wa kweli wa kitaifa ikiwa ukuaji wa uchumi unaowanufaisha watu wachache na kuacha zaidi ya Watanzania milioni 36 wakiwa maskini wa kutupwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Serikali ya CCM imeshindwa vibaya kulitekeleza katika miaka hii mitano ya Awamu ya Nne ni uendelezaji wa sekta isiyo rasmi, kwa kuijengea uwezo wa kupata mikopo nafuu na hivyo kuwasaidia Watanzania maskini kujikwamua katika laana hiyo ambayo haikuletwa na Mungu, bali imetokana na sera mbovu na usimamizi mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukubwa wa Sekta ya Uchumi isiyokuwa rasmi ni karibu mara kumi ya sekta iliyo rasmi ya uchumi. Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ya Mwaka 2009, inaonesha kila mwaka ajira katika sekta isiyo rasmi ya uchumi imekua kwa wastani wa watu 630,000 kwa mwaka wakati tafiti zilizofanywa na taasisi ya *Finscope* na kugharimiwa na *Financial Sector Deepening Trust Fund (FSDT)*, inaonesha kuwa ni 9% ya wananchi ambao wanatumia huduma rasmi za kibenki, 2% ya wananchi ndiyo wanaopata huduma nyingine za asasi ndogo za kifedha, 35% wanatumia huduma ambazo siyo rasmi, kwa maana kwamba wanaendesha biashara yao kiujanja ujanja tu. Aidha, 34% ya wananchi hawapati kabisa huduma za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizi zinatuonesha kuwa, hata kama Serikali itajitahidi vipi kuongeza vyanzo vya kifedha na kutengeneza mazingira mazuri kwa wawekezaji, lakini tusipofanya maboresho na kuimarisha asasi/taasisi zinazotoa huduma za kifedha kwa wananchi wa mijini na vijijini, kuondoa umaskini wa kipato litakuwa ni jambo lisilowezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Mkakati wa Kuendeleza Kilimo, programu zinazotakiwa kutekelezwa katika ngazi ya wilaya, mojawapo ni kwa Halmashauri kutunga sheria ndogo ndogo na kanuni zitakazoruhusu utendaji mzuri kwa asasi ndogo za fedha (*rural finances*), kusaidia katika kuinua kilimo na shughuli nyingine zisizo za

kilimo (*off farm activities*). Inasikitisha kwamba, Serikali ya CCM haikuona umuhimu wa kuutekeleza mkakati huu ipasavyo ili kuboresha hali za watu wetu maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Asasi za Fedha na Umaskini wa Kipato; Sheria ya Mabenki na Asasi za Fedha ya Mwaka 2006 ilipitishwa na Bunge lako hili kwa lengo la kuipa Benki Kuu uwezo na uhuru zaidi wa kusimamia kikamilifu benki na asasi za fedha nchini ili kupanua huduma za sekta hii na hasa kuwawezesha wananchi kupata mikopo ya masharti nafuu ili washiriki kikamilifu kujiondolea umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inarudia tena kwa kuitaka Serikali kuziwezesha asasi ndogo za fedha kupata mikopo nafuu au kuingia nayo ubia ili kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo kwa riba nafuu inayolipika. Kinyume na hapo, bado uchumi wetu utaendelea kushikiliwa na kundi la watu wachache na kuwaacha Watanzania walio wengi wakiwa omboomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ameitaja Mifuko mingi ya mikopo ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Uwezesaji Kiuchumi. Tanapendekeza pafanyike tathmini huru, yaani *independent evaluation* ya Mifuko hii kama inakidhi malengo yake na kwa kiasi gani ni endelevu, kwani bado hatujaona mafanikio yake kiasi cha kuweza kujenga kada mpya ya wafanyabiashara na wawekezaji wa kat.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya malengo ya MKUKUTA wa Kwanza ilikuwa ni kupunguza umaskini wa kipato kwa Watanzania wanaoishi mijini hadi kufikia 12.9% na kwa wale wanaoishi vijiji hadi 24% ifikapo mwaka 2010. Malengo haya yaliwekwa kutokana na ukweli kwamba, 34% ya kaya zilikuwa zinaishi chini ya mahitaji ya msingi kwa vigezo vya umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa, ukuaji wa uchumi umeshindwa kwenda sambamba na ukuaji au uondoaji wa umaskini wa kipato. Hili limechangiwa na sababu nyingi, lakini Kambi ya Upinzani inaona kwamba mbali ya kutokuwa makini katika kuoanishwa kwa mkakati wa kupambana na umaskini, pamoja na sera zetu za kukuza uchumi pia imechangiwa kwa kiasi kikubwa kwa Serikali kutokuwa na mkakati muhimu na unaoeleweka wa kushiriki na kuiwezesha tasnia ndogo ya fedha ya Microfinance.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasema hivyo kutokana na takwimu zilizotolewa na Serikali katika Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ya Mwaka 2009, inayoonesha kuwa uwezo wa matumizi kwa kaya katika mchango wa Pato la Taifa umeshuka kutoka 77% mwaka 2000 hadi 73% mwaka 2007. Wakati kwa upande wa matumizi ya Serikali, kwa kipindi hicho umepanda kutoka 12% hadi 18%.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake ni kwamba, umaskini wa kipato kwa kaya umeongezeka, kwani uwezo wa kaya kufanya manunuzi kwa mahitaji ya lazima umepungua wakati Serikali imeongeza uwezo wake wa kufanya manunuzi. Manunuzi mengi ambayo yanafanywa na Serikali ni yale ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja na maisha ya kawaida ya mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema hapo juu kuwa, tasnia ndogo ya fedha ya Microfinance ndiyo ingekuwa injini ya kuongeza kasi na uwezo wa kaya katika kufanya manunuzi, lakini kwa makusudi mazima Serikali ya CCM inashindwa au inakataa kuiwezesha ili iweze kuwafikia Watanzania ambao wanahitaji huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa, dunia nzima hasa mataifa ambayo kila siku Serikali inayatolea mifano hapa Bungeni kuwa wameweza kupambana na umaskini wa kipato kama vile India, Malaysia, Peru na kadhalika, wana mkakati maalum wa kuingia ubia na asasi au taasisi ndogo za fedha (Microfinance), kwa kuzipatia fedha ili zenyeze zifanye kazi ya kuwakopesha wananchi kwa riba ambayo itawawezesha wananchi kumudu na kuendelea na biashara zao wakati wakikidhi mahitaji yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa, zaidi ya 85% ya Watanzania wanaishi vijijini, lakini kutokana na tafiti zilizofanywa zinaonesha kuwa 56% ya Watanzania wanaishi vijijini wanaendesha maisha yao kwa shughuli ambazo si za kilimo (*non farm activities*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, shughuli hizo zinazoendeshwa na 56% ili kuleta tiya kwa wao na kwa Taifa kwa ujumla wake ni muhimu ushirikishwaji wa sekta ndogo ya fedha. Tunaposema sekta ndogo ya fedha (Microfinance), maana yake ni kwamba, asasi ambayo ina uwezo wa kutoa mikopo midogo midogo kulingana na mahitaji ya wakopaji, uwezo wa kutoa bima ya biashara kwa wakopaji, uwezo wa kutoa bima za afya kwa wakopaji na familia zao na pia uwezo wa kutunza akiba kwa wakopaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina uhakika kuwa, tasnia hii ndogo kama ikiwezesha viliyo na Serikali, umaskini wa kipato utapungua kwa kiwango kikubwa kama siyo kumalizika kabisa.

Mhesimiwa Spika, Sekta ya Fedha imekuwa ikibadilika sana hivi sasa. Zimeibuka huduma ambazo zinaweza kusaidia sana kuhakikisha kuwa Sekta ya Fedha inakua. Mfano mzuri ni huduma ya M-Pesa ambayo inasemekana kuwa takriban shilingi bilioni mbili kila siku zinatumwa kwa kutumia njia hii ya utumaji wa fedha.

Huduma hizi zinapaswa kupewa kipaumbele na Serikali ili kuweza kuhakikisha kuwa, fedha za wananchi zinatumwa katika njia salama na pia serikali kuona jinsi ya kukusanya mapato kutokana na faida zinazoletwa na huduma za namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Taasisi ya Serikali inayotoa mikopo kwa asasi/taasisi ndogo za fedha kwa riba ambayo ni kati ya 18% na 20% kwa mwaka. Je, kwa njia hii ni kweli asasi zinazokopa toka katika Taasisi ya Serikali kwa riba hiyo zitamkopesha mwananchi wa kawaida kwa riba kiasi gani ili nazo ziendelee kufanya biashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2009/2010, wakati Mheshimiwa Waziri akifanya marejeo ya uwezeshaji kiuchumi alisema kuwa; "Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi na Mradi wa Kuhudumia Biashara Ndogo Ndogo (SELF), kwa pamoja ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 68.58 kwa wajasiriamali 131,640 kupitia SACCOS 210 na Vikundi 86."

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa fedha hizo zilikopeshwa kwa riba kiasi gani kwani inaonesha kuwa, taasisi hii ya Serikali nayo inatoa mikopo kwa asasi ndogo ndogo kwa riba za kibiashara kama mabenki ya biashara. Hili ndiyo lengo la uanzishwaji wake? Kama ndiyo hivyo ni kwa nini ikae kwenye mwamvuli wa Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inazidi kushawishika kuwa Serikali ambayo inadai kuwa imepewa ridhaa na wananchi imeshindwa kwa makusudi kuwaondolea wananchi hao umaskini, kwa kushindwa kuzisimamia na kutoa maagizo kwa taasisi za fedha ili zikopeshe kwa riba nafuu asasi ndogo za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia BoT kuelekeza Taasisi za Fedha kuweka angalau asilimia 15 ya amana kwa kukopesha asasi ndogo za fedha na wakulima, wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuwa na maendeleo ya kiuchumi na kupunguza umaskini wa watu wetu bila ya kuwa na umeme wa uhakika. Malengo ambayo yaliwekwa na MKUKUTA ni kwamba, ifikapo mwaka 2010 idadi ya kaya/nyumba ambazo zitakuwa zimeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa iwe 20%. Wakati malengo hayo yakiwekwa mwaka 2001, idadi ya kaya ambazo zilikuwa zimeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa zilikuwa ni 10%

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu inaonesha kuwa, Dar es Salaam ambayo mwaka 2001 kaya zilizokuwa zimeunganishwa na Gridi ya Taifa zilikuwa 58.9% na kwa maeneo mengine ya mijini ilikuwa ni 29.7%; lakini mwaka 2007, Dar es Salaam ilishuka na kuwa 50.8% na maeneo mengine ikashuka kuwa 25.9%. Nusu ya nyumba za Jiji la Dar es Salaam hazina umeme na kwa Taifa zima ni 14% ya Watanzania tu wenye umeme. Miaka 50 baada ya Uhuru; hii ni aibu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako limekwishaipa Serikali kwa kipindi cha miaka mitano jumla matumizi ya kawaida Tshs. 197,207,126,900. Matumizi ya maendeleo kwa miaka mitatu ni Tshs. 804,123,439,500. Hii yote ni kwa ajili ya kutekeleza malengo ya MKUKUTA, ambao tuliambiwa ungepunguza umaskini na kukuza uchumi wa nchi yetu na watu wake. Lakini chini ya Serikali ya CCM inaonesha kuna mchwa wanaotafuna fedha hizo na hivyo kazi iliyokusudiwa inashindikana na ndiyo maana hadi leo tumeshindwa kuwa na umeme wa uhakika katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Rais akiomba ridhaa ya Watanzania Wilayani Mbinga, alitoa ahadi kuwa katika kipindi chake cha utawala, kila nyumba hapa Tanzania itakuwa na umeme uliouunganishwa katika Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inawataka Watanzania waanze kutembea kwenye maeneo ya wale waliowapa ridhaa na kutoa hukumu stahili wakati wa uchaguzi hapo mwezi wa kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inauliza: Je, pamoja na kutenga fedha hizo hali ya upatikanaji wa umeme imeimarika? Tuwaachie Watanzania watoe majibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ingeliwa makini, ingeliweza kuihamasisha Mifuko ya Hifadhi za Jamii ya Taifa kuwekeza kwenye mradi mmoja mkubwa wa umeme na leo tungeliwa na umeme wa uhakika na wa kutosha na pengine hata wa ziada na kuweza kuuza kwa majirani zetu na kuiongeza nchi yetu mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuonesha jinsi Serikali ya CCM ilivyochoka kuendesha nchi na kushindwa hata kufikiri na kubuni mipango mipya ya kuwakwamua Watanzania kutoka kwenye lindi la umaskini, hivi karibuni makampuni yanayotafuta gesi yamegundua mashapo mengine yenye hazina kubwa sana ya gesi huko Mkuranga. Jambo la kusikitisha ni kwamba, hadi sasa Serikali haijakuwa na mpango madhubuti wa kujenga kiwanda cha kuzalisha mbolea katika Wilaya ya Mkuranga, badala yake inategemea ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais mwaka 2007 wakati akifungua Mkutano Mkuu wa CCM kule Kizota, Mkoani Dodoma kuwa, kuna kampuni kubwa duniani itakuja kujenga kiwanda cha mbolea katika Mkoa wa Mtwara. Hadi sasa Watanzania wanasubiri kwa hamu Kampuni hiyo kuja lakini kwa utendaji wa Serikali ya CCM wanaweza wakasubiri maisha!

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa ni Serikali kushindwa kupanga mipango yake mapema na kukurupuka mwishoni na hapo ndipo mafisadi wanapozitafuna fedha za walipa kodi bila huruma. Kambi ya Upinzani inasema nchi yenye wasomi wengi wanaotegemewa katika mataifa mbalimbali duniani, haiwezi kuendeshwa kiholela bila ya kuwa na mipango madhubuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuelewa Raslimali za Nchi; kutokana na kukua kwa teknolojia ulimwenguni, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali itumie teknolojia ya *MAPING* ili kujua kwa kina rasilimali zote zilizoko nchini na namna tunavyoweza kuzitumia. Teknolojia hii inapatikana hata Spain.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Serikali imeshindwa kujua wingi wa rasilimali za madini tuliyonayo nchini, lakini bayo zaidi hata kuzigawa kwa kufuatia umuhimu wake imeshindikana. Hakuna nchi duniani *uranium* inaweza kutolewa kiholela au makaa ya mawe au shaba, chuma, *nickel* na kadhalika (*industrial minerals*), isipokuwa Tanzania.

Sababu kubwa ni kwamba, hatujui thamani, wingi na pahala zilipo na kwa kiasi gani zitasaidia uchumi wetu. Huku ni kukosa mipango mizuri na endelevu na

kutokutumia vyema rasilimali watu. Tanzania imekuwa kama shamba la viazi, kila mwekezaji anakuja anachimba na kuondoka navyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri utafutwe utaalamu haraka sana kabla hatujaingia katika Shirikisho la Kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki ili Watanzania wajue rasilimali zao kikamilifu ili kuepuka migongano ya kijamii inayoweza kuja baadae kwa kushindwa kwetu kusimamia ipasavyo utajiri wa Watanzania.

Tukifanikiwa kujuja rasilimali tulizonazo, hata Taasisi ya Uwekezaji ya Taifa (*Tanzania Investment Centre – TIC*), watakuwa wanatoa vibali kwa wawekezaji kulingana na rasilimali zilizopo, wakijua mazingira halisi ya uwekezaji. Hii itasadid Serikali kukusanya kodi kulingana na uzalishaji na rasilimali zilizopo, badala ya kutoa vibali kwa wawekezaji bila kuzingatia maliasili zilizopo (*Natural Resources*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa pia niseme tunarudia kauli yetu ya awali kuwa ni vyema Serikali ikazipa uwezo wa kujiendesa NDC na STAMICO ili ziwe na uwezo wa kumiliki maeneo ya *industrial minerals* na kuingia ubia na makampuni ya nje bila ya kudhulumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kupitishwa kwa Sheria Mpya ya Madini ya Mwaka 2010, serikali ilitarajia kukusanya mapato mengi zaidi kutokana na Sekta ya Madini. Kambi ya Upinzani imeshtushwa sana na uamuzi wa serikali kuamua kurejesha msamaha wa kodi ya mafuta kwa makampuni ya madini. Mwaka 2008/2009, serikali iliyasamahe makampuni ya madini kodi yenye thamani ya zaidi ya shilingi 91 bilioni katika ushuru wa mafuta. Mbaya zaidi, ushuru huu unatolewa kwa makampuni ya madini na siyo kwa wakandarasi wa ndani na hivyo kuua kabisa uwezekano wa kuwezesha wakandarasi (*contractors*) wa ndani kushiriki katika Sekta ya Madini.

Kambi ya Upinzani inataka serikali ianze kutekeleza mara moja Sheria ya Wahandisi ya Mwaka 1997, ambapo wakandarasi wa kigeni wanalipa 15% ya kodi ya zuio na kwamba kampuni yoyote ya madini yenye kuchimba yenyewe (*owner mining*) na kama ni kampuni ya kigeni ilipe 15% kodi ya zuio (*Withholding Tax*) kama mkandarasi wa kigeni. Lengo ni kuunganisha Sekta ya Madini na Sekta ya Ujenzi na hivyo kuongeza ajira na kubakiza fedha za uwekezaji hapa nchini. Asilimia 25 ya mapato ya kampuni ya madini hutumika kulipia gharama za kuchimba madini.

Hiki ni kiasi kikubwa, kuiachia makampuni ya madini tena kwa kupitia msamaha wa kodi na wala siyo kutokana na taratibu za kawaida za kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mojawapo ya rasilimali na nyenzo muhimu katika kukuza uchumi na kupambana na umaskini kwani ndiyo inayotoa ajira kwa wastani wa asilimia 75 ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania bado hawajanufaika na rasilimali hii ambayo ina ukubwa wa kilomita za mraba 875,000. Kutokana na taarifa ya Waziri wa

Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; ni viwanja 18,641 na mashamba 734 katika mikoa 21 ambavyo vimepimwa na watusika kupewa Hati na viwanja 56,743 vilipimwa kupitia Mradi wa Kupima Viwanja 20,000 kuanzia mwaka 2002/2003 hadi Juni, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizingatia kwamba, umuhimu wa rasilimali hii siyo tu kumwendeleza Mtanzania kiuchumi bali pia kumpa urithi wa asili; ni kwa vipi kwa mwenendo huu Watanzania wanaoongezeka kila mwaka wataweza kumilikishwa ardhi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, utambuzi wa ardhi ni mojawapo ya chanzo kikuu cha mapato kwa Serikali kupitia kodi ya ardhi na kodi hii haiwezi kulipwa kama wamiliki wa ardhi hiyo hawakusajiliwa na kupewa Hati. Mfano, Wizara ya Ardhi ulikusanya kodi ya ardhi ya Tshs. 586,998,900 kwa Mkoa wa Dar es Salaam baada ya kusajili nyumba 217,407 tu. Je, kama zoezi hili la kusajili na kutoa Hati kwa ardhi yote (nyumba) ni kiasi gani kama nchi itakuwa ikikusanya kwa mwaka? Jambo hili lingeweza kusaidia kupata mapato badala ya kwenda kukopa kwenye Mabenki ya Biashara.

Kambi ya Upinzani ilitegemea kwa umuhimu wa pekee na kwa kuzingatia ushirikiano wa Afrika Mashariki, mipango ingelikuwa wazi zaidi na makini katika umilikishaji wa viwanja na mashamba kwa Watanzania, pia ikichukuliwa kuwa inaongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utambuzi wa Rasiliamali Watu; lipo tatizo la kuwa na takwimu sahihi za rasilimali watu ambao watatoa huduma katika sekta zote za uchumi wetu. Kwa mfano, Sekta za Afya na Elimu zina upungufu mkubwa wa watumishi na ukiangalia mipango yetu hasa katika nyanja za Sayansi, mahitaji ni makubwa kuliko uzalishaji wa wataalamu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa Serikali ina lengo thabiti la kuwa na mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini unaotekelezeka, Kambi ya Upinzani inaendelea na ushauri wake kwamba, Serikali inastahili kujipa muda kutathmini MKUKUTA na kushirikisha wadau wote katika kuandaa Mpango Mbadala wa Kukuza Uchumi, kuongeza ajira za uhakika na kupunguza umaskini. Vinginevyo, tutaendelea kufanya makosa yale yale kila uchao. Serikali makini huwa hairudii makosa yale yale. Waingereza wanasema; *Once beaten twice shy. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha Utawala Bora na Uwajibikaji; dhana nzima ya Utawala Bora na Uwajibikaji ndiyo msingi mkuu wa kujenga Taifa imara na lenye uchumi endelevu. Mazingira mazuri ya ufanyaji biashara na uwekezaji katika ngazi zote za kiuchumi na pia katika ngazi zote za kisiasa na kiutawala huimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayoheshimiwa na raia wake, hujengwa katika misingi ya Utawala Bora na Uwajibikaji kwa viongozi wake. Kambi ya Upinzani inaona kuwa, Tanzania ni nchi inayoheshimika duniani, lakini suala la Utawala Bora na uwajibikaji bado liko nyuma sana na hivyo kusababisha kuwepo kwa tatizo la rushwa na kuota mizizi katika ngazi zote za kiutawala. Wenzetu waliodhamiria kujenga Utawala

Bora, kwa mfano, Rwanda, wanaochunguzwa kwa rushwa, hupumzishwa hadi uchunguzi unapomalizika; sisi hatufanyi hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Benki ya Dunia ya Mwaka 2009 inaonesha kuwa, Tanzania ni nchi ya 131 katika suala zima la urahisi wa mazingira ya ufanyaji biashara. Nafasi hiyo inatokana kwa kiwango kikubwa na urasimu katika utekelezaji wa kazi zake za uendeshaji wa Serikali wa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na msukusuko wa uchumi duniani, ugumu wa kufanya biashara katika nchi yetu ni jambo ambalo limesababisha kuteremka kwa uwekezaji kutoka nje (*FDI*), toka dola milioni 744 mwaka 2008 hadi dola milioni 650 mwaka 2009, sawa na upungufu wa 14.5%. Pamoja na mambo mengine, kubwa ni urasimu kwa wawekezaji wa nje na hata wa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu imekuwa ikitoa ahadi za kurekebisha hali hiyo lakini kila uchao hali inazidi kuwa mbaya. Kupata leseni ya biashara Rwanda inakuchukua siku tatu, Tanzania katika makaratasi inatamkwa isizidi siku tano, lakini hali halisi ni miezi mitatu na hata kujibiwa barua ya kuthibitisha kupokea barua yako inaweza kukuchukua mwezi mmoja. Hivi hata hili nalo linahitaji wahisani kuja kutusaidia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki Tanzania ilipewa miaka mitatu na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ili ianishe maeneo gani ya kiuchumi au kibiareshara inaweza kulisha Soko la Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasikitika sana kwa Tanzania kupitia asasi zake za kiutendaji kuwa hadi sasa nchi husika bado hazijapewa taarifa rasmi kuhusu maeneo ambayo Tanzania ina fursa bora zaidi za uzalishaji (*Comperative Advantage*) na kama tukijipanga vizuri tunaweza kuuza chakula katika soko hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo wasiwaso hasa ukiangalia bajeti ya mendeleo ambayo ni 3.7% ukilinganisha na Kenya na Uganda ambako ni wastani wa asilimia 9% kwa mwaka huu wa fedha.

Tanzania itakuwa katika Soko la Afrika Mashariki na pia itakuwa msafirishaji wa malighafi za viwanda vya Kenya, kwani viwanda vyetu hata vya ngano vinaagizia ngano nzima kutoka Australia na Saudi Arabia; hii ni aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inatia aibu kwa Serikali hata kushindwa kuwataarifu Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi ambao ni washirika wenzetu wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kuhusu uwezo wa wakulima wetu kiuzalishaji.

Upo wasiwaso kuwa, kama tulivyoshindwa kutumia *AGOA* pia tutashindwa kutumia Soko la Pamoja la Afrika ya Mashariki; ipo hatari ya Tanzania kuwa soko tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukimya wa Tanzania katika suala hilo sasa hivi Uganda ndiyo inayoonekana kama nchi inayoweza kuzilisha nchi zote za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Takwimu zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 2008 na 2009 Uganda imeuza tani 100,000 za nafaka kwa Kenya na 13,000 kwa Rwanda. Tanzania pamoja na miundombinu mibovu lakini wakulima wetu wana uwezo mkubwa wa kuzalisha chakula, tatizo ni kuwawezesha na kuwapatia bei muafaka ya mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii yote inatokana na kutokuwa na mipango madhubuti ya kuitoa nchi kwenye umaskini uliokithiri na badala yake nchi inazidi kuingizwa kwenye mikopo isiyoleta tija kwa Watanzania. Hali ya kushindwa kujifaidisha na kuwemo kwetu katika Jumuiya na Soko la Pamoja la Afrika Mashariki haitofautiani na ile ya Daraja la Umoja kati ya Msumbiji na Tanzania ambapo hadi leo Tanzania haijajipanga vizuri jinsi ya kutumia daraja hilo kiuchumi na kijamii. Hivi ni lini sisi tutaamka?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Pesa za Kunusuru Uchumi. Rushwa ni hatari na ni uhalifu dhidi ya binadam kwani husababisha jamii kupata madhara makubwa kuliko inavyofikiriwa na watu wengi. Hii inatokana na tafiti zilizofanywa na kuwasilishwa katika semina iliyofanyika nchini Uganda na kuwahusisha wabunge chini ya APNAC.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mtu asiyejua kuwa Serikali ililetu ombi kwenye Bunge lako Tukufu kuomba idhini ya kutumia kiasi cha shilingi trilioni 1.7 kwa ajili ya kuimarisha uchumi kutokana na mtikisiko wa uchumi wa dunia uliotokea mwaka 2009. Kambi ya Upinzani iliamini kabisa kuwa wakati Serikali inaomba idhini ya Bunge ya matumizi ya fedha hizo, dhahiri ilikwishafanya upembuzi yakinifu kuhusiana na matumizi ya fedha hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina maana kwamba sekta au makampuni ambayo yalikuwa yanadai kuwa yameathirika sana na mtikisiko huo yalitakiwa kwanza kufanyiwa ukaguzi ili kujua hali halisi ya kuathirika kwao na kiasi gani kitawawezesha kurudi katika biashara walizokuwa wakizifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ilitoa angalizo katika hotuba yake kuhusiana na fedha hizo kuwa inaweza kuwa ni njia nyingine ya ufisadi uliopindukia kama ilivyokuwa katika suala la *EPA* ambalo hadi sasa Watanzania hawajapata majibu sahihi kutoka kwa wale wanaotakiwa kutoa majibu kuhusiana na ufisadi

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tetesi kuwa makampuni ambayo yamepata fedha hizo yamefanya udanganyifu mkubwa na kuchukua fedha za bure kama ilivyokuwa katika suala zima la *EPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika takwimu za fedha zilizotolewa na Benki Kuu zinaonyesha kuwa fedha zilizopata idhini ni Shilingi trilioni 1.692 na zile zilizogawiwa ni shilingi trilioni 1.28. Kwa kuangalia tofauti katika ya fedha zilizoidhinishwa na zile zilizotolewa utaona kuna bakaa (*change*) kama wanavyoita wenyewe, ya shilingi bilioni 412. Kwa kuwa kazi waliyopewa na Serikali imekwisha Benki Kuu inafanya utaratibu wa *ku-exit* hadi leo bado ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo haujafanyika, hii ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa fedha yoyote ya Serikali inayotumiwa baada ya kupata idhini ya Bunge inatakiwa ikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kambi ya Upinzani inauliza, je, ukaguzi kwa makampuni yaliyopata fedha hizo umefanywa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ameyakagua? Na kama tayari taarifa yake iko wapi? (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Kambi ya Upinzani inataka kujua ni kwa nini kila Serikali inapofanya manunuzi au kutoa huduma fulani ni lazima fedha zibakie? Mfano katika manunuzi ya rada, ipo *change* ya bilioni 29, na tunaamini kabisa hata kwenye ununuzi wa ndege ya Rais kuna bakaa au *change*. Huu ni udhaifu mkubwa sana unaotoa mianya ya rushwa kubwa katika nchi yetu (*grand corruption*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema kuwa rushwa ni *crime against humanity*, hivyo basi Serikali za Mataifa ya nje zimekuwa zikipambana lakini pale ambapo Mataifa hayo yamefanya kazi na kumaliza ni kwa nini Serikali yetu inashindwa kumalizia upande wake wa wajibu? Huu ni udhaifu mkubwa unaoonyesha kuwa Serikali imeshindwa kupambana na rushwa kwa vitendo au haina dhamira ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inazitaka nchi za nje na mashirika yao kutusaidia kutoa taarifa za watu wetu wanaoficha mabilioni ya fedha kwenye mabenki yao nje ya nchi na yale ya *Off-shore banking*, ili tuweze kupambana na rushwa kubwa. Sheria ya Rushwa inasema anayetoea na anayepokea pamoja na anayetunza wote ni wakosa, hivyo benki zinazotunza fedha hii chafu nazo ni wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Public Private Partnership (PPP)*. Kambi ya Upinzani tokea mwaka 2004 kuitia hotuba zetu za bajeti tumekuwa tukiitaka Serikali kuweka utaratibu wa kuendesha miradi yake kwa ubia na sekta binafsi (*Public Private Partnership*).

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuwa jambo hilo jema limepigwa danadana, hadi pale *IMF* na wahisani walipopunguza misaada yao ndio leo Serikali inaleta Muswada wa Sheria kwa dharura ili kuanzisha mfumo huo. Ni kwa nini Serikali isiupokee ushauri wa Watanzania mapema hata kama ni kutoka Upinzani, ili kuondokana na kutegemea wahisani kila uchao? (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kuwa ushauri wetu kwa Serikali toka mwaka 2004 kuhimiza uanzishwaji wa *PPP* sasa umefanyiwa kazi na tunaamini kuwa matunda yake yataanza kuonekana hivi karibuni baada ya Sheria kuitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muda na Ukuaji wa Uchumi (*Time management*). Muda ni bidhaa ambayo pindi ikishapita basi haipatikani tena. Tanzania katika mipango yake ya maendeleo suala la muda limekuwa halitiliwi manani au kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani baada ya kufanya tafiti imegundua kuwa muda unaopotezwa na watumishi wa umma au wajasiriamali kwa kuja au kutokujua ni mwingi mno. Maeneo yafuatayo ndiyo yamekuwa yakikwaza hata shughuli za maendeleo: kwanza, ni kwenye mabenki yetu ambapo inasababisha hata Watanzania kukata tamaa ya kufungua akaunti, pili ni misururu mirefu barabarani jambo linalosababisha kuchelewa kwa shughuli za kiuchumi, tatu ni katika vyombo nya kutoa haki, yaani Mahakama na Polisi na nne, ni hospitali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na usumbu huo, watumishi wa Umma na wajasiriamali wanajikuta kwa siku wamekwishapoteza zaidi ya saa nne. Wakati umefika sasa kwa Serikali kutambua kuwa muda ni fedha (*Time is money*) hivyo ni lazima itafiti, ichambue na kuona ni fedha kiasi gani tunapoteza kwa njia ya kutokusimamia vizuri matumizi ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii si ngumu, kwani inajulikana kwa mfano, wastani wa malipo ya mfanyakazi ni kiasi gani kwa saa. Ndiyo maana wenzetu katika nchi zilizoendelea zinatumia mfumo wa *to clock time in and time out* na kinachoangaliwa pia ni saa halisi ya mtumishi kufanya kazi na siyo saa ambayo mtu anapaswa kuwa ofisini, lakini hayuko, au akiwepo anapiga hadithi, au anatumia rasilimali za Serikali kama simu kufanya biashara zake binafsi.

Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inataka Serikali ianze kutafuta njia ya kupunguza muda unaopotea, ama kwa kuchelewa kutolewa maamuzi au kutokuwa na mipango imara ya majukumu ya mfanyakazi.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato ya ndani pia bado ni tatizo kubwa linalotusumbua. Kwa mfano, malengo ya kukusanya mapato ya ndani kwa mwaka 2008/2009 yalikuwa ni 15.9% ya pato la Taifa, mwaka 2009/2010 yalikuwa ni 16.4% ya pato la Taifa na mwaka 2010/2011 ni 17.2% ya pato la Taifa. Shabaha ni kufikia 18.3% kwa mwaka 2011/2012. Je, tunapokuwa tuko nyuma kiasi hicho katika ukuSanyaji wa mapato, lile lengo la awali limesahauliwa au limeonekana halitekelezeki? Ni kitendawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapendekezo ya Mpango uliowasilishwa, Serikali Kuu, Mikoa na Halmashauri zinatakiwa katika kipindi cha miaka mitatu ziweke kipaumbele katika mambo 10, lakini nitataja moja tu nalo ni (ii) kuhakikisha kuwa rasilimali (fedha) zinaelekezwa kwenye utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi (2005), *MDGS*, **MKUKUTA II**, **KILIMO KWANZA** na vile vile mambo ya **MTAMBUKA** kama vile **HIV** na **AIDS**, Maboresho, Jinsia na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuja hivi Kilimo Kwanza ni Mpango tafauti na ule wa **MKUKUTA**, **MKURABITA** (ambao sasa hautajwi) na **MDGS**? Hii si kujirudia rudia kwa mipango kama hii yaani *overlapping*.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya Serikali. Bajeti ya 2007/2008 ilitumia zaidi katika matumizi ya kawaida (Tshs. 3.886 bilioni.) kuliko matumizi ya maendeleo (Tshs. 2,201 bilioni). Bajeti ya 2008/2009, Serikali ilitumia zaidi katika matumizi ya

kawaida (Tshs. 4.726 trilioni) kuliko matumizi ya maendeleo (Tshs. 2.489 trilioni), Bajeti ya 2009/2010 Serikali ilitumia Tshs. 6.7 trilioni na matumizi ya maendeleo Tshs. 2.8 trilioni. Miaka 12 ya bajeti za nyuma, matumizi halisi ya maendeleo yamekuwa madogo kuliko yalivyoidhinishwa katika bajeti zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kama tulivyowahi kusema kuwa ukubwa wa Serikali utasababisha matumizi makubwa ya kawaida. Kambi ya Upinzani inaona kuna kasoro kubwa ya kiuwiano kati ya matumizi ya kawaida na yale ya maendeleo, hivyo kuchelewesha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Fedha nyingi zinatumika katika uendeshaji wa Serikali kuliko katika maendeleo na huduma za jamii na hivyo kupanda kwa pato la Taifa kutakuwa ni kidogo na manufaa ya moja kwa moja hayawezi kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona tatizo hili linatokana na ukubwa wa Serikali Kuu na taasisi zilizo chini yake na pia Serikali kuunda taasisi na wakala ambazo zinachukua nafasi ya mashirika yaliyobinafsishwa wakati hazichangii katika pato la Taifa na hivyo kuzidisha ukubwa wa Serikali. Pili, ni matumizi ya kifisadi yasiyoleta tija kwa nchi na safari zisizoisha za viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linadhihirika tena katika mapendekezo ya Bajeti ya mwaka huu wa fedha wa 2010/2011 ambayo yamewasilishwa na Mheshimiwa Waziri hapa. Katika mapendekezo haya ambayo kwa hakika yanaacha maswali mengi kuliko majibu, Serikali imesema inakadiria kukusanya kutoka mapato ya ndani Tshs. 6,003 trilioni lakini papo hapo bajeti yake ya matumizi ya kawaida (*recurrent budget*) ni Tshs. 7,790 trilioni. Tunataka Waziri wa Fedha atupe maelezo, Serikali itatoa wapi ziada ya Tshs. 1,787 trilioni kugharimia bajeti hiyo ya matumizi ya kawaida. Huu ni mfano mmojawapo unaoonyesha kuwa bajeti hii ni ya kukurupuka na isiyotekelzeza kama vile ilivyoshindikana kutekeleza ahadi zilizomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ulinganisho wa takwimu za matumizi ya kawaida kwenye pato la Taifa (GDP) kwa Tanzania, Kenya na Uganda utaona kuwa takwimu za Kenya zinapanda na kushuka toka mwaka 2007/08 - 2010/2011 (20.5%, 19.4%, 20.0% na 19.4%), Uganda takwimu zao za matumizi zinashuka (12.0%, 11.8%, 10.3% na 9.8%) wakati takwimu za matumizi ya maendeleo zinapanda (5.6%, 9.9%, 10.2% na 10.3%). Tanzania takwimu za matumizi ya kawaida zinaonyesha kupanda (14.9%, 17.7%, 21.5% na 22.7%) kwa mtiririko wa miaka na za maendeleo Tanzania 2007/2008 hadi 2010/2011 ni 7.9%, 8.0%, 3.1% na 3.7%, hii ni hatari kwa ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi kwenye manunuzi. Serikali kuitia kwa Waziri Mkuu ilikwishatoa agizo kuhusiana na kukataza kununua magari ya kifahari yanayotumiwa na viongozi wa Serikali, lakini toka atoe rai hiyo hadi leo hakuna utekelezaji wowote na Serikali imeendelea kuwanunulia watumishi wake magari hayo. Samani zinazonunuliwa katika maofisi ya Serikali na kwenye nyumba za viongozi kila mwaka zinatoka nje ya nchi. Hizi zote zinazidisha matumizi kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utashi wa Kiongozi Mkuu ni muhimu sana katika kila jambo linalohusiana na mustakabali wa nchi. Mfano mzuri ni Rais Kagame wa Rwanda ambaye amekuwa mfano wa kuigwa katika kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Alidiriki kukamata magari yote ya Serikali ya kifahari na kuyauza na alikusanya USD 3 milioni na kutoa waraka wa aina ya magari yatakayotumiwa na viongozi wa Serikali yasizidi cc2500, matumizi ya simu yasizidi USD 150 na kuzuia *roaming telephone services*. Hakuishia hapo tu kwani hata yale magari ya wahisani wa maendeleo nayo yaliuzwa kwani fedha tunazoiita misaada si misaada kwa maana halisi ya misaada bali ni mikopo kwa nchi, kwani katika mradi wa kupunguza umasikini kati ya USD 5 milioni, USD 1 ni magari, USD 1 milioni ni samani za ofisi, USD 1 milioni ni mishahara na USD 1 milioni ndio za kuondoa umaskini. Alifanya maamuzi na akayasimamia. Huu ndio utashi na ujasiri wa kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kama kwa kipindi chote ambacho Serikali ya CCM imekuwa madarakani kama kungekuwa na utashi wa kweli wa kuwaondolea Watanzania umaskini basi hilo lingewezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani katika bajeti zake zote mbadala imekuwa ikitoa mwanga kwa Serikali wapi viro vyanzo wa mapato mbadala, lakini ufuutiliaji wa vyanzo hivyo umekuwa ukipuuzwa na Serikali ya CCM labda kwa sababu vimetolewa na Upinzani lakini wakati huo huo isione vigumu kuendelea kuwakamua Watanzania maskini ambao inaendelea kuwafukarisha kila uchao kutokana na sera zake mbovu. Serikali inasahau kuwa wananchi ni wadau wakubwa wa maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu misamaha ya kodi. Ukiangalia takwimu zilizotolewa katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha kuwa katika kipindi cha miezi sita tu kabla ya kusoma Mpango wa Bajeti Bungeni, Serikali ilikwishatoa misamaha ya kodi inayofikia Tshs. 324.14 bilioni. Kwa mwaka uliopita pekee, Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali inaonyesha kuwa misamaha ya kodi ilifikia Tshs. 725 bilioni. Hizi ni fedha nyingi sana za Watanzania maskini. Misamaha hii kwa kiasi kikubwa ndio tuliyokuwa tunaipigia kelele kwani wanapewa wawekezaji katika tasnia ya

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa kila mwaka kelele zinapigwa kuhusu misamaha ya kodi, bado hali haijawa nzuri. Zaidi ya Tshs. 673 bilioni ya mapato yametolewa kama misamaha (Bajeti 2008/2009 inakadirisha misamaha ya kodi kuwa takribani shilingi 819.9 bilioni na mwaka 2009/2010 misamaha ilikuwa ni 3% ya pato la Taifa). Kwa maelezo ya bajeti ya Waziri, wenzetu Kenya na Uganda misamaha ya kodi ni 1% ya Pato la Taifa kwa Kenya na 0.4% kwa Uganda wakati Tanzania ni 2.1% ya pato la Taifa. Ni lazima tuandae utaratibu wa kupunguza misamaha hiyo ili kupunguza rushwa na bajeti tegemezi, lakini pia kuwa na utaratibu ulio wazi zaidi wa kutoa misamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Misamaha hii ya kodi ndicho chanzo kikuu cha kuleta nakisi (*deficit*) katika bajeti yetu. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inatarajia misamaha hiyo ambayo kwa takwimu za Serikali ni asilimia 30 ya makusanyo yote ya kodi au 3.5 ya pato la nchi itapunguzwa angalau kuwa sawa na wenzetu wa Kenya au Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha leo kuona Serikali yetu iko tayari kuwabebesha Watanzania mzigo wa madeni kwa kukopa katika mabenki ya biashara lakini inaogopa kuyabana makampuni ya nje inayoyasemehe kodi - badala yake inayabembeleza. Mtanzania kufungiwa biashara zake habembelezwi. Hii ni hatari katika kujenga Taifa linalojiamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jambo hili linawezekana kama kweli tutakuwa makini katika kusimamia mipango yetu, jambo ambalo limekuwa ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu Wa Hesabu Za Serikali inaonyesha kuwa Tshs.16,785,000/- ililipwa kwa makosa kwa mtumishi kama posho ya kujikimu kwa afisa huyo kuhudhuria kozi fupi ya siku 30 huko Swaziland.

Kambi ya Upinzani inasema malipo hayo ni sehemu tu ya mchezo unaoendelea kwa Wizara/Idara na taasisi zote za Serikali kupeleka watumishi nje ya nchi kwa baraka za Idara kuu ya Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inauliza, je, mtindo huu wa kuwadharau wataalam wetu waliopo katika vyuo vyetu umeipoteza Serikali kiasi gani? Kama gharama kwa mtumishi mmoja kulingana na cheo chake na kozi anayoisoma ni kati ya USD 5,000-8,000 kama *tuition fees*, posho ni kati ya USD 350-500 kwa siku, usafiri wa kwenda na kurudi ni kati ya USD 3,000-4,000. Jumla ni takriban USD 22,500 kwa kozi ya wiki tatu (siku 21). Hizi ni sawa na Tshs. 29,250,000/-.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtumishi mmoja wa Serikali anaweza kulipiwa mamilioni haya kwa muda wa siku 21, kiasi gani kimepotea na ni watumishi wangapi wa Serikali wamekwisha kwenda nje kwa utaratibu kama huo? Je, fedha hizo zingeweza kuwalipia wanafunzi wangapi katika vyuo vya elimu ya juu hapa nchini amba Serikali huwatimua na hata kuwapiga mabomu ya machozi ikidai haina fedha za kuwagharimia masomo yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tathmini ya matumizi ya fedha ambazo zimekwishatumika kwa njia hiyo kwa Wizara, taasisi, idara na wakala za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu amegundua malipo ya asilimia 30 ya nyumba kwa watumishi lakini ukweli ni kwamba watumishi hao wanaishi katika nyumba za Serikali. Mdhibiti amegundua malipo ya Tshs. 13,299,400/- alizolipwa mtumishi anayeishi katika nyumba ya Serikali kama posho ya nyumba, TShs. 282,453,350/- kama gharama za hoteli wakati wahusika walikwishapewa posho za kujikimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchezo huu wa matumizi ya fedha za Serikali ndio unaosababisha Bajeti ya Maendeleo kuzidi kuwa ndogo siku hadi siku na matumizi ya kawaida kuendelea kupanda. Kambi ya Upinzani inachelea kuamini kama kweli

wanaofanya udanganyifu huu ni kada ya chini ya watumishi au ni wale wa ngazi za juu wanaofanya hivyo kwa malengo ya kujitajirisha huku Watanzania wanyonge wakiendelea kuteseka kwa kukosa huduma nyingi za jamii. Mbali ya hayo, jumla ya masurufu ya Tshs. 1,174,930,558 hayakurejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na ukiukwaji mkubwa katika manunuzi kunakofanywa na Wizara kama ilivyobainishwa na Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kambi ya Upinzani imekuwa ikilipigia kelele suala hili la manunuzi kwa muda mrefu sasa kwani ndiyo sehemu inayosababisha kuwepo kwa ujisadi papa na nyangumi na kuyumbisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubinafsishaji. Hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2009, mashirika ya umma 336 yalikuwa yamebinafsishwa ambapo ama yalikuwa yameuzwa na kuingia mikataba na mengine kuacha kazi zilizokuwa za msingi kabla ya mashirika hayo hayajauzwa kwa watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni asilimia 19% tu ya mashirika yaliyouzwa au kuingia ubia ndiyo yanayofanya vizuri, 44% yanajiendesa kihasara na 37% hayafanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Kambi ya Upinzani hapa inatokana na ukweli kuwa Serikali imekuwa ikipata mapato kidogo sana kama ushuru wa bidhaa za viwandani. Takwimu zinaonyesha Tshs. milioni 84,899.9 ongezeko kidogo ambalo haliendani na idadi halisi ya viwanda na hivyo kulifanya zoezi zima la ubinafsishaji kuwa ilikuwa ni mradi binafsi wa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kurejea upya makubaliano ya uuzaaji wa viwanda vyetu na pale ikibainika kuna udhaifu kwa upande wa wanunuzi hatua stahili za kurekebisha hali zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mishahara kwa watumishi wa umma. Kambi ya Upinzani toka mwaka 2007 imekuwa ikitoa mapendekezo yake kuhusiana na kuongezwa kwa mishahara kwa watumishi wa umma na pia kwa kuonyesha vyanzo mbadala vya mapato ili kutimiza dhamira hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti mbadala ya mwaka 2007/2009 tuliiata Serikali kupandisha kima cha chini hadi Tshs.250,000/- kwa mwezi kulingana na hali ya maisha ya siku hizo. Katika bajeti yetu ya mwaka jana tuliltaka Serikali kupandisha kima cha mshahara hadi Tshs. 315,000/. Sababu za Kambi kutoa ongezeko hilo ziliezwa vizuri katika hotuba yetu ya Msemaji wa Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa kama Serikali ingelikuwa na mipango madhubuti katika uendeshaji wa shughuli zake kusingekuwa na kitu kinachoitwa migomo ya watumishi kudai mishahara na malimbikizo yake. Mamlaka zote zinaelewa sheria na kanuni za utumishi ziko vipi, hivyo basi ilitakiwa kupanga bajeti yake kwa kuzingatia watumishi wake kwani watumishi ndiyo injini ya kuendesha

uchumi. Tatizo ni kuwa Serikali inakuwa na mipango ya zimamoto, ndio maana leo kwa sababu ya uchaguzi watumishi wanapandishiwa mishahara, wakati huko nyuma Serikali ilisema haina uwezo na hata kusema haina haja na kura za wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukuaji wa uchumi na malengo ya maendeleo ya milenia. Waziri ameeleza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne bila kuyahuisha mafanikio hayo na Malengo ya Maendeleo ya Milenia ambayo yamekubaliwa na Jumuiya ya Kimataifa yawe dira ya mipango ya maendeleo ya nchi maskini kama Tanzania. Malengo ya milenia ni tafsiri, yenyewe vigezo, ya mapambano dhidi ya maadui wakubwa watatu umaskini, ujinga na maradhi. Tunaweza kuyahesabu kuwa ni malengo yetu walijotuweka waasisi wa nchi yetu na hususan Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere tangu tunapigania uhuru wa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji endelevu wa pato la Taifa ni muhimu kwa kufikia malengo ya milenia. Ukuaji wa pato la Taifa wa wastani wa asilimia 7.1 kwa mwaka haukusaidia sana kupunguza umaskini. Ukuaji wa uchumi haujawanufaisha Watanzania walio wengi. Inawezekana takwimu za pato la Taifa zina makosa. Vile vile mfumko wa bei kati ya 2001 na 2007 kwa kutumia bei za bidhaa zinazonunuliwa na Watanzania wa kawaida zilizoainishwa katika *Household Budget Survey (HBS)* 2007 zimeongezeka kwa asilimia 93 wakati mfumko wa bei unaoleezwa na Serikali kati ya 2001 na 2007 ni asilimia 42. *HBS* 2007 inaonyesha kuwa mfumko halisi wa bei ni zaidi ya mara mbili ya ule unaotangazwa na Serikali. Tanzania bado inakabiliwa na udhaifu mkubwa wa takwimu na kwa hiyo kuathiri uibuaji wa sera na mipango ya maendeleo. Bila kuwa na takwimu sahihi hatuwezi kupanga na kusimamia maendeleo yetu kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo halisi yako saba na yanakusudia ifikapo mwaka 2015:-

(i) Kutokeza umaskini uliokithiri na njaa. Kupunguza kwa asilimia hamsini idadi ya watu maskini ambao kipato chao ni chini ya dola moja kwa siku na kupunguza kwa asilimia hamsini idadi ya watu wanaokumbwa na njaa.

(ii) Elimu ya msingi kwa wote kuhakikisha watoto wote wa kike na wa kiume wanahitimu elimu ya shule ya msingi.

(iii) Usawa wa kijinsia na fursa sawa kwa wanawake kuondoa tofauti ya uwiano wa wasichana na wavulana katika elimu ya msingi ifikapo mwaka 2005 na katika ngazi zote za elimu ifikapo 2015.

(iv) Kupunguza vifo vya watoto wachanga, kupunguza kwa theluthi mbili vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano.

(v) Upatikanaji wa huduma bora za uzazi, kupunguza kwa robo tatu idadi ya vifo vya uzazi.

(vi) Kupambana na UKIMWI, Malaria na magonjwa mengine, kuzuia kabisa na kuanza kupunguza maambukizo mapya ya UKIMWI, kuzuia kabisa na kuanza kupunguza milipuko ya malaria na magonjwa mengine hatari.

(vii) Kulinda mazingira yetu, kujumuisha misingi yote ya maendeleo endelevu katika sera na programu za kila nchi; kuzuia upotevu wa rasilimali ya mazingira.

(viii) Lengo la nane linahimiza ushirikiano wa Kimataifa kuziwezesha nchi maskini kufikia malengo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi wa Bajeti za Kaya wa mwaka 2007 (2007 *Household Budget Survey*) unaonyesha kwamba umaskini umepungua kidogo sana toka asilimia 38.6 mwaka 1990, asilimia 35.7 mwaka 2001 mpaka asilimia 33.3 mwaka 2007. Kwa kuwa idadi ya Watanzania inaongezeka kwa asilimia 2.9 kila mwaka. Idadi ya watu maskini imeongezeka kwa milioni moja na nusu toka watu milioni 11.4 mwaka 2001 na kufikia watu milioni 12.9 mwaka 2007. Izingatiwe kuwa kigezo kilichotumiwa na *HBS* 2007 cha mtu mzima kutohesabiwa kuwa siyo maskini ni kutumia shilingi 641/- au zaidi kwa siku ukiwa Dar es Salaam, shilingi 532/- au zaidi kwa siku ukiwa katika miji mingine na shilingi 469/- au zaidi kwa siku ukiwa vijijini. Ni wazi kigezo hiki ni cha chini mno na bado idadi ya watu maskini imeongezeka. Wanaoathirika zaidi na umaskini ni wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo kilichokubaliwa Kimataifa kuwa matumizi ya chini kabisa kwa mtu mzima asihesabiwe kuwa ni maskini wa kutupwa ni dola moja kwa siku. Benki ya dunia inakadiria kwa kutumia kipimo hiki, umaskini Tanzania umeongezeka toka asilimia 73 ya Watanzania wote mwaka 1990 mpaka kufikia asilimia 89 mwaka 2000. Kwa kutumia kigezo hiki cha Kimataifa na takwimu za uchunguzi wa bajeti za kaya wa 2007, zaidi ya Watanzania 90 katika kila Watanzania 100 ni masikini wa kutupwa. Waheshimiwa washiriki wa warsha hali hii inatisha. Hatuwezi kuwa na mshikamano wa kweli wa kitaifa ikiwa ukuaji wa uchumi unawanufaisha watu wachache na kuwaacha zaidi ya Watanzania milioni 36 wakiwa maskini wa kutupwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya milenia ni pamoja na kupunguza kwa nusu asilimia ya Watanzania wenye njaa. Watanzania wenye lishe duni na utapiamlo wameongezeka toka asilimia 28 ya Watanzania wote mwaka 1990 na kufikia asilimia 41 mwaka 1995 na kupungua kiasi na kufikia asilimia 35 mwaka 2007.

Ili kupunguza umaskini tunahitaji kuongeza ajira bora na za uhakika (*decent work*). Benki ya Dunia inakadiria kuwa Watanzania wengi mno wanategemea ajira zisizokuwa na uhakika. Watu wenye ajira zenye mashaka wamepungua kidogo toka asilimia 92 ya Watanzania wote wenye umri wa kuajiriwa mwaka 2000 na kufikia asilimia 88 mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la milenia ambalo tunaweza kulifikia ni elimu ya msingi kwa wote na usawa wa kijinsia katika elimu ya msingi. Hata hivyo ni muhimu kuboresha elimu ya msingi ili wanaoanza shule wamalize kwa sababu elimu wanayopata

ina manufaa. Bila kuiboresha elimu ya msingi tunaweza kurudi nyuma kama ilivyotokea miaka ya themanini kuhusiana na elimu ya *UPE*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la milenia kuhusu vifo nya watoto wadogo ni kuvipunguza kwa theluthi mbili kati ya mwaka 1990 na 2015. Vifo nya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja vimepungua toka 96 kwa watoto 1000 waliozaliwa na kufikia 89 mwaka 2000 na 73 mwaka 2007. Lengo la Milenia ni kupunguza vifo nya watoto wachanga kufikia 32 kwa watoto 1000 ifikapo 2015. Kwa miaka sita (6) iliyobakia, tukiendelea na uzoefu tulionao, lengo hili haliwezi kufikiwa.

Vifo vingi nya watoto wachanga vinatokea kwa watoto wenyewe umri wa chini ya mwezi mmoja. Kila mwaka watoto wanaozaliwa (*newborn*) 51,000 wanafariki kabla ya kufikisha mwezi mmoja. Watoto wengine 43,000 wanazaliwa njiti (*still born*). Vifo nya watoto wa chini ya mwezi mmoja na ni asilimia 29 ya vifo nya watoto wote wa chini ya umri wa miaka 5. Utafiti wa madaktari wa watoto unaonyesha kuwa theluthi mbili (sawa na watoto 34,000) ya vifo nya watoto vinaweza kuepukika ikiwa huduma za msingi za afya zitawafikia kina mama wajawazito na watoto wao. Serikali inabidi iweke mkakati na fedha kuwahudumia kina mama wajawazito na watoto wachanga.

Vifo nya uzazi havijapungua bali vinaongezeka. Kuna vifo nya uzazi 578 katika kila wajawazito 100000 wanapojifungua. Wataalam wa Benki ya Dunia wanakadiria kuwa katika mwaka 2007 kulikuwa na vifo 950 kwa kila kina mama laki moja waliojifungua. Inakadiria kuwa kina mama 13000 wanafariki katika matatizo ya uzazi kila mwaka. Lengo ni kuvipunguza na kufikia angalau vifo 132 katika kila watoto laki moja wanaozaliwa ifikapo mwaka 2015.

Kwa mwenendo unaoonekana katika Uchunguzi wa Bajeti za Kaya 2007 na takwimu za Benki ya Dunia, Tanzania, pamoja na kupata misaada mingi toka nje, haitafikia malengo ya milenia ya kupunguza umaskini na kuboresha huduma za afya.

Sera muhimu za kutekeleza ili kufikia malengo ya milenia ni kuhakikisha kuwepo kwa huduma bora za uzazi kwa kila mama mjamzito. Kuwekeza katika miundombinu hasa maji safi na salama, nishati mbadala ya kisasa, barabara vijijini ili kupunguza kazi za shurubu na muda mrefu unaotumiwa na kinamama kutafuta kuni, kuchota maji na kupeleka watoto kupata huduma za afya.

Utandawazi na ukuaji wa uchumi. Utandawazi umefanya uchumi wa dunia hivi sasa kuwa wazi zaidi na kuingiliana sana katika biashara, uwekezaji, huduma za fedha na teknolojia. Nchi zilizokua kwa kasi ya juu zimefanya hivyo kwa kuingiza maarifa, teknolojia na ujuzi kutoka nchi za nje. Njia moja ya kupata maarifa na teknolojia kutoka nje ni kupitia uwekezaji unaofanywa na makampuni ya nje. Njia nyingine ni kupata elimu, maarifa na teknolojia iliyopo katika nchi zilizoendelea na kuitumia kwa kuzingatia uhalisi na mazingira ya nchi yako.

Uchumi wa dunia unatoa fursa ya soko kubwa kwa nchi zinazoendelea. Kinadharia, Tanzania inaweza kuuza bidhaa zote za viwandani inazozalisha kwa bei ya

soko la dunia. Suala la msingi ni je, kuuza nchi za nje ndiyo njia pekee ya kukuza uchumi au tunaweza kukuza uchumi kwa kutegemea soko la ndani ya nchi?

Mikakati ya kuendeleza uchumi kwa kutumia soko la ndani inaweza kufanikiwa kwa muda mfupi hasa kwa nchi kubwa zenyenye watu wengi. Zaidi ya hapo matatizo ya kutetereka uchumi yanaweza kutokea ikiwa nchi itafungua mipaka yake ghafla kwa bidhaa kutoka nje. Hata hivyo mikakati ya uchumi inayotegemea soko la ndani tu hufikia ukomo wake mapema. Soko la ndani ni dogo mno kuendeleza ukuaji wa uchumi kwa muda mrefu na hautoi fursa ya kujikita na kuboea katika eneo la uzalishaji ambalo nchi ina ushindani au inaweza kujijengea ushindani mkubwa.

Ukuaji wa haraka wa uchumi katika nchi maskini hutegemea upatikanaji wa ajira kwa nguvu kazi ya ziada iliyomo nchini. Kwa kadri uchumi unavyokua ndivyo unavyoajiri nguvukazi ya ziada hasa vijijini iliyoko katika sekta ya kilimo na iliyoko mijini katika sekta isiyo rasmi yenye tija ndogo. Raslimali za nchi hasa nguvu kazi ni lazima ziwe tayari kuhama toka eneo au sekta yenye tija ndogo kwenda kwenye eneo na sekta zenyenye tija kubwa ambazo kwa kawaida huanzishwa mijini ambako ni rahisi kupata watu wengi wenye ujuzi na huduma muhimu kwa viwanda kama vile umeme na maji. Ukuaji wa uchumi huambatana na ukuaji wa miji na nguvu kazi kuhamia mijini. Hata hivyo, ili miji iwe vitovu vya ukuaji endelevu ya uchumi inahitaji miundombinu mizuri.

Sera za kukuza uchumi ni lazima zizingatie kuweko na utulivu katika uchumi mpana kama vile kuepukana na mfumko wa bei, ukosefu wa fedha za kigeni, ulimbikizaji mkubwa wa madeni ya sekta ya umma unaotokana na nakisi katika bajeti ya Serikali na hasara za mashirika ya umma. Vile vile mkakati wa uchumi unapaswa kutoa motisha kwa wajasiriamali, wadogo, wa kati na wakubwa kuwekeza katika sekta mbalimbali kwa kuwahakikishia kuwa wakifanya shughuli zao kwa ufanisi na kufanikiwa kupata faida, faida yao hiyo haitaporwa na vyombo vya dola au majambazi. Vile vile ni muhimu kuwa na mikakati ya hifadhi ya jamii ya kupunguza makali ya maisha kwa watu watakaoathirika na mabadiliko ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtikisiko wa uchumi duniani umeleta changamoto kubwa kuhusu kutegemea utandawazi katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo katika nchi maskini. Je, nchi tajiri zitalinda ajira na viwanda vyao kwa kuweka vikwazo vya biashara? Uchumi wa dunia utaibuka toka mtikisiko huu na kuanza kukua kama ilivyokua kabla ya mtikisiko? Ni wazi Marekani ambayo kwa muda mrefu ilipunguza uwekaji wa akiba na watu wake kutumia kwa kukopa watawajibika kupunguza matumizi na kuongeza akiba. Ukosefu wa ajira utaendelea kuwa mkubwa na kasi ya kukua kwa uchumi itapungua.

Ulaya Magharibi na kanda ya *Euro* inakabiliwa na kuongezeka kwa madeni ya Serikali. Huenda Ulaya ikajikuta inakabiliwa na kutokua kwa uchumi wake. Nchi za Asia, China na India ndizo ambazo zinategemea kuongoza kwa kukua uchumi. Kwa Tanzania kama nchi ndogo tunaweza kukuza uchumi kwa kasi kubwa ikiwa tutajipanga vizuri na kutumia mali ya asili yetu kwa tija kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kubuni sera nzuri ni mwanzo tu. Sera zinapaswa kuwekwa katika mipango ya utekelezaji na kutekelezwa kwa umakini wa hali ya juu. Utekelezaji na matokeo yake yafanyiwe tathmini ya mara kwa mara ili makosa yagunduluiwe na kurekebishwa. Kujenga utumishi bora, wenye ujuzi, usiroyumbishwa na rushwa ndani ya Serikali ni changamoto muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utumishi mzuri ulio imara haujengwi siku moja. Viongozi wa kisiasa ni wepesi kuhujumu kuwepo kwa utendaji mzuri Serikalini ikiwa watawatumia watendaji wa Serikali kufanikisha malengo ya kisiasa ili waendelee kubaki madarakani kwa kuiba kura wakati wa uchaguzi au utekelezaji wa miradi ya muda mfupi kwa malengo ya kuvutia wapiga kura. Serikali inawajibika kuvutia watumishi wenye uwezo na ari ya kufanya kazi. Ni muhimu mishahara ya wafanyakazi Serikalini iwe inavutia lakini utumishi Serikalini uzingatie uwezo na siyo mtoto wa nani au unamjua nani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ya mwaka huu ni moja ya bajeti mbaya katika historia ya nchi yetu. Ni bajeti ambayo itaumiza sekta binafsi inayozalisha mali kwa kuitoza kodi nyingi sana ili kulipia gharama za uendeshaji za Serikali (sio gharama za maendeleo) na wakati huo huo ni bajeti inayoifanya Serikali ishindane na sekta binafsi katika kutafuta mikopo kwenye mabenki ya biashara. Bajeti hii itaumiza ukuaji wa uchumi na kupelekea uzalishaji kupungua na hata kusababisha watu kukosa ajira au kupunguzwa kazini kwa wingi.

Bajeti hii ni bajeti ya kujinyonga kwa chama kinachotawala kwani itaongeza ukali wa maisha kwa wananchi, haijibu changamoto za umma na inasaidia zaidi wenye nacho kuliko watu maskini. Hasira za wananchi hao watazionyesha katika masanduku ya kura mwezi Oktoba mwaka huu na Kambi ya Upinzani inaamini watakuwa na haki ya kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru wote kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Inaitwa hotuba ya kisiasa, ahsante sana na tunashukuru umeweza kutoa hotuba yako mwenyewe mpaka mwisho hakuna hata dalili kama unaumwa kwa jinsi ulivyotoa kwa nguvu sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nawashukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Mwenyekiti wa Kamati walioshughulikia hotuba zile mbili za Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango kwa uchambuzi wao mzuri, nadhani wangepata muda mwingi basi tungekoma lakini ni dakika thelathini tu. Tunashukuru sana.

Kwa hiyo, sasa tunaingia katika kuchangia dakika kumi kila atakayepewa nafasi halafu kwa kuwa kawaida hizi hotuba zinachangiwa na watu wengi, sasa wewe unakuwa hapa katikati unasema unaondoka halafu utataka upewe nafasi siku nyingine, haitawezekana. Sisi tutafuata orodha tu kama haupo basi utakuwa haupo kwenye orodha na kama utajaaliwa basi mwishoni kabisa labda kama kutakuwa na nafasi maana

haitakuwa na maana mtu ameondoka hapa na mwingine amekaa hapa anasubiri anakosa nafasi anapewa yule aliyeondoka na kurudi. Kwa hiyo, tunakwenda kwa kadri tulivyo atakayekuwa hayupo basi ajue hayupo.

Kwa hiyo, wanaoanza kuchangia hapa sasa na kwa dakika tulizonazo ni Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Mtutura Mtutura, nianze na hao kwanza.

Mheshimiwa Athuman Janguo karibu.

MHE. ATHUMAN S. JANGUO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama hapa kufanya kazi hiyo. Napenda kuwashukuru wapiga kura wa Kisarawe kwa imani yao walijonipa kuwa katika Bunge hili kwa muda wa vipindi vitatu mfululizo. Mwaka huu tumeshakubaliana wao na mimi tutachagua Mbunge mpya ili aendeleze yale mazuri tuliyofanikisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii inawasilishwa katika mazingira magumu sana hasa yafuatayo:-

Inawasilishwa baada ya mtikisiko wa uchumi, fedha na hali ya mabadiliko ya hali ya hewa duniani, inawasilishwa huku shilingi yetu ya Tanzania ikiporomoka thamani yake, inawasilishwa wakati tunaingia katika matumizi makubwa ya uchaguzi na vitambulisho vya Taifa, inawasilishwa wakati wahisani wameonyesha dalili ya kupunguza misaada yao kufidia ile ziada waliyoitao mwaka uliopita. Lakini pamoja na hayo yote Serikali inakuja na bajeti ya shilingi trilioni 11,112 bilioni yaani zaidi ya ile ya 2009/2010 kwa 14.2%.

Ukuaji wa uchumi wa 7.1% hadi 8% kutoka viwango vya mwaka uliopita na kupunguza upandaji wa bei kutoka zaidi ya 10% hadi 8%. Kwa malengo haya nadhani Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi na Serikali yote wanastahili kupongezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sifa hizo bajeti ina upungufu na ninapenda kuzungumzia yafuatayo:-

Mapato yetu ya ndani ya trilioni sita (6) hayatoshelezi hata kutimiza matumizi ya kawaida ya trilioni 7.8.

Kama kawaida bajeti zetu, bajeti hii ni ya ulaji, tunakula kila tunachokusanya hatuwekezi, ni 29% ndiyo bajeti ya maendeleo katika bajeti nzima ya shilingi trilioni 11 nilizozisema.

Uwiano wa bajeti ya maendeleo unazidi kushuka dhidi ya matumizi ya kawaida, kwa mfano, mwaka uliopita au bajeti iliyopita, bajeti ya maendeleo ilikuwa ni 29.64% lakini mwaka huu tunalenga kuwa na bajeti ya maendeleo ya 29.14 ya bajeti nzima. Tunazidi kutegemea misaada na mikopo ya nje.

Katika mwaka 2009/2010, katika bajeti yake mikopo hiyo ilikuwa ni 12.5%. Mwaka huu imepanda maradufu kufikia 25.2% ya bajeti nzima. Wakati mwingine tunachokitegemea kukipata kwene mikopo sicho kinachokuja kwani kama tunavyoambiwa katika bajeti hii, katika bajeti iliyopita tayari kulikuwa na upungufu wa 14%. Pamoja na hayo ningependa niipongeze Serikali kwa uamuzi wa kupunguza mikopo yenye masharti ya kibashara kwa matumizi ya kawaida, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza. Bajeti hii inatilia mkazo kauli mbiu ya Kilimo Kwanza kwa kutenda yafuatayo: Moja kuongezeka bajeti ya Kilimo kwa 35.5% zaidi ya mgao wa mwaka tunaoumaliza. Mbili, kuboresha sheria mbalimbali zilizotajwa katika ibara za 59,60 na 61. Misamaha hiyo itawasaidia wakulima hasa wale wadogowadogo. Mheshimiwa Waziri usijali punguzo la shilingi bilioni 2.39 kutokana na hali hii kwani tunapanda mbegu na tutavuna miaka ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la 35% si la kujivunia kwani shilingi bilioni 667 za mwaka uliopita ni sawa na 6.7% ya bajeti nzima na shilingi 903 zilizopangwa kwa bajeti hii ni sawa na 7.8% ya bajeti nzima. Miaka saba tangu Azimio la Maputo bado hatujafikia lengo la 10% tunakwenda wapi? Ni kilimo tu ndicho kitatupeleka haraka katika kupunguza umaskini kama Waziri mwenyewe anavyokiri katika Ibara ya 67 ya taarifa ya hali ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaotoka kwenye maeneo yanayolima korosho tunaliafiki sana pendekezo la Mheshimiwa Waziri la kuongeza ushuru wa korosho zinazouuzwa nje ya nchi. Hili litasaidia sana kuongeza pato la wakulima hasa wale wadogo wadogo na wabanguaji. Vile vile litaongeza ajira kwani korosho ambazo sasa hivi zinasafirishwa nje ya nchi zitakuwa zinabanguliwa hapa nchini na watu wengi watapata ajira. Lakini niishauri Serikali kuwa, sambamba na kuongeza ushuru huo isaidie wakulima na wabanguaji wa korosho kwa kufanya yafuatayo:-

Moja, lile ongezeko la ushuru wa korosho kutoka 10% hadi 15% zile korosho zisizobanguliwa zinazouuzwa nje sasa zipelekwe kwenye mfuko wa kuendeleza zao la korosho ambaa umezinduliwa mwaka huu.

Pili, zao la korosho lihusishwe kwenye misamaha iliyotajwa katika Ibara ya 61. Tatu, ielekeze taasisi za fedha kulegeza masharti ya mikopo kwa wakulima na wabanguaji wa korosho nchini. Nne, iongeze ruzuku kwenye bei za pembejeo za korosho. Kwa kufanya hivyo ninaamini kabisa kwamba, zao la korosho litawenza kuongeza tija na kuongeza mapato ya Serikali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi kupigiwa kengele ya pili. Kwa hiyo, napenda nikushukuru tena na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii kuwa mchangiaji wa pili katika bajeti ambayo ni bajeti ya funga miaka mitano ya uhai wa Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi tu kwa Waziri pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri ya maandalizi ya bajeti hii ambayo ninaisema ni bajeti nzuri ambayo tunakwenda katika kipindi cha uchaguzi tukiwa na uhakika kabisa kwamba yale tuliyotenda katika miaka mitano wananchi wameyaona na ni mwendelezo wa shughuli nzuri za Serikali ya Awamu ya Nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kuweza kusema kwamba na mimi nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya kwa kusimamia na kuweza kufanya utekelezaji wa shughuli za kimaendeleo kwa kuweza kudhibiti na kukusanya kodi ya ndani tangu tulipoingia mwaka 2005, 2006 na 2007. Kumekuwa na nyongeza ambayo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka katika makusanyo ya kodi.

Jambo hili ni jambo jema sana, kutoka trilioni mbili za mwaka wa kwanza hadi kufikiwa trilioni saba si haba, ni kazi nzuri na siku zote Serikali ambazo zinaongozwa na watu makini ni Serikali ambazo zinasimamia ulipaji kodi ya ndani kwa sababu vyanzo vya mapato ambavyo vinatakiwa viendeshe Serikali, ni vyanzo ambavyo vinatokana na kodi ya ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika kwa hayo mema yaliyotendeka, ndio yaliyotendeka ndani ya Jimbo langu la Iramba Magharibi na watu wa Jimbo la Iramba Magharibi wanao uhakika kabisa wanajua tulivyofanya vizuri katika sekta ya elimu, sekta ya maji, sekta ya barabara, sekta ya kilimo na sekta nyingine nyingi kama ambavyo tumezifanya katika awamu hii yote ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo ninao uhakika na kama ambavyo wamekuwa wakiniahidi wapiga kura wangu wana uhakika kwamba, watanirejesha ndani ya Bunge hili ili tuendeleze yale ambayo tumekuwa tukiyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza haya ya awali lakini nitaelezea kwa uchache kabisa namna ya kuishauri tu Serikali ili kuboresha zaidi kule tuendako kwa sababu tunahitaji fedha za kutosha, ili tuweze kufanya vizuri zaidi ya hapa. Tuna uhakika kabisa tumefanya vizuri lakini sasa tunapokwenda katika bajeti hii na zile bajeti zinazokua, nilichokuwa nashauri, bado yapo mapungufu ambayo yanaonekana katika kuchangia pato la Serikali, ambayo ni muhimu sana na hivyo Serikali inatakiwa tuangalie kwa umakini ili tuweze kuboresha hivyo vyanzo ili tuweze kupata zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha kwanza nilikuwa nataka nisemee sekta ya madini. Sekta ya madini ni sekta muhimu sana lakini mchango wake kwa pato la Serikali bado ni mdogo sana. Kwa hiyo, naomba kufuatana na Tume mbalimbali zilizoundwa mpaka hii Tume ya mwisho ya Mark Bomani, naamini tujaribu kufuata yale ambayo waliyapendekeza kwamba ili tuweze kuongeza lile pato tutoke hapa tulipo ili tuweze kuwa na pato ambalo linaweza likachangia pato la Serikali na tukaweza kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nizungumzie kuhusiana na kilimo. Najua Kilimo ndiyo uti wa mgongo na kilimo ndicho ambacho sisi tunategemea kiweze kuchangia sana katika hili pato la Taifa na sasa hivi hata ukiangalia ni asilimia takriban 14 ambazo ndizo zimechangiwa katika pato la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba, bado hatujatoa msukumo wa dhati katika kilimo. Hatujatoa msukumo wa dhati kwa sababu tumeonekana kweli tunasema tunakipa kilimo kwanza na tumekipa majina mazuri, lakini naamini kwamba ule utekelezaji wake bado haujagusa wananchi ili waweze kuzalisha zaidi. Suala ambalo limetolewa naweza kusema nimeona vipaumbele vilivyowekwa na kimetajwa Kilimo kama namba moja, ukurasa wa 37-38.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kutoka kipengele cha kwanza mpaka cha tatu, kimezungumzia vizuri sana namna ambavyo tunaweza tukakiboresha kilimo kuhusiana na pembejeo, kuboresha mfumo wa utoaji wa taarifa ya masoko ya wakulima, kujenga miundombinu ya masoko, kuanzisha na kuongeza shughuli za uongezaji thamani katika mazao ya kilimo, ni mambo mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haya mambo hayafanyiki kwa kiwango kinachotakiwa ili wakulima waweze kuongeza pato zaidi ya hapa ambapo tumefikia. Imeeleza katika kipengele cha pili, kuimarisha huduma za ugani. Ni dhahiri bado tunahitaji huduma ya ugani, hasa huduma hizi za kitaalam, tunahitaji sana kilimo cha kitaalam na hasa katika maeneo ya wakulima, maeneo mbalimbali ambayo moja kwa moja ni ya wakulima tunaomba hizi huduma za ugani, hasa kupata huduma za kitaalam wananchi wapewe utaalim ili waweze kuondokana na kilimo cha kizamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, na pia imeeleza juu ya kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Hii nataka nizungumzie katika mikoa yetu, hii mikoa ya kati, mkoa wa Dodoma, Singida na Shinyanga. Kwa kweli sisi katika mikoa hii ya kati wananchi wanalima sana na wanalima kwa kiwango kikubwa sana. Lakini kilimo chenyewe ni cha kubahatisha zaidi kwa sababu mvua zenyewe zinaponyesha zikiondoka ndiyo kinaishia hapo. Sasa ili waweze kufanya vizuri, naomba Serikali kutilia umuhimu juu ya suala la umwagiliaji, na hii miradi ya umwagiliaji ikamilike ili tuweze kupata hata kilimo cha misimu miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwa sisi watu wa mikoa ya kati kwa sababu tuna wanyamakazi wengi na kama tuna wanyamakazi wengi uwezo wa kujihudumia sisi

wenyewe katika kilimo tuna uwezo mkubwa. Kwa hiyo, tujengewe uwezo kwa kujengewa miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona bado kuna mgogoro kidogo ambao hili nililisema hata mwaka jana, tatizo ninaloliona Wizara hii ya Kilimo kutenganishwa na shughuli za umwagiliaji bado ni tatizo. Bado ni tatizo kwa sababu wanaoshughulika na umwagiliaji ni watu wa maji na wanaotoa shughuli za kitaalam za kilimo ni watu wa kilimo na wanaojuua mahali pa kulima vizuri ni watu wa kilimo. Sasa hapa *coordination* inakuwa ni ngumu sana mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tulikuwa tunaomba Serikali kuangalia upya juu ya suala hili kwa sababu pengine inaleta mkanganyo. Naweza kutoa mfano, katika Jimbo langu tuna eneo ambalo lilikuwa linahitaji umwagiliaji, eneo la Mlandala. Miundombinu ilijengwa, waliojenga ni watu wengine wa idara ya maji, lakini leo wanaosimamia juu ya umwagiliaji ni watu wa kilimo. Watu wa kilimo wanasema sisi tunasubiri miundombinu ikamilike ili tuweze kutoa huduma za utaalam ili watu wawezekulima. Watu wa maji wao wanasema hatujapata fungu la fedha, sasa hii inaleta mkanganyo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali kutilia maanani na hasa iangalie juu ya uwezekano wa kuweza kuhakikisha kwamba kilimo kinapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie bajeti ya Serikali ya mwaka huu unaokuja. Nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta bajeti yenye msimamo hasa tukizingatia kwamba mwaka huu ni wa uchaguzi na vilevile kuzingatia vitambulisho vya Taifa. Kwa kweli, naipongeza Serikali na niseme tu kabisa kwamba, naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kuishauri Serikali kwenye mambo yafuatayo: Kwa sababu huko nyuma Serikali ilikuwa imetoa ahadi ya kutekeleza miradi mbalimbali, kwa hiyo, nashauri Serikali badala ya kuanza na miradi mipyä itekeleze miradi ambayo ilikwishaanza. Tukianza na miradi kwa mfano ya miundombinu, Serikali imeahidi kutengeneza barabara mahali pengi, tukichukua barabara za Kitaifa kumalizia barabara ya Manyoni-Singida, barabara ya Manyoni-Itigi-Tabora kwenda Kigoma, barabara ya Tabora-Sikunge-Mbeya na barabara ya Tabora kwenda Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile barabara ya Shinyanga kupitia mto Sibiti kwenda Arusha na hasa kujenga daraja la mto Sibiti ambalo fedha zilitengwa toka mwaka jana lakini wakachelewa kuanza kwa sababu ya Mkandarasi kuchelewa kupatikana. Niwaambie tu kwamba, daraja lile ni kiungo cha mikoa ya Mara, Shinyanga, Mwanza na nchi jirani na upande wa pili Singida, Dodoma, Arusha na Kilimanjaro na nchi za jirani. Naomba mwaka huu kwa sababu masika yanaanza mapema kule kwetu hiyo kazi ianze mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna barabara za Dodoma-Babati, Dodoma-Iringa. Serikali ipeleke nguvu pale na zile barabara za Milenia kutoka Tunduma-Panda na kuendelea, nashauri sana Serikali kwa sababu ilikwishatoa ahadi itekeleze hizo ahadi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kilimo kwanza. Serikali kwa kweli imekwishaanza kuhimiza kilimo kwanza na wananchi wamekwishakiitikia. Hivi karibuni Waziri Mkuu alifika Iramba Mashariki na alipongeza jinsi watu wa Iramba Mashariki wanavyotumia kila eneo linalofaa kwa kilimo kulima kwa njia zinazotakiwa. Kwa hiyo, tungeomba sana pembejeo zipatikane mapema kwa nchi nzima, zipatikane mapema, zana za kilimo zipatikane mapema, haya matrekta na *power tillers* yapatikane mapema na zile ambazo zina spea ili kuhimiza wananchi wetu wafanye kazi nzuri ya kuzalisha mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba tulipitisha sheria hapa Bungeni ya kuanzisha bodi ya mazao mchanganyiko. Imepita miezi mingi, hiyo bodi sasa imenyamaza na sasa ndiyo msimu wa ununuza wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu ni wakulima wazuri sana wa vitunguu maji, katam, alizeti, ngano na sasa hivi hata Waziri Mkuu alipofika kule tulimweleza sasa hivi wananchi wetu wamevamiwa na walangazi kutoka nchi jirani za Kenya, Rwanda na Burundi. Wanunua kwa bei ambayo isingekubalika, hii bodi ya mazao ingekwishaanza kazi ingetusaidia sana kuwasaidia wananchi wetu ili waweze kupata bei bora. Sasa ningeomba Serikali iniambie imefikia wapi, wananchi wa mikoa ya kati nao wangependa kunufaika kama wenzetu wa korosho na kahawa wanavyonufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Serikali imeanzisha mpango kwamba kila Kata iwe na kituo cha afya na kila kijiji kiwe na zahanati. Nchi nzima wamekwishaanza kufanya hiyo kazi na huko ninakotoka mimi kwa kweli napongeza sana kwa sababu karibu vijiji vyote vimeshajenga zahanati au viko kwenye hatua ya kumalizia. Tunaomba huduma zinazoendana na hiyo zipatikane, vifaa vya hospitali, vifaa vya vituo vya afya na waganga. Sasa hivi nchi nzima tuna upungufu wa waganga kwa hiyo, naomba Serikali itafute njia ya kumaliza tatizo hili na tatizo hili limalizwe na bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye elimu wananchi wetu karibu kila Kata wamejenga sekondari na ninakotoka mimi kata na vijiji wamejenga sekondari lakini sekondari hizo hazijakamilika, hazina maabara, hazina walimu wa kutosha. Kwa hiyo, naomba Serikali ipeleke nguvu kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningezungumzia ni juu ya maisha ya wananchi wetu. Wananchi wetu wameshaona faida ya kukaa kwenye nyumba bora na kuishi maisha ambayo watapata umeme. Lakini sasa hivi bei ya saruji, mabati na vifaa vingine vya ujenzi bado viko juu sana. Sijui Waziri wa Fedha atatuambiaje juu ya hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kutoa masikitiko yangu juu ya utendaji wa miradi ya *TASAF*. Bahati nzuri Kamati yetu ya *LAAC* inatembea nchi nzima. Kwa

kweli maeneo mengi miradi ya *TASAF* haiendi kama inavyotakiwa. Kwenye vitabu wameandika miradi imekamilika lakini ukienda *site* hakuna kitu na kuna maeneo mengine unakuta kabisa hata kuanza haijaanza. Sasa hizi ni fedha ambazo walipa kodi wetu wataumia nazo, watakatwa kwenye mapato yao ili tulipie haya madeni. Ningeomba ufanywe utaratibu Serikali iteue Tume itembelee miradi yote ya *TASAF* kwa kweli mtalia na mtaona jinsi ambavyo wananchi wetu wanahujumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nizungumzie juu ya kodi. Ningeishauri Serikali itafute viwango vingi vya kodi. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hoja hii. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu Mawaziri pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba ku-*declare interest* yangu kwa kutumia kanuni namba 61 kwamba baadhi ya maneno nitakayoyasema yatahusisha shughuli ninazozifanya na hasa sekta ya nyama kwa kuwa nina kiwanda cha nyama. Katika hotuba ya Waziri sehemu ambayo imesamehe ushuru, natoa rai kwa Waziri katika ukurasa wa 51 kwamba kile kifungu (d) kinachozungumzia *compressor* maalum zinazotumika kwenye vifaa vya kupoza maziwa naomba pia inaposema maziwa itaje na nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza hivyo kwa sababu na sasa viwanda vya nyama vimeanza kujengwa nchini na wenzetu Serikali wanajenga Kiwanda pia pale Ruvu. Mapendekezo hayo hayo yahusu pia kifungu namba (f) na (g) cha ukurasa wa 52. Vile vile ukurasa wa 54 kile kifungu kinachozungumzia habari ya bidhaa za maziwa namba (ii) ya ukurasa wa 54 isomeke: “Bidhaa za maziwa na nyama”. Kwa sababu vitu hivyo vilivyotajwa humu ndio vinahitajika pia kwa sekta hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo ningependa kwanza kama nitapata muda wa kukushukuru wewe na Mheshimiwa Spika na viongozi wenzangu wote kwa sababu kama mnnavyojua nimekwishaamua kwamba sikusudii kugombea tena Ubunge. Kwa hiyo, nitatafuta wakati mzuri niweze kuagana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Lakini nitatoa rai, rai yangu ya kwanza ninayoiomba Serikali yetu ni kuwa, Waheshimiwa Wabunge wote tukiongozwa na Rais wetu kwa ule mwito wa mafiga matatu Rais, Mbunge na Diwani, naomba kumpongeza Rais na nyinyi Waheshimiwa Wabunge wote kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba wananchi watakapokuwa wanafikiria kuchagua Wabunge watofautishe kati ya kununua khanga na kuchagua Mbunge. Kubadilisha Mbunge isifananishwe na kubadilisha khanga na kipimo kiwe ni kazi ya ilani mlivyotekeleza sio sura, ni Ilani mliyoitarajia kutekeleza. Naomba nimshukuru rasmi Rais wetu kwamba kwa miaka mitano ya uongozi wake ameweza kusimamia ilani na kujenga Chuo Kikuu ambapo kitakapokamilika kitakuwa cha kwanza katika Afrika, nampongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa chuo hiki sasa kimekwishapewa jina la Dodoma naomba Watanzania tufikirie siku za usoni tunaweza tukachagua mlima mmoja mzuri kule kilikojengwa chuo tuweke sanamu ya Rais kama kumbukumbu katika maisha yake, kwa sababu amefanya kazi nzuri. Kwa mkoa wa Rukwa Waheshimiwa Wabunge tarehe 18 na 19 Rais atakuwa anaweka jiwe la msingi wa kujenga barabara ya lami kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga, kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda, na kutoka Sumbawanga kwenda Kasanga. Natoa shukrani nyingi kwa Serikali kwa niaba ya wananchi wa mkoa wa Rukwa. (*Makofii*)

Baada ya hapo, nataka kutoa rai Katiba yetu inasema Tanzania itakuwa ni Jamhuri ya Muungano na itakuwa ni nchi ya Ujamaa na Kujitegemea. Sasa baada ya miaka 40 naomba jambo hili tusione sifa kupewa misaada wala tusione sisi ni watu wazuri tunapewa misaada. Kwa sababu mtu mzima umeoa, una watoto, miaka 40 kuendelea kupewa chumvi na jirani sio sifa. Kwa hiyo, napendekeza katika kipindi cha miaka mitano hii tutengeneze mkakati maana mipango tunayo na ukisoma hotuba ya Waziri hata namna alivyochambua vipaumbele hata changamoto ni safi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema tusitumie hii sasa kutengeneza mkakati wa nchi kujitegemea. Tuna rasilimali nyingi sana kuliko nchi zinazotupa msaada na wenyewe wataendelea kutusaidia kwa sababu nchi inayosaidia haiwezi kuwa uhuru kamili, kuna mambo yatatuingilia kuyaamua. Tukijitegemea hatuombi msaada, mtu atupe msaada sio kwa sababu lazima tupewe, maana inapokuwa lazima bajeti ipewe msaada ndipo tatizo linapoanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo rai yangu kubwa tujenge misingi na nchi yetu ni tajiri tujenge uchumi wa kujitegemea. Bandari ya Tanga, Dar es Salaam na Mtwara zote zikitengenezwa vizuri zinatosha kuendesha Serikali hii. Fedha ya bandari peke yake vitu vitatu hivyo. Twende kwenye madini sisi sasa dhahabu wanasema kama si wa tatu ni wa nne, gesi rasilimali sisi ni matajiri kuliko wenyе mafuta. Watu wanadhani utajiri ni kuwa na mafuta hapana sisi tuna vyote. Tuna maziwa, mabonde, mito, madini, tuna wanyama pori tunawazidi wenyе mafuta kwa rasilimali. Tuna bahari sasa Mungu atupe nini halafu na watu tunao tena viongozi wetu mna akili nyingi kweli, kilichobaki ni namna gani tunaipanga mipango yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo kosa tunalolifanya vile vile kwamba tukisema maendeleo tunamtazama mtu mmoja anaitwa Rais, suala la kuleta maendeleo ni la kila Mtanzania na nataka niseme bila *apology* kwamba Watanzania wengi hata na viongozi wengi ni wavivu hatufanyi kazi kama nchi zingine. Watu walioendelea wanafanya kazi kuliko sisi ambao hatujaendelea. Ukifika vijijini unakuta watu wanaota juu, mijini watu wamerundikana hawana kazi, wanacheza bao na viongozi tunawaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatujafanya mipango ya kutumia rasilimali na watu wetu hatuwezi kwenda. Hiyo ndiyo rai yangu kubwa. Pigeni kelele mpaka kesho kama nchi hajitegemei ni bure. Sisi tuna sifa ya kulisha majirani wote. Burundi na Rwanda ni kwa reli, mitaji ya kilimo hawawezi kulima kama sisi. Kwa hiyo ninachosema, tuchague maeneo tuyafanyie mikakati na Serikali Kuu isimamie kila mtu

afanye kazi. Kila Waziri aliyepewa Wizara asimamiwe kutekeleza malengo yake. Kila Mkuu wa Mkoa na kila raia na sisi wenyewe kila mtu awe mfano kwa nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo ningesema huo ndio wosia wangu tusipofanya kazi maendeleo ni ndoto. Ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya bajeti, hotuba ya mwisho ya bajeti kwa Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi katika kipindi chake cha miaka mitano toka wameingia madarakani. Toka Serikali hii imeingia madarakani kwa miaka minne iliyopita Bunge limeidhinisha zaidi ya shilingi trilioni 26 kama bajeti, toka mwaka 2006/2007 mpaka mwaka 2009/2010. Leo na mpaka Jumatatu tunajadili na kwa wingi wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi humu kwa vyote vyote vile watapewa hundi nyingine ya shilingi trilioni 11. Kwa hiyo, jumla katika miaka mitano tutakuwa tumewapa jumla ya shilingi trilioni 37 kwa ajili ya kuweza kuleta maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika kipindi cha miaka minne iliyopita jumla ya Watanzania milioni 1.9 wamekuwa maskini zaidi na kuongeza idadi ya watu maskini mpaka kufikia milioni 13. Kwa hiyo, tunapojadili bajeti hii tunazungumza bajeti ambayo tuna Watanzania zaidi ya milioni 13 ambao wanishi chini ya Dola moja kwa siku na bajeti hii hajibju matarajio yao. Bajeti hii haielezi ni jinsi gani Watanzania hawa wataweza kushiriki na kukua na kuondoka katika wimbi la umaskini. Bajeti hii ni *the longest suicide letter* ambayo Chama cha Mapinduzi imejandikia mbele ya wananchi. Kwa sababu ni bajeti ambayo inatoa faida zaidi kwa watu ambao tayari wana uwezo na haielezi changamoto kwa watu ambao ni maskini zaidi ya milioni 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa aliyetoka kuzungumza hivi sasa alizungumza kuhusiana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Mwaka 2005 Chama cha Mapinduzi kiliwaahidi Watanzania kwamba watahakikisha kwenye ilani yao sekta ya kilimo inakua kwa asilimia 20. Kwa mujibu wa MKUKUTA wa kwanza ambao tunaumaliza sasa ilitakiwa sekta ya kilimo ikue kwa asilimia kati ya nane mpaka 10 ili kuweza kuwaondo nusu ya Watanzania kwenye umaskini. Kwa masikitiko makubwa kwa taarifa ya hali ya uchumi ambayo Waziri wa Fedha ameisoma jana sekta ya kilimo likua kwa asilimia 3.2 tu mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano toka Serikali ya Awamu ya Nne iingie madarakani sekta ya kilimo imekua kwa wastani wa asilimia nne peke yake. Mmeshindwa hata kufikia nusu ya malengo yenu ya ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mmeshindwa hata kufikia nusu ya ahadi kwa mujibu wa MKUKUTA. Hii ni aibu kubwa sana na tumewapa jumla ya shilingi trilioni 26 kwa miaka minne iliyopita na mmeshindwa kukuza kilimo angalau kufikia

Mheshimiwa Naibu Spika, faida kama za Dodoma *University* naomba nitoe *challenge*. Kwa Mbunge yoyote wa Chama cha Mapinduzi asimame na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi aonyeshe ni wapi Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imesema itajenga Chuo Kikuu Dodoma? Yeyote mionganoni mwenu asimame

nam-*challenge*, hakuna. Mtu yejote asimame na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi aseme Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi iliahidi *University of Dodoma*, hakuna. Kwa hiyo hamwezi kufaidika na kutaka kujisifu kwa vitu ambavyo wala hamkuwaambia wananchi. UDOM wazo la ujenzi na kugeuza Dodoma kuwa *University City* ni wazo ambalo lilitolewa na CHADEMA toka mwaka 1992. Huo ndio ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha jana ...

KUHUSU UTARATIBU

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 55. Hivi ni utaratibu mzuri kudanganya Watanzania ya kwamba Chama cha Mapinduzi kilisema uongo wakati kuna kifungu kizima kinachoeleza jinsi tutakavyosimamia uimarishaji wa elimu katika ngazi zote. (*Makofi*)

Je, huu kweli ni utaratibu mzuri au tunaanza kupiga siasa ili tupate kura. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mongella. Napenda tu kuwaambia Waheshimiwa Wananchi wote hili Bunge wajue ndio hivyo itakavyokuwa. Maana yake elimu sio Chuo Kikuu ndio itakavyokuwa mazungumzo yenye yatakuwa namna hiyo. Kwa hiyo nafikiri uko sahihi Mheshimiwa Mongella kwamba elimu ndio ina-cover kila kitu, huwezi kuandika nitajenga na shule na kila kijiji. Kwa hiyo ni sahihi ulivyosema. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Makatibu wa-make sure kwamba hizo dakika ambazo zimepotea zimeangaliwa.

NAIBU SPIKA: Utapata.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha ametusomea bajeti ya mapato ya ndani kuongezeka kwa zaidi ya shilingi trilioni moja (*Domestic Revenue*). Tofauti kati ya *Recurrent Budget* peke yake kwa mujibu wa takwimu ambazo amezisoma Waziri wa Fedha zinaonyesha kwamba asilimia 23 ya *Recurrent Budget* ita-finance-wa kutohana na mikopo na misaada kutoka nje. *Recurrent* yaani Mishahara, mafuta jumla ya shilingi trilioni 1.8 ni a *black hole* kwenye *Recurrent Budget*. Huko nyuma tulifikia wakati ambapo (*Domestic Revenue*) au fedha za ndani ziliweza kuendesha matumizi ya kawaida. Sasa hivi tunakwenda katika hali ambayo fedha za ndani hazitoshi kuendesha matumizi ya kawaida. Hii ni hali mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani katika kila shilingi 100 tunaitumia katika matumizi ya kawaida shilingi 23 inabidi twende tukakope, tunakopa kulipa mishahara, tunakopa kulipa posho, tunakopa kununua mafuta ya magari yetu, hii ni nchi ya namna gani? Kama alivyosema Waziri Kivuli wa Fedha na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, bajeti hii ni moja ya bajeti mbaya kuliko zote katika historia ya nchi yetu. Kwa sababu ni bajeti ya

kutumia tumbo, ni bajeti ya chote tunachokikusanya tunakila hatuendelei na bado tunabakia na *gap* ya kwenda kutafuta na kwenda kukopa na misaada kwa ajili ya kula na sio kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa sababu asilimia 65 ya bajeti ya maendeleo bado inategemea wafadhili na ukichukua *recurrent* na *development budget* asilimia 44 ya bajeti yetu na sio 33 kama Waziri alivyosema bajeti bado tunategemea wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali ikubali sio sifa kuwa na bajeti kubwa sana. Kwa sababu bajeti hii inapelekea kwa mfano kodi ambazo zitaongezeka kwa ajili ya kuziba kuongeza mwanya wa makusanyo shilingi bilioni 300 zinatoka *Large Tax Payers Department*. Shilingi bilioni 300 zitatoka *trade taxes* na hali ya uchumi sio nzuri kiasi hicho. Maana yake ni kwamba tunategemea watu wa *import* zaidi ili tuweze kukusanya zaidi. Ni hali ambayo sio nzuri, ni hali ambayo inaweza kuleta matatizo zaidi katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha amezungumza kuhusu kuuzwa kwa hisa za *NBC* na Serikali kupata zaidi ya shilingi bilioni 30. Lakini nimeangalia kitabu namba moja *Revenue Book* hiyo *source of revenue* haimo. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Fedha aweze kutoa ufanuzi kwa nini haimo? Shilingi bilioni 30 za *share* za *NBC* hazimo kwenye *Revenue Book*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu na la mwisho kwa sababu ya muda. Waziri wa Fedha jana alizungumza kurejesha misamaha ya kodi ya mafuta kwa Kampuni za Madini. Madhara ya uamuvi ambao umeufanya ambao ni kwamba tunarudi nyuma ile *goodwill* ambayo tumeitengeneza kwenye Sheria Mpya ya Madini tunaiua. Naelewa kwamba Serikali inaogopa kushtakiwa kwa sababu watu wamesaini zile *MDA*. Lakini kuna meza za kuhakikisha kwamba sekta ya madini inafungamanishwa na sekta nyingine. Ukiruhusu Makampuni ya Madini yaagize mafuta kuzalisha umeme wao bila kulipa kodi maana yake ni kwamba hawatanunua umeme kutoka *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna kazi ambayo imefanyika tayari Wizara ya Nishati na Madini. Migodi yote isipokuwa mmoja sasa unaweza kupata umeme kutoka *TANESCO*. Lakini kwa kuwaruhusu kuagiza mafuta ya kuzalisha umeme wao wenyewe tunaingia kwenye tatizo la fungamanisho kati ya sekta ya madini na sekta ya umeme. Lakini zaidi ya hapo tunawapa nafasi zaidi makampuni ya madini yaache kutumia *local contractors* ili kuhakikisha kwamba sehemu ya fedha na asilimia 25 ya mapato ya makampuni ya madini inatumika kwenye kazi ile ya kuchimba. Kwa hiyo *local contractors* kama wangepata fedha hii tungepanua zaidi uchumi.

Kwa hiyo kuna haja ya kuwa na *measures* maalum ya ku-*mitigate* huo uamuvi ambao Serikali imeufanya na kwa vyovoyote vile si uamuvi sahihi na uamuvi ambao haukufikiriwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda hakuna, siungi bajeti mkono.

NAIBU SPIKA: Ahsante unaweza kuandika mengine. Anayefuata ni Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura.

MHE. MTUTURA ABDALLAH MTUTURA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe shukrani za dhati kwa Serikali yetu ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dr. Kikwete na kwa ngazi ya Serikali ikiwa inaongozwa na Mheshimiwa Pinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007 Juni, katika Bunge lako hili Tukufu niliwhi kuiomba Serikali kwamba waiangalie kwa macho mawili Wilaya ya Tunduru. Leo nafarijika kutamka wazi kwamba ombi langu lile lilikubaliwa na Serikali ikaliangalia Tunduru kwa macho mawili na kwa ujumla mabadiliko makubwa sana yamefanyika katika kipindi hiki cha miaka mitatu. Kwa hiyo kwa niaba ya wanachi wa Tunduru napenda kutoa shukrani za dhati kwa Serikali yote. Mawaziri wote pamoja na Watendaji wote wa Serikali kuu mpaka ngazi ya Serikali ya Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko hayo ninaweza kuyataja machache ingawa ni mengi, kuna maboresho ya ajabu yametokea katika barabara yetu ya kutoka Tunduru hadi Masasi ambayo zamani ulikuwa unasafiri masaa kumi, leo hii unasafiri kwa masaa manne. Suala la pembejeo tumeweza kufupisha na kuwaletea wananchi pembejeo mapema sana, pembejeo za kutosha na za bei ambazo kama ilivyoleezwa kwenye Ilani kwamba inakusudia kuleta pembejeo yenye kumpa tija mkulima. Kwa hiyo bei imeshuka kutoka 36,000/- kwa mfuko wa kilo 25 mpaka shilingi 16,000/- na mwaka huu ni 14,000/. Haya ni mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, suala la bei ya korosho nayo imezidi kuimari, mwaka 2007 korosho ziliuzwa kwa shilingi 340/- mpaka 350 kwa kilo. Hivi ninavyozungumza kwa msimu huu na msimu uliopita korosho zile zimeuzwa shilingi 700/. Hayo ni mabadiliko makubwa na wananchi wameuza korosho zao palepale zilipo badala ya kuzisafirisha kupeleka mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizi kuna tatizo moja ambalo limekuwa sugu sana katika Wilaya ya Tunduru. Suala hili ni wanyama waharibifu, hususan mnyama anayeitwa tembo. Mwaka huu wananchi wa Tunduru hasa baada ya kupata pembejeo za kutosha na za ruzuku, wamelima kiasi cha kutosha sana, lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo bado wanasumbuliwa na wanyama tembo ingawa uzalishaji umekuwa mkubwa lakini unarudishwa nyuma kwa sababu ya tatizo hilo. Kwa hiyo tunaiomba Serikali watusaidie kuwadhibiti hawa wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo njia ambazo tunaweza tukawadhibiti sisi wenyele lakini isije ikawa tukaanzisha mgogoro mpya na Serikali. Sasa ili tusifikie hapo tunaiomba Serikali iwe makini kuhakikisha kwamba mnyama huyu ndovu basi anadhibitiwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 62 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuongeza tozo ya *export levy* kutoka asilimia 10 mpaka asilimia 15. Suala hili tunampongeza sana kwa sababu lina nia njema ya kuimari, viwanda vya ndani vya ubanguaji wa korosho. Sasa katika pato hilo ambalo litapatikana katika tozo hiyo

tunaiomba Serikali angalau asilimia 20 ya fedha zitakazokusanya basi zielekezwe katika mfuko maalum ambao umezinduliwa juzi wa kuanzisha Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho. Mfuko huu ni muhimu kwa sababu utakuwa ni mkombozi mkubwa kwa wakulima wa korosho katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nina imani kwamba uchaguzi huo wa 2010, Mheshimiwa Dr. Kikwete atapita kwa kura nyingi na za kishindo na vilevile nina imani kutokana na utendaji mzuri wa Waziri wetu Mkuu bado atamwona na kama hivyo ndivyo basi namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anifikishie ushauri wangu huu kwa Mheshimiwa Rais. Kama alivyoeleza Dr. Mzindakaya kwamba uchumi wa nchi yetu au pato la Taifa la nchi yetu linaweza likakua maradufu endapo Serikali yetu itahakikisha usafiri wa reli na bandari zetu zinaimarika. Sasa kwa mantiki hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afikishe ushauri huu kwa Mheshimiwa Rais aangalie uwezekano wa kuanzisha Wizara itakayoshughulikia usafiri wa Reli na Bandari. Hiyo Wizara iitwe Wizara ya Maendeleo ya Bandari na Reli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri atakayepewa Wizara hiyo basi dhamana yake kubwa iwe kuhakikisha kwamba miaka hiyo atakayekabidhiwa anajikita kuhakikisha kwamba Bandari zetu na Reli zinafanya kazi kwa kiwango cha hali ya juu ili tuweze *kutape* ule uchumi wa nchi jirani ambazo zinategemea Bandari hizi za Dar es Salaam, Mtwara na ile ya Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi duniani ambazo uchumi wake unategemea bandari peke yake. Sasa sisi licha ya kuwa na bandari lakini vilevile tuna hizi reli mbili. Reli ya Kati na Reli ya TAZARA. Kama Bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga zitaimarishwa na usafiri wa reli ukaimarishwa, *gauge* ikaongezwa upana wake, nina hakika kabisa theluthi mbili ya pato ya Taifa linaweza likatokana na usafiri wa reli pamoa na bandari. Kwa hiyo, ushauri wangu ni huo kuhusu Serikali ijayo ambayo naamini itakuwa ni ya Chama cha Mapinduzi kwa asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, niunge mkono rai ambayo imetolewa na Mheshimiwa Dr. Mzindakaya. Watanzania tusione aibu kujikagua sisi wenyewe. Nakubaliana kwa asilimia 100 kwamba asilimia 98 ya Watanzania hatufanyi kazi kikamilifu. Hili tusione aibu kulieleza. Ni aibu kuona mtu anacheza *pool* saa tatu asubuhi, ni aibu kuona mtu anacheza bao saa nne asubuhi siku ya kazi, ni aibu Mbunge anafika eneo anaambiwa sasa Mheshimiwa Mbunge unatuachaje? Hii ni fedheha kwa nchi kama hii ya kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema msije mkafanya kosa, mnasema mnasubiri Wizara fulani huko mbele ya safari. Kama mlivyoona muda wake ni mfupi kabisa. Hapa na kwa Waziri Mkuu ndiyo wakati wa kujimwaga kwa kitu chochote unachotaka kusema. Kama una jambo lako unataka kusema ombeni. Naona hapa kama kuna watu wanaogopa kuomba wakiamini wataomba kwenye Wizara, utakosa. Naomba ujaze hapa ukipata nafasi utapewa. Ombeni kwenye Wizara hii na ya

Waziri Mkuu, kule kwingine hamtapata. Sasa namwita Mheshimiwa Khadija halafu Mheshimiwa Ahmed, watafuata Mheshimiwa Kaboyonga na Mheshimiwa Mtangi.

MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia nikaweza kusimama hapa mbele ya Bunge lako na kuweza kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu naona Bajeti hii ina tarakimu nyingi ya trilioni 11.1 lakini pesa nyingi zinakwenda kwenye Uchaguzi Mkuu. Kwa hotuba ya Waziri wa Fedha ametudokeza kwamba Wafanyakazi huenda wakaongezewa mishahara lakini ukiangalia kuna vitu ambavyo fedha hizo watakazozipata zitakuwa sawasawa na mchukuzi anachukua maji katika pakacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kuna vitu ambavyo vinamgusa moja kwa moja mfanyakazi kama vile alivyosema Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwamba pikipiki gari ndogo na nyingine nyingine zote zitapandishwa kodi ya leseni pamoja na usajili. Mfanyabiashara hawezi kukubali faida ile apate hasara yeye. Kwa hiyo, moja kwa moja habari hizi zitamkuta mtumiaji wa chini ambaye ni maskini kabisa. Kwa hiyo kile kitu ambacho kimeongezwa na sijui bei gani lakini kinaweza kikatoka kwa upande mwengine. Kwa hiyo, niishauri Serikali kwamba haya mambo ya pikipiki na mambo ya gari ndogo ambazo zinawagusa wananchi wa chini moja kwa moja bora kodi hizi ziondolewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imeangalia sana wakulima pamoja na watu wa mifugo lakini mvuvi haijamgusa kabisa. Mvuvu hivi karibuni tulishuhudia katika vyombo vya habari kwamba anachomewa nyavu zake kwa sababu zile nyavu ni haramu. Kwa hiyo tulitegemea Serikali nayo itamwangalia mtu huyu lakini hatujaona hata sehemu moja ambayo inamlenga mvuvi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali na huyu mvuvi badala ya kumpa sanduku la kwenda kufugia nyuki baada ya kuchomewa zile nyavu zake basi vilevile na yeye aangaliwe katika kupunguziwa mambo ya ushuru au aletewe zile nyavu mbadala ambazo zitaweza kumsaidia ili tuondokane na ule uvuvi haramu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba mara nyingi Serikali inakuja na vitu vya kuongeza mapato, ni vinywaji baridi, pombe na mambo mengine na hivi vinaongeza pato kidogo tu. Lakini kuna pato kubwa ambalo tunalikosa katika bandari. Wenzetu wa Kenya wamejielekeza kabisa katika kuhakikisha wanajenga Bandari ya Uhakika ili iweze kuwaleta maendeleo. Jambo kubwa ambalo linaleta kipato kikubwa ni bandari. Lakini ukiangalia bandari yetu ina miundombinu mibovu, hakuna reli, barabara kiasi tumejitahidi lakini barabara zetu zinatumia mamilioni ya pesa lakini kwa sababu hatujajenga miundombinu ya reli barabara zile zinaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Kibaha mpaka ukifika Chalinze barabara ni mbaya sana imedidimia sana kwa sababu ya kubeba mizigo mizito. Vilevile barabara mpaka unafika Dodoma ina matuta zaidi ya 50 ambayo barabara hii hutumiwa kwa kupita magari makubwa yenye uzito mkubwa ambayo inasababisha kulitia Taifa hasara kubwa kwa sababu kila siku barabara inaharibika na inabidi tujenge tena. Kwa

hiyo naiomba Serikali ielekeze nguvu zake zote kwa kuhakikisha kwamba inatengeneza bandari pamoja na miundombinu yake ili hii mizigo yetu mizito iweze kupita katika njia za reli na kuwafikia walengwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na bandari, bandarini kuna mambo mengi sana pamoja na kwamba watu wanajitahidi lakini kuna meli ambazo zinapakia mizigo ya watu wa nje. Sasa kumezuka mtindo wa wizi uliokithiri. Mara nyingi magari yanapokuja katika bandari yetu tayari ndani ya meli watu wengi wanalamika kwamba vinaibiwa vitu ndani ya meli. Kama vile *control box* ambayo ndiyo inaendesha gari, magari mengi sana yanalala majumbani na watu wengi sana wanalamika lakini Serikali bado haijapanga mikakati. Kwani sisi tumeingia katika soko la pamoja la Afrika Mashariki. Sasa unapokuwa unaiachia nchi, watu wanafanya wanavyotaka, wizi unakithiri ndani ya meli, vitu vinakuja vinaibiwa, tutapunguza mapato makubwa kwa sababu watu hao hawatakubali kuleta mizigo kwa kuitia Bandari ya Dar es Salaam kutokana na wizi uliokithiri na nchi yetu inaingia aibu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba sana Serikali ilisimamie jambo hili ili kama kweli hayo mapato tunayoyataka tuhakikishe kwamba mapato hayo yanapatikana. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijitahidi katika hilo kwani wizi unajulikana kwa sababu bandari imeweka mpango mzuri. Kama meli ikifika wanayo fomu wanaangalia kitu gani kimepungua, inaonekana moja kwa moja meli gani imeleta mizigo ambao una mapungufu. Kwa hiyo, ninachoomba Serikali ihakikishe kwamba inafuatilia suala hili ili nchi yetu isizidi kupoteza wateja ambao tunawahitaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi sana kama ajali za barabarani. Ajali za barabarani pamoja na madereva lakini kuna vyanzo vingine ambavyo vinasababishwa na kukosa *TBS* au viwango vya ubora kwa mabasi yetu. Tumewasamehe ushuru watu wa *DARTS* ambao hata huyo mtoto hajazaliwa maana hata hizo njia hazijajengwa. Lakini tunasahau kama tuna mabasi wanabebe abiria na roho zao zinapotea kila siku kwa chukua *chassis* za malori tukajenga bodi za mabasi na ajali zikitokea hasara kubwa inatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe kwamba inawasaidia na wao kuwapa *exemption* watu wa mabasi kwani wataleta mabasi ambayo yana uhakika. Tunawasamehe ushuru watu wa madini, wageni, tunasamehe ushuru magari ya utalii lakini tunashindwa kuwasamehe Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofî*)

MHE. AHMED ALLY SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika bajeti hii ya mwaka 2010/2011 ya nchi yetu. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu wake na wote waliohusika kuileta bajeti hii. Bajeti hii, kutokana na hali ya nchi yetu, ni nzuri sana na hasa pale inapogusa suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka yote mitano pamoja na Baraza lake lote la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sauti yangu imekauka, hii ni kutokana na kwamba juzi tu nilitoka Jimboni, nafikiri nimeongea kweli kweli mpaka sauti imepungua. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza, naipongeza sana Serikali kwa kuliona suala hili. Mimi binafsi, asilimia kubwa ya wananchi wa Jimbo la Solwa, ni wakulima na moja kati ya kazi kubwa ambazo mimi nitapenda hasa kuzisimamia, ni suala zima la hili la Kilimo Kwanza kwa wananchi wa Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina nia nje na nzuri mno ilivyotenga fedha kwenye mabenki haya ya kutoa mikopo kwa wakulima. Hofu inakuja kwamba, kama wakulima wadogo wadogo hatujawaandaa wala hatujawajulisha wala hatujawaelimisha namna ambavyo wanatakiwa kuwa ili waweze kukidhi masharti ya mikopo hii, mikopo hii yote mikubwa itaenda kwa wakulima wakubwa na wale wenye uzoefu na wanaoweza kuchukua mikopo hii kwenye mabenki haya. Sasa, ile dhana nzima ya Serikali ya kuwasaidia wakulima wadogo wadogo itakuwa imeishia hapa hapa tu kwenye bajeti hii ya mwaka huu. Naiomba Wizara itenye fedha ili iweze; kwanza kabisa, kuwaelimisha wakulima juu ya hati za mashamba yao, hati za dhamana ambazo zinaweza kukidhi masharti haya kupitia hivi vikundi vidogo vidogo vya SACCOS n.k. Tusipofanya hivi, hatutawasaidia wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana sasa hivi katika Jimbo la Solwa, tayari tunazo ofisi za pembejeo katika Kata za Didia, Pandakichiza na sasa hivi tunajenga kwenye Kata ya Salawe ambazo zinaweza kutumika kuwaelimisha wakulima. Hizi *information* zote kwa maana ya kutenga au kuelimisha wakulima, zinaweza zikapitia kwenye ofisi zetu hizi za pembejeo. Wakulima inakuwa ni rahisi mno kuwa na *access* ya kujua namna ya kuchukua mikopo. Mimi binafsi namwomba Waziri wa Fedha anipe maelezo haya. Nitashirikiana naye kuelimisha wakulima wa Jimbo la Solwa na kuwasimamia ili waweze kuelewa dhana nzima ya Kilimo Kwanza iweze kuwanufaisha wakulima wadogo wadogo kama ambavyo Serikali imekusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ndiyo jibu sahihi la kuwawezesha wakulima waweze kunufaika na rasilimali zao. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mzindakaya alivyotuasa hapa kwamba tuwe na uchumi makini na mzuri wa nchi inayoweza kujitegemea. Tunajitegemea namna gani? Viwanda ndiyo jibu sahihi, maana sasa hivi, Mkoa wa Shinyanga kwa mfano au Jimbo la Solwa tuna-*export raw material* tu au malighafi tuseme, tuna pamba, nimeshawahi kuongea sana hapa, asilimia 60 ya pamba ya Tanzania inatoka Mkoa wa Shinyanga, tuna ng'ombe milioni nne lakini Mkoa wa Shinyanga, hatuna kiwanda. Tuna dengu, Tanzania nzima ndiyo tunaongoza, tuna-*export* lakini hatuna viwanda vya dengu. Niombe na kutoa ushauri, Serikali iweze kuchukua *profile* au *advantage* za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano wa Mkoa wetu wa Shinyanga, iweze kuchukua *profile* kwa ajili ya Mkoa wa Shinyanga na Mikoa mingine, ziwekwe kwenye hizi taasisi ambazo ni *contact* baina ya *Investor* na Serikali yetu, kwa maana ya *TIC* na *EPZ*. Hakuna mwekezaji anayeweza akajua umuhimu wa Mkoa wa Shinyanga tusipouza *products* zetu. Kwa maana hiyo, tukiweza kufanya hivyo, tutaweza kupata wawekezaji. Tunahitaji viwanda vya nguo katika Mkoa wa Shinyanga, tunahitaji viwanda vya nyama, tunahitaji viwanda vya dengu, tunahitaji viwanda vya tumbaku, vikiwepo pale vitawenza kununua mazao ya wakulima wanaolima katika Mkoa wetu wa Shinyanga, hata uchumi ndipo utaweza kuona kwamba unakua vizuri kwa kuweza kujitegemea wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Vitongoji, hili ni suala naona kama tunaliruka sana. Nilipokuwa katika ziara yangu katika Jimbo la Solwa, lilijitokeza katika kila Kata niliyotembelea. Wenyeviti wa Serikiali za Vijiji pamoja na Vitongoji wanafanya kazi kubwa sana. Tukiongelea Kilimo Kwanza, ni wao, tukiongelea michango, ni wao, kila kitu ni wao halafu *at the end* Serikali inakuwa haioni umuhimu wa kuboresha maslahi yao. Sasa, nishauri, nadhani kabisa hata kwenye bajeti hii Serikali itakuwa haikuwafikiria, lakini kwa mwaka 2011/2012, naishauri sana Serikali ifikirie maslahi ya Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Vitongoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu katika Mkoa wa Shinyanga ilishuka kwa kiasi kikubwa. Tatizo kubwa kabisa ni Walimu tunaowapata wanaondoka. Wanaweza kuja *intake* ya Walimu 100, wanaondoka 70 au 80, hawafurahishwi na mazingira ya vijijini. Moja katika ushauri ambao ninaipa Serikali, katika bajeti ya mwaka unaokuja, iweze kutenga fedha kubwa mno ili tuweze kuondokana na tatizo la nyumba za Walimu. Nyumba za Walimu ndiyo kivutio kikubwa cha Walimu wanaokuja katika maeneo ambayo yako vijijini. Unamtoa Mwalimu kutoka Singida Mjini au Dar es salaam, unampeleka kijijini kule, amezoea kujirusha, ni suala gumu mno. Anakuja siku ya kwanza, siku ya pili anaondoka zake. Tusipokuwa na mikakati mizuri, tatizo la upungufu wa Walimu na kushuka kwa elimu litakuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari, nawashukuru Wabunge wote, kila anayechangia anaongelea suala la Bandari. Kenya sasa hivi wanajenga Bandari pale Malindi na lengo lake ni kwamba iweze ...

(*Hapa kengele ililia kuashiri kwisha kwa muda wa mchangiaji*)

MHE. AHMED ALLY SALUM: Nimemaliza?

NAIBU SPIKA: Ndio Mheshimiwa.

MHE. AHMED ALLY SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.
(*Makofi*)

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada hii muhimu. Nami kama ada, nianze kwa kuwashukuru

wananchi wa Jimbo langu la Tabora, kwa ushirikiano mzuri tuliokuwa nao katika miaka mitano ambayo ndiyo tunaimalizia. Katika kipindi hiki, tumefanya mengi ikiwa ni pamoja na kufika mahali ambapo sasa Serikali inaanzisha ujenzi wa barabara ya lami kutoka Nzega kwenda Tabora, kutoka Tabora kwenda Kigoma, tunajenga kiwanja cha ndege kwa lami, tunakarabati bwawa la Igombe na pampu mpya za kusukuma maji katika Mji wa Tabora. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali yetu na katika kipindi kinachofuata, kazi yetu kubwa ni kuweza kuyaendeleza mafanikio haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mada iliyio mbele yetu, mimi ni mmoja wa Wanakamati wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Kwa hiyo, mawazo mengi ambayo yako katika hotuba iliyosomwa asubuhi hii na Mheshimiwa Dkt. Kigoda, yamesheheni vile vile na mawazo yangu. Kwa hiyo, nitatumia fursa hii kuongezea tu hapa na pale katika maeneo ambayo naona ni muhimu. Nianze na mahali ambapo Mheshimiwa Salim ameachia, eneo la Bandari na matumizi mazuri ya uchumi wa Kijiografia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ni tajiri, nadhani sisi wenyewe hatujaweza kuojipanga vizuri kutumia utajiri tuliopewa na Mwenyzi Mungu. Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, zikitumika vizuri, zitainua uchumi huu tena kwa haraka sana. Tatizo tulilonalo hapa ambalo nataka kulisisitiza ni miundombinu yetu hususan reli zote mbili (ya TAZARA na ya Kati). Reli ya TAZARA, ni muhimu sana kwa uchumi wa Tanzania hata bila kwenda Zambia, sisi wenyewe tu hapa ndani ya Tanzania, reli ile ni muhimu sana. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuhakikisha inafanya kazi. Reli ya Kati, habari yake ndiyo hiyo kwamba tuna nchi zaidi ya sita ambazo zinatutegemea. Tatizo letu, Shirika letu la Reli ni gongwa, tena linaumwa sana, liko kwenye kitengo cha wagonjwa mahututi. Kuna haja ya Serikali kuhakikisha kwamba Shirika hili linapona haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazungumzo yanayoendelea baina ya Serikali na kampuni ya *Rites* ya India yamalizwe haraka. Lakini, yakishamalizika, hapo ndiyo mwanzo sasa wa uwekezaji mkubwa ambao Serikali inahitajika ifanye. Kwa hiyo, matarajio yangu ni kwamba bajeti hii itakuwa imetenga tengo ambalo litajibu matatizo ya Shirika la Reli kwa haraka. Yako ya muda mfupi na ya muda mrefu. Matatizo ya muda mfupi ni kwamba, Shirika lile halina injini zinazofanya kazi, mabehewa yake mabovu, sehemu fulani fulani za reli ni mbovu na ndiyo maana mpaka leo baada ya ile sehemu ya Kilosa kuja mpaka Dodoma kutengenezwa, bado safari hazijaanza kwa sababu shirika halina uwezo wa kununua hata mafuta. Pia vipuri vya mabehewa na injini, ni muhimu, kwa hiyo, Serikali itenye fedha zitakazoweza kujibu tatizo hili haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii haiwezi kuendelea bila kuwa na viwanda. Baadhi ya viwanda vyetu tunaviu wenye kwa sera zetu za kodi. Viwanda vya *cement* ambavyo vinatumia malighafi ya nchi hii, sasa hivi viko hatarini kuanza kupunguza shughuli zake kwa sababu vinashindanishwa na *cement* inayotoka Egypt na Pakistan. Egypt na Pakistan wanatoa ruzuku kwa viwanda vyao ili viweze kuuza *cement* kwa bei rahisi. Kwa hiyo, sasa sisi Tanzania tunachukua ile ya Egypt na Pakistan kwa gharama ya *cement* inayotengenezwa na viwanda vyetu. Viwanda vyetu vimefanya upanuzi mkubwa, viko tayari kuzalisha *cement* ya kutosha katika nchi yetu, lakini Sera zetu za Kodi kwa

ajili ya kuruhusu *cement* rahisi kutoka nje, tutaua viwanda vyetu. Kwa sababu hiyo, ndio maana haishangazi kwamba hata katika mfumo wa mapato ya Serikali, mapato ya Serikali kutokana na viwanda vyetu nchini ni madogo kwa sababu sisi wenyewe hatuviendezevi viwanda vyetu. Kwa hiyo, tuna haja ya kuhakikisha viwanda vyetu vinafanya kazi na tunavilinda. Kwanza, kwa sababu ya kupata kodi, pili, kwa sababu ya ajira na tatu, kwa sababu viwanda hivi vinatumia malighafi yetu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadithi ni hiyo hiyo kwa viwanda vya magunia. Tunahimiza kilimo cha mkonge, tunahimiza kilimo cha pamba, bila kuwa na viwanda vya kusokota pamba pamoja na mkonge ili kutoa bidhaa ambazo zinatokana na mazao haya ya kilimo, shabaha yetu ya kukuza kilimo kwa maana ya Kilimo Kwanza itakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika pengo la bajeti ya Serikali baina ya mapato ya ndani na matumizi ya kawaida ambayo ni shilingi trilioni 1.8, Serikali inapanga kukopa ndani na nje. Maelezo marefu yametolewa kwenye hotuba aliyosomwa na Kiongozi wangu, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, lakini, mimi nataka nisisitize tu kwamba, kwa kutumia njia ya kukopa ndani pamoja na lile tatizo la kuifanya *private sector* isiweze kupata mikopo kama ambavyo ingeweza kupata kwa sababu Serikali ndio itakuwa mkopaji mkubwa. Tunazungumzia Serikali kukopa si chini ya shilingi trilioni mbili kutoka ndani. Tatizo lingine litakalotokea kutokana na hiyo hali ya Serikali kukopa ndani ni pamoja na *rates* kwa maana ya *interest rates* zitapanda, sasa, *interest rates* zikipanda, ule mzigo wa Deni la Taifa utazidi kuongezeka. Kwa hiyo, hapo ndipo tunapotoa tahadhari kwamba njia hii ya kukopa ndani ina matatizo hayo, unafanya *private sector* yako isiweze kukopa na riba zitapanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la maeneo mengine ambayo nchi hii ikiwekeza nguvu zake, inaweza vile vile ikachangia katika ukuzaji wa uchumi wetu. Eneo hili moja ni mradi wa *Soda Ash* kule *Lake Natron*. Magadi ni nyenzo muhimu katika viwanda. Sasa hivi nchi hii inatumia magadi katika viwanda vyake kutoka nje na moja ya sehemu tunayoagiza magadi ni kutoka Kenya. Kule Kenya vile vile kuna Flamingo, lakini kwa nini Kenya wanavuna magadi yao, sisi Tanzania hatuyavuni eti kwa sababu ya Flamingo? Hebu tuangalie namna gani tunaweza tukawafanya Flamingo hawa wakaendelea kuishi na sisi kama Taifa tukaendelea kufaidika na rasilimali hii muhimu ya magadi kutoka *Lake Natron*, tukifanya hivyo, uchumi wetu jamani, utakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la Kilimo Kwanza, katika mipango ya Serikali, kuna Mfuko unaitwa Mfuko wa Mikopo ya Pembejeo za Kilimo. Mfuko huu una uzoefu wa kuwakopesha wakulima, lakini haupewi fedha za kutosha. Hivi tunavyozungumza, kuna tengo la kama shilingi bilioni 3.2 hivi, ndizo ambazo zimebekwa. Mfuko una uzoefu na una maombi yasiyopungua shilingi bilioni 10. Ninaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza tengo kwa ajili ya Mfuko huu wa Pembejeo za Kilimo ili uweze kukidhi mahitaji ya wakulima ambayo tayari yamekwishathminiwa, tatizo ni uwezo wa kukopesha kwa sababu Serikali haijaweka tengo la kutosha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mdogo, nirudi sasa kwa haraka haraka kuzungumzia eneo tunalosema kwamba, Serikali yetu badala ya kutegemea vyanzo vya wahisani wale wa kawaida, hebu tuanze kama ambavyo tumekwishaanza kwenye Reli ya TAZARA, twendeni na India. Mimi nafahamu kwamba Serikali ya India ilikuwa tayari kuikopesha Serikali ya Tanzania kiasi kisichopungua Dola milioni 83 kwa ajili ya kufufua shughuli ya Shirika la Reli. Lakini tumekuwa tunajivuta kuzungumza na India, hivi India wana matatizo gani na Tanzania? Mimi sina sababu yoyote ya kuipendelea India isipokuwa naifahamu India kama moja ya *emerging markets*, ni nchi ambayo uchumi wake umekwenda mbali sana kiteknolojia na kiuwezo. Serikali ya India iko tayari kuikopesha Serikali ya Tanzania Dola 83 milioni, tuna tatizo gani kuzungumza na Serikali ya India? Huu mkopo utakuja kwa masharti nafuu. Yale yale ya *IDA* (*International Development Agency*), sasa tuna tatizo gani? Kwa sababu ni India? Mbona China tumekwenda? Nasisitiza na naiomba Serikali kwamba hebu zungumzeni na India kama mlivyozungumza nao wakatupa mkopo kwa ajili ya pembejeo za kilimo (matrekta).

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, naomba niipongeze Serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuweza kutuvusha katika dharuba mbalimbali zikiwemo zile za kuyumba kwa uchumi Duniani. Sisi tunaozungukazunguka Duniani, kama tusingekuwa na Serikali mahiri, tungepata matatizo makubwa zaidi kuliko yale ambayo tunayaona sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitoe nafasi ya kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika maeneo tunakotoka. Kwa mfano, katika Wilaya ya Ukerewe, sasa hivi kwa kushirikiana na Serikali na wananchi wa Wilaya ile, tumekuwa na mafanikio yafuatayo:- Shule za sekondari, tumetoka kuwa na sekondari mbili mpaka 20, tuna barabara za kuaminika, kupitika na kufikika katika Wilaya nzima, tuna umeme ambaeo umefika mpaka vijijini, tuna usafiri wa uhakika kati ya Kisiwa cha Ukerewe na Kisiwa cha Ukara na sasa hivi tunategemea Panton mpya itakayokuwa inatuvusha na kutuunganisha na Mkoa wa Mara kupitia Lugezi mpaka Kisolya. Ni matumaini yangu kwamba tunavyoendelea, tukienda kwa kasi hii na baada ya kuichagua tena Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Wilaya hii itakuwa ni Wilaya ya mfano na hasa ukizingatia kwamba na mimi nitaweka jina langu ili niendelee kusukuma maendeleo hayo nikishirikiana na Serikali yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niwashukuru wananchi wa Wilaya ya Ukerewe, walionipa imani na tukafanya nao kazi kwa pamoja. Nataka nianzie hapo hapo kwa kusema kwamba, katika kuijenga nchi yetu hii ya Tanzania, utaratibu wa uongozi tumeuweka vizuri sana. Tuna Serikali Kuu, tuna Serikali za Mitaa, tuna Serikali za Vijiji na mimi leo ninataka nisemee Serikali za Vijiji. Serikali za Vijiji lazima ziwe na mapato ili ziweze kuitwa Serikali na viongozi wake waweze kuwa wanalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Vitongoji, Wenyeviti wa Vijiji wanafanya kazi kubwa sana za kuleta maendeleo, ndiyo wanaosimamia hizi shule za Sekondari zijengwe, ndiyo wanaosimamia Zahanati zijengwe, ndiyo wanaofanya maendeleo yote tunayoyaona na kujivunia, yote yanatokana na hawa Wenyeviti wa Vijiji. Pale unapukuta Mwenyekiti wa Kijiji ni mtu hodari na shupavu, utakuta barabara zimetengenezwa vizuri, shule zimejengwa, inategemeana na uongozi wa kijiji hasa Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa wanatumia muda mwingi sana katika kusimamia maendeleo na katika kujitolea. Wakati umefika, tupunguze popote tutakapopunguza lakini tupeleke kuwasaidia hawa wananchi angalau hata *honorarium* kama tulivyofanya kwa Walimu wa Elimu ya Watu Wazima wakati tuna mkakati wa kufuta ujinga wa kutojua kusoma na kuandika, mbona tuliwalipa na wakati ule tulikuwa na pesa kidogo, tusiwalipe mishahara, tuwalipe *honorarium*, Mwenyekiti akipewa hata shilingi 30,000 kwa mwezi anaweza angalau akanunua sabuni ya kufulia nguo zake. Kwa hiyo, mimi nataka niseme bila kigugumizi kuwa wakati umefika tusione aibu, watu wanataka kugoma wakati wana mishahara mikubwa sembuse hawa amba o hawana kitu na bado wanasmamia mambo yote tutakayoyaamua hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiishawasaidia angalau kuwapa *honorarium* ya utambuzi, watu hawa hawatauza ardhi ovyo vijijini. Watu hawa watasmamia kutokuwepo kwa rushwa katika maeneo yao ya vijijini, watu hawa watafanya maajabu na mageuzi, watasmamia Kilimo Kwanza, watasmamia kila kitu na tutapiga hatua. Kwa hiyo, katika bajeti hii, nasema tuitizame, tuone ni wapi tunaweza tukawekeza katika watu hawa amba o ndiyo msingi mkubwa. Ukichukua Mwenyekiti wa Kitongoji, mtu akgombana na mke wake, kwa Mwenyekiti wa Kitongoji, ameibiwa ng'ombe, kwa Mwenyekiti wa Kitongoji, shamba lake limechukuliwa, kwa Mwenyekiti wa Kitongoji, hana utambuzi wa aina yoyote kwa muda wake wa usiku na mchana anaotumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninapenda niongeze kitu kimoja, bajeti hii inatupa taabu mpaka inafika mahali kuonyeshana vidole kama vile kuna mchawi ambaye hataki maendeleo. Mimi nitaona ajabu uwe na Serikali isiyotaka maendeleo, itakuwa ni ajabu sana, tatizo kilichopo ni kidogo mno kwa hiyo, tuko katika kusema tugawe tupeleke wapi. Mimi ninadhani suala kubwa, ifike mahali tuzungumzie namna ya kuongeza hicho kidogo ili kiwe kiasi kinachowezu kugawika. Sisi akina mama tuna uzoefu, unakuta akina mama hasa wasiofanya kazi, akiamka asubuhi anapewa shilingi 5,000 akiomba jamani hizi hazitosh, mume anasema hapana hizi ndizo nilizo nazo, usiniombe tena lakini akina mama hawa ni wabunifu wa hali ya juu, atajua kwamba nichukue ka-mkaa kidogo, nichukue mchicha nichanganye na dagaa lakini ikifika mwisho wa siku wanawe wamekula na wanalala usingizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachohitaji hasa katika ngazi za Wilaya kwenye Halmashauri zetu, ni kupata Watendaji amba o ni wabunifu. Ma-*DED* wetu siyo wabunifu, wako pale tu kusimamia zile pesa ama kuzigawanya zile pesa zinazokuja lakini ubunifu ya *DED*, Afisa Mipango na wengine, wamekaa wakafanya ubunifu

kwamba Wilaya hii ina *potential* sasa tufanye kila kinachowezekana tuweze kuongeza pato, mimi kwa kweli ninasema tukitaka kufanikiwa ni lazima tuhakikishe kuwa hii kada inayokaa Wilayani ni ya watu wabunifu, siyo wasomi tu unaweza kuwa msomi na siyo mbunifu. Hayo mawili hayaendi pamoja kila wakati, kisomo kinakusaidia kuwa mbunifu lakini siyo lazima kama hukuumbwa na kipaji cha ubunifu ukaweza kuwa mbunifu na wakati mwingine wao ndiyo wanakuwa kikwazo cha ubunifu wa wananchi walioko kule vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninapenda niseme tunapajaribu kutatua tatizo hili la watu kuondokana na umaskini lazima kada iliyoko katika Halmashauri zetu wawe ni wabunifu, wawe wanatatu matatizo ya wananchi badala ya kuongeza matatizo ya wananchi, wawe ni watu ambao watasimamia pesa za Serikali ili angalau hicho kinachoingia katika Wilaya zetu kiweze kuwa ni cha manufaa. Ukichukua kitabu kile cha Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, utakuta kuna pesa ambazo tunapata hapa Bungeni zingetumika kwa usahihi huko katika maeneo zinakokwenda, tungeweza kupata matokeo makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimalizie kwa maombi ambayo yanaweza kutufikisha katika hatari kubwa, kiwanja cha ndege Mwanza ndugu zangu ni hatari kubwa na kinahudumia Mikoa ya Kaskazini na hakihudumii tu wale watu wa Mikoa hiyo, kuna watu na nyie mnakuja ambao hamtoki Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na wapi mnapita katika kiwanja hicho, hebu tafadhalini sana kiwanja cha Mwanza, mmesikia wananchi wa Ukerewe wamepata ajali zaidi ya mara mbili na meli Mv Clarius. Kuna wakati Mv Clarius ilitoboka, bahati nzuri wakakimbia haraka wakarudi Nansio. Mv Butiama imesimama majini mara mbili inapigwa wimbi kwa sababu ni meli za zamani toka mwaka 1980, mwaka 1970, ndiyo unaweka watu 200, 300 tumepeata fundisho lile la Mv Bukoba mnataka tena tupate fundisho lingine la kuua watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.
(*Makofisi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Herbert Mtangi, nadhani atakuwa msemajji wetu wa mwisho mchana huu.

MHE. HERBERT J. MTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii muhimu kwa Taifa letu. Kwa sababu muda ni mfupi, nitazungumza kwa kifupi sana lakini yapo mambo makubwa muhimu sana ambayo sisi Tanzania kama nchi lazima tuyatambue, tunapozungumzia nguzo za kukuza Uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguzo kubwa za kukuza Uchumi wetu ni kama zifuatazo, kwa uchache, ziko nyingi lakini nitataja hizi tano. Kwanza, ni ufanisi wa Bandari zetu. Tukiwa na Bandari zenyе kufanya kazi, kwa ufanisi na Bandari za kutosha, zitasaidia kukuza uchumi wa Tanzania. Pili, ni reli kwa sababu Bandari itakapokuwa inafanya kazi kwa ufanisi lakini hakuna uwezo wa kusogea mizigo inayoletwa katika Bandari kuipeleka katika maeneo yaliyokusudiwa au katika nchi jirani kwa gharama

nafuu, nguzo yetu ya uchumi hii itakuwa haitusaidii. Kwa hiyo, lazima tufanye jitihada ili Bandari zetu zifanye kazi kwa ufanisi lakini lazima tuimarishe reli ili iweze kuchukua mizigo bandarini kupeleka inapokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu, ni barabara, haiwezekani mizigo yote ikachukuliwa na reli lakini barabara lazima ifanye kazi vizuri na tuwe na barabara za kutosha za Kitaifa, za Mkoa, za Vijiji, mpaka kwenye ngazi ya vitongoji, zitasaidia sana kukuza uchumi wa Taifa letu. Nne, ni Madini, kwa sababu Tanzania tuna bahati ya kuwa na Madini mengi sana basi sekta hii ya Madini ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa Tanzania, tunafanya nini ili kutumika sekta hii ya Madini katika kukuza uchumi wetu, ni maswali ambayo lazima tujiulize na eneo la tano ambalo ni muhimu, ni utalii, katika nchi kama Tanzania ambayo tuna vivutio vingi sana vya utalii, lazima tuhakikishe kuwa tunatumia vivutio vyote vya utalii katika sekta ya utalii ili kusaidia kukuza uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, hebu tuangalie nini maandalizi yetu kama Taifa katika maeneo hayo matano niliyoyataja, tunaelekeza nguvu zetu katika kuboresha maeneo hayo ili kweli tuweze kuhakikisha kuwa tunakuza uchumi wa Tanzania? Tukienda kwenye Bandari bado hatujafanya ya kutosha, tunazungumza siku zote habari ya Bandari ya Dar es Salaam lakini yale tunayoyafanya, hayatoshelezi, hivyo ufanisi wa Bandari, kitega uchumi ambacho tunakitazamia sana, kinatuangusha na kinadidimiza uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Mtwara ina kina kirefu hatujaitumia na ina – *connection* nzuri sana ya kuhudumia nchi za Kusini mwa Tanzania lakini hatujaitumia. Bandari ya Tanga iliyopo sasa, kina chake ni kifupi lakini ina eneo zuri sana la kina kirefu, hatujaitumia, kila siku tunasema tutaimarisha Bandari ya Tanga, ni nini hatua zinazochukuliwa kuimarisha Bandari ya Tanga, hatuzioni na nikitzama katika vitabu hivi, hata Wizara ya Miundombinu pia nimejaribu kutazama sioni kama tumeweka nguvu za kutosha kuhakikisha Bandari ya Tanga inajengwa kama tunavyokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pale Dar es Salaam tumeshatoa ushauri mara nyingi kwamba eneo ni ndogo, ukienda pale ,kwa siku moja, mimi nimeshakwenda, utakuta zaidi ya magari 2000 yako pale. Magari ukiyaweka kama *unit*, yanachukua sehemu kubwa sana ya sehemu ya Bandari lakini tukashauri pajengwe angalau sehemu ya juu ili hayo magari yapaki kwa juu, yatoe nafasi, chini *container* ziweze kuwekwa, je, hilo limechukuliwa hatua? Kwa muda wa miaka mingi tunasema hivyo lakini bado halijachukuliwa hatua, bila kusaidia hilo, ufanisi wa Bandari utaendelea kushuka kwa sababu bidhaa zitakuwa zinasongamana na nafasi itakuwa hakuna. Kwa hiyo, tujitahidi, wenzetu wa Rwanda, Burundi na Demokrasia ya Congo wanahitaji sana Bandari ya Dar es Saalam kuliko Bandari zozote Mashariki lakini wanalazimika kwenda Mombasa kwa sababu wafanye nini sasa kama makontena yao yatakan Bandarini kwa muda mrefu bila kusafirishwa, kama barabara zetu hazitoshelezi, kama reli haifanyi kazi, wanaondoka wanakwenda Mombasa na sisi Watanzania tunaangalia hivi hivi Rwanda, Burundi, Demokrasia ya Congo wanahama Bandari ya Dar es Salaam wanakwenda Mombasa, tunategemea nini Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, unaposema ufufue na ujenge upya Bandari ya Tanga lazima uhakikishe vilevile reli ya kutoka Tanga kuititia Muheza kwenda Arusha hadi kutokea Musoma imejengwa. Wenzetu wa Uganda walikuwa wako tayari kutoa fedha, Watanzania wenyewe ambapo sehemu kubwa ya reli inapita katika nchi yetu, hatukuwa tayari kusaidia na hivyo Waganda wamesita na leo Waganda wanatumia Bandari ya Mombasa zaidi kuliko ambavyo wangeweza kutumika Bandari ya Tanga na Bandari ya Dar es Salaamu. Kwa hiyo, tusipofanya jitihada ya kuondoa hali hii basi matarajio yetu kwamba uchumi utakua kwa kiasi kikubwa ni ndoto na ndiyo maana utaona katika kipindi chote hiki ukuaji hauzidi ya asilimia mbili ni 0.2 tu ndiyo uchumi gani unaotakiwa kukua hivi? Kumbe tungetumia *facilities* hizi, nina uhakika kiwango cha ukuaji wa uchumi kingeongezeka kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara, mimi nimewahi kukutana na Wataalamu, rafiki zangu wako Marekani, wametushauri kutumika aina fulani ya utengenezaji wa barabara kwa kutumia lami nyepesi, lami nyepesi itatuondoa katika gharama kubwa sana ambazo tunazitumia katika kuzijenga barabara za Mikoa kwa kiwango cha changarawe na kiwango cha vumbi, kila mwaka barabara hizo zinatengenezwa, hivyo ukichukua mkusanyiko wa utengenezaji wa gharama hizo za barabara kwa mfano kwa miaka mitano tu utakuta kwamba pengine nusu ya barabara hiyo tumekwishaitengeneza kwa kiwango cha lami, lakini kama tutatumia teknolojia hii ya lami nyepesi kwa kipindi cha gharama ya miaka hiyo mitano, tungekuwa tumetumia zaidi ya asilimia 75% ya urefu wa barabara kwa kuweka lami nyepesi kwa gharama ambazo tunatumia kila mwaka kwa barabara za changarawe ambazo hazitusaidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu wa Marekani wamekubali kuja Tanzania, nimewaelekeza wameshakubali, wameshakutana na watu wa *TANROADS*, wako katika majadiliano, wanafanya *soil analysis* katika sehemu za barabara, wako tayari kuisaidia Tanzania. Katika nchi zote za Afrika ya Mashariki na Kati, ndugu zangu hao wameichagua Tanzania kuja kufanya majoribio na wanafanya majoribio hayo kwa gharama zao wao wenyewe na nina uhakika barabara ile ya Muheza kwenda Amani itakuwa sehemu ya majoribio ya wenzetu Wamarekani hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii, ni sekta kubwa sana lakini bado hatujaitumia vizuri. Ninaomba Wizara inayohusika iende chini itizame vigezo na maeneo yote yaliyokuwa muhimu zamani yafufuliwe, hayo ndiyo maeneo makubwa ya vivutio vyta utalii. Turekebishe Sheria zetu za Utalii, tufanye kila kinachowezekana kuutangaza utalii na nina uhakika Tanzania bado ni *potential* kwa utalii. Kule Muheza tuna maeneo makubwa, tuna vipepeo ambavyo havijaonekana maeneo yoyote Duniani, viko Muheza, watalii wanataka kuja kuviona, hatuweki mifumo yetu vizuri, hatutangazi vizuri, kwa hiyo, watu wengi hawajui.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kubwa huku kwenye sekta ya madini, ukitazama haya marekebisho ambayo tumepewa hapa, tulikuwa tunadhani Sheria ile mpya ya Madini itatusaidia sana lakini nikitafakari haya marekebisho, naanza kupata hofu kwa sababu sehemu kubwa ya madini imekwishachukuliwa na wawekezaji, lakini

wawekezaji hawa katika Sheria zilizopita tumewapa msamaha mkubwa kupita kiasi kwenye mafuta na kwenye vitu vingi sana je, itatusaidia hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, muda nimesema ni mdogo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa michango yenu mizuri sasa, tukirudi mchana atakuwepo Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mrope, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama na wengine kwa sababu tutakuwa na wachangiaji kama 16. Kama nilivyosema awali, wale ambao wana wasiwasi, naomba ombeni nafasi ya kuchangia, kama mkiangalia ile ratiba yetu, tutakapofika kwenye Wizara, itakuwa ngumu sana kupata nafasi. Itakuwa ni ngumu kupata nafasi kama Waziri akisoma asubuhi, mtachangia watu wangapi tu, anaingia kujibu hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombeni hapa kuna nafasi halafu na kwa Waziri Mkuu tutakapofika, mtaomba nafasi, msiogope maana Wizara hizi unaongea yote yale unayotaka kuongea na ndiyo maana Mawaziri wapo hapa kwa sababu itabidi wazingatie yale uliyoongea hata kama umeongea kwa Wizara wa Fedha ama kwa Waziri Mkuu, mtapoteza muda kwa sababu kufuatana na hesabu zangu kesho asubuhi tutakuwa na watu na jioni watapungua sana, Jumatatu tunamuachia Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, sina matangazo mengine, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka hapo saa kumi na moja jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

HOJA ZA SERIKALI

(*Majadiliano yanaendelea*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naambiwa saa hizi South Africa ndiyo kuna uzinduzi wa mpira, sasa ninyi ndiyo labda mpira haupo kwenye damu, lakini kwa sababu siyo kipindi cha maamuzi, tunaweza kuendelea na waliopo, hofu yetu ni kwamba walioomba kuchangia kama hawapo ndiyo itakuwa tatizo. Namwita Mheshimwia Esther Nyawazwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mrope, Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Ali Khamis Seif ajiandae.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kusimama tena ndani ya Bunge lako Tukufu baada ya miaka mitano na kwa kazi nzuri tulioifanya ikiongozwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kusimamia amani na utulivu hatimaye leo tunazungumzia bajeti ya 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, imenisikitisha kidogo asubuhi kwa baadhi ya wachangiaji, anasimama na kuhoji na kusema hakuna kitu chochote ambacho

kimefanyika katika Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ninaomba sana, kama kweli wewe ni Mtanzania, tuwe tunazungumza vitu vya ukweli, hivi leo utasema Mkoa kwa Mkoa hatukuunganishwa kwa lami, utazungumza hilo mbele ya wananchi wanaona? Utasema kwamba umeme vijijini sasa hivi haujafika, mpaka Chuo Kikuu watu wanahoji wakati tulikuwa tunalalamika watoto wetu wanaishia *Form Six* na Chuo Kikuu kimejengwa ndani ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Watanzania wanaelewa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la usafiri kwa kule vijijini, usafiri mwingi uliokuwa unatumika ni wa baiskeli, leo mtu anasimama hapa anasema hamna kitu chochote ambacho kimefanyika, sasa hivi vijana wengi wana pikipiki, hayo siyo maendeleo? Ninaomba tujaribu kuwaongoza vizuri Watanzania hawa waelewe Serikali yao inawafanya nini. Katika hili kwenye mapato, nitamwomba Waziri nisije nikasahau kwamba aangalie vizuri kuhusu kodi ya pikipiki huko vijijini kwani zinasaidia sana, vijana wengi wanajajiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tuwe tunajiuliza, unaposema kwamba Serikali imefanya nini lakini na wewe vidole vinne vinakuuliza umewafanya nini wananchi. Kwa hiyo, tunapozungumza ndani ya nyumba hii, tuwe tunasema kwamba Serikali imeshindwa kufanya hivi lakini mimi nimefanya hivi. Kwa hiyo, ninaomba tuendelee kuzungumzia masuala ya wananchi kuhakikisha kwamba maendeleo tunayasimamia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kusahau, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia, lakini ili tuendelee vizuri na mikakati ambayo tumejiwekea, mipango mizuri ambayo Mawaziri wetu wamezungumza, bajeti yetu ni nzuri, mipango ni mizuri na tunaenda vizuri kabisa, tujaribu kuendelea kuisimamia miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la barabara tumejitahidi kiasi cha kutosha sana, kama tumeshafikia kufungua Mkoa kwa Mkoa sasa hivi tunaelekea Wilaya kwa Wilaya, kwa hiyo naomba nisisitize tu kwamba bajeti hii iangalie, kwa sababu mtu anatoka Dar es Salaam kwa barabara ya lami mpaka Nairobi, kimebaki kipande kidogo tu kilomita 22 pale Manyoni, hiki ni kitu ambacho kwa kweli ni lazima tusimulie kwamba Serikali ya CCM imefanya kazi kubwa sana, tunaomba magari yenze uzito mkubwa yassiingie Mjini Mwanza, tuimarishe barabara ya Usagara na magari yenze uzito mkubwa yakatie Usagara na yaingie Kisesa na yaelekee kama ni Nairobi au Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ningeomba barabara hii ya Kamanga kwenda Sengerema, mtusaidie sana kwa sababu tumeshaboresha ya Usagara kwenda Sengerema lakini bado kuna wananchi wengi wanapita maeneo ya Kamanga, hiyo barabara iboreshwe iwekewe lami ili iweze kuwasaidia sana wananchi wanaoishi katika Wilaya ya Sengerema na wanaoelekea Geita na kwenda Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nasisitiza suala la uwanja wa ndege wa Mwanza, naungana kabisa na Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella kuzungumzia Uwanja wa Mwanza. Tumekuwa tukihudumia watalii kutoka Arusha, wanatua kwa ndege

Arusha, lakini uwanja wa ndege wa Mwanza kama tukiukarabati Serengeti ni karibu sana, tutakuwa tumekusanya mapato mengi ya utalii kwa kupertia uwanja wa ndege wa Mwanza kwa kuwavutia watalii waende Serengeti ili wakajionee Mbuga zetu za Wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine zuri zaidi kwa Uwanja wa Mwanza, sasa hivi kuna kisiwa cha Saanane, kina wanyama wazuri sana pale na ni kivutio kizuri ambacho kitaongeza uchumi wa Mkoa wa Mwanza kama uwanja huu wa Mwanza utakarabatiwa na kuwa wa Kimataifa, watalii wengi watakuja tena na kutuungisha katika kisiwa chetu cha Saanane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Kati, ni muhimu, imezungumziwa na watu wengi, mizigo mingi tunaipoteza, ninaomba kwa msisitizo mkubwa kwamba reli hii ikarabatiwe ili iweze kufanya kazi na wananchi wengi wanaitumia ili waweze kufika katika maeneo ambayo wanatakiwa wafike.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado ninaomba kuhusu Feri ya kutoka Nansio kwenda Irugwa Ukerewe, tumsaidie sana Mheshimiwa Balozi Mongella, watu wa Irugwa wamekuwa wakihangaika sana kupata usafiri wa kufika maeneo hayo, mmetufanya mambo mengi, Feri ya MV Misungwi imefanya kazi vizuri, ya kutoka Kisorya kwenda Nansio inafanya kazi vizuri, bado ninaombea ndugu zangu wa Irugwa wapate feri ili iweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kupunguza umaskini tunagusa Kilimo Kwanza, ninaposema Kilimo Kwanza unamgusa mwanamke, wanawake wengi wanakuwa wasimamizi wakuu mashambani na ni waaminifu sana hata wakipewa mikopo wanawenza wakarudisha kwa kusaidiwa, lakini tunasema kwamba tupitishe Benki ya Kilimo ambapo benki mara nyingi zinatumia riba kibashara, ninaomba Waziri wa Fedha na Uchumi ahahakikishe kwamba fedha za Kilimo Kwanza zinapitia kwenye *SACCOS* ambazo nyingi wanawake wamejiunga kule, akina mama wa Mkoa wa Mwanza wana *SACCOS* zao nzuri kila Kata kuna *SACCOS*, ninaomba Wizara ya Fedha mtupitishie fedha hizo kupertia *SACCOS*, wale wenye miradi mikubwa basi wataenda kwenye mabenki ili waweze kusaidiwa. Naomba sana tuwawezeshe wanawake kwa kupertia kwenye *SACCOS*, *SACCOS* hizi zinawajumuisha wanawake wengi na ni waaminifu, ninaomba sana wawezeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake ipo lakini nayo inajiendesha kibashara ndiyo maana sitaki kuizungumzia lakini bado tunaiomba na yenye kwa sababu bado iko Dar es Salaam iende Mikoani, wanawake wa Mwanza wanaihitaji sana, mkafungue tawi pale Mwanza ili iweze kuwasaidia akina mama wale wenye mitaji mikubwa, wako tayari kukopa lakini *SACCOS* ndiyo mkombozi mkuu kwa wanawake wote walioko katika Mkoa wangu wa Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii, niombe mambo yangu mawili yafuatayo, tunapoanza kutoa fedha za maendeleo kusaidia Wizara hizi, ninaomba Wizara ya Nishati na Madini tuiangalie sana, ni Wizara ambayo inakusanya mapato, sasa hivi

ninaomba tuwawezeshe *STAMICO*, tuwawezeshe Wakala wa Kukagua Madini, tukikagua madini, nafikiri hawa wakala ambao wameshaanza kazi yao nzuri, wakisaidiwa na *TRA*, tunaweza kupata mapato mazuri sana kutokana na madini yetu tuliyonayo. Sasa nakuomba Waziri unapoanza kugawagawa, angalia Wizara ambazo unaweza kusukuma pesa zako haraka sana na zikazalisha zikaweza kurudisha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niwashukuru sana *TRA* kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, *TRA* ni mamlaka ambayo sasa hivi imetufikisha hapa, ingawa wale wengine hawaoni hata juhudhi na kuwapa ahsante, niwaombe katika awamu hii, *TRA* waendelee kwa moyo wao wa kujitolea kuhakikisha kwamba mapato yanasmamiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nashukuru na sasa nitamwita Mheshimiwa Ruth Msafiri.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kutoa salamu za shukrani kwa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uongozi wake mahiri na makini. Kwa kipindi cha miaka mitano, amewezesha Taifa letu kuweza kusonga mbele, ametupatia nafasi kubwa ya kupata muda wa kuchangia katika vikao hivi na sasa tunapohitimisha, sisi tunamwambia hongera kwa kazi, amepambana na majanga makubwa, majanga ya ukame, amepambana na mafuriko, lakini bado ameweza kulifikisha Taifa letu mahali hapa, nataka nimpongeze sana, salamu hizi zinaenda kwa wote walioshirikiana naye pamoja na Baraza lake la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kuwatetea wazalishaji wadogo wadogo wa Taifa hili, ni wachangiaji wazuri katika uchumi wetu na wakiandaliwa vizuri wanaweza kuliwezesha Taifa letu kusonga mbele. Ninaomba Serikali isipandishe zile *CC* za kuanzia 0 - 2000 kwa sababu kwenye zile *CC* 0-2000 unakuta ni pikipiki, bajaji na magari madogo madogo ambayo mimi naamini ni kwa ajili ya kusaidia wale wazalishaji wadogo wadogo, yanayoweza kwenda kwa mwendo wa kasi kuponya maeneo mbalimbali na hakika haya si magari kwa ajili ya watu wakubwa, si magari kwa ajili ya *luxury* ni kwa ajili ya kuwezesha shughuli za familia, akina mama kupeleka watoto shule na kurudisha watoto shule na kuwahi shughuli mbalimbali. Ni mwaka jana tu ambapo tumeidhinisha vyombo kama pikipiki kutumika kwa ajili ya usafiri, ni mwaka juzi tu tuliposhusha hizi *CC*, sasa tena mwaka huu tunapoanza kuzipandisha, nafikiria pengine tungeacha kwanza, tukaona huu mwelekeo na tukasimama katika upande mwingine, tukawezesha kwa mfano pikipiki kuwa na sheria nzuri, zikasimamiwa na kuweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba vyombo hivi ni kwa ajili ya vijana na kwa ajili ya familia zinazoinukia na kwa kweli ni za wazalishaji wadogowadogo. Mimi naomba, magari yenye *CC* 0-2000 si magari ya kuliingizia Taifa hili pesa nyingi, ni magari ya wajasiriamali wadogo wadogo, kwa kweli yangeondolewa

katika kuongezewa kodi. Kodi ianzie na magari yenyeye CC 2000 na kuendelea, litoe pesa nyingi tu hata hizo zilizowekwa zinaweza zikaongezwa kwa sababu si gari ya mahitaji, ni gari ambalo lina kazi maalumu na mtu anayetaka kununua gari kubwa hivyo, sisi tunafikiria kwamba anawea pia akasaidia kutoa mchango wake mzuri kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natetea vyombo hivi kwa sababu misamaha iliyotoka humu, kwa mfano kupunguza kodi kwenye mifugo, Kilimo Kwanza, hao ndio wanaotegemea kutumia hivi vyombo vidogo vidogo kubeba majani ya mifugo, ndivyo vinabeba chakula, sasa unapoviongezea kodi muda mfupi tu, nafikiria hapo wazalishaji tunakuwa hatujawapa nafasi. Naomba hili Serikali yetu iliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika wazalishaji wadogo wadogo, waangalie makampuni madogo yanayoanzishwa na Watanzania. Mwaka jana, niliongoza kikosi cha wanawake fulani ambao walitaka kuanzisha kampuni lakini walishindwa, kwa sababu kabla mtu hajawaza kuanzisha kampuni kufikia mahali pa kuisajili anaambiwa akishaipatia *TIN Number* aikadirie, halafu aseme kwamba atapata kazi ya kiasi gani aanze kulipa. Sasa mimi nashangaa Watanzania wenyeji wanapotaka kuanza kazi za kujiinua, kwanza walipe, wageni wakija wana kipindi cha huruma, hii ni kitu ambacho Serikali yetu inatakiwa kukiangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni yote madogo madogo ya Kitanzania ambayo akina mama nao wameinukia kujuunga humo, ninaomba na yenyewe yawe na kipindi cha huruma kisichopungua miaka mitano kama wanavyopewa wageni, ili kusudi wanapoanzisha hizi kampuni zifanye kazi, walipe pale tu wanapokuwa wamepata kazi za kufanya ambazo zinaonekana, baada ya kupata *TIN Number* wawe na ruhusa ya kuweza kupata kazi na Serikali iwatambue waweze kupata kandarasi za ujenzi wa barabara, waweze kupata *tender* za kuuza vifaa kwenye maeneo ya Serikali na yejote aliyekubalika, wakiwa wana msamaha na wakiwa wanafanya hivyo kwa ruhusa, si kama wanafanya hivyo kwa wizi, kwa sababu kama hatutawenza kuyaangalia makampuni ya Kitanzania na pale ambapo wanawake wanakwenda, tutakuwa kwa kweli tumewanyima nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine kwa wazalishaji wadogo wadogo, Taifa letu kuna wakati liliwahi kuingiza pesa nyingi zinazotokana na uvuvi, lakini wavuvi katika bajeti hii hawajapewa nafasi maalum. Naomba wavuvi wapewe nafasi maalumu, tusimalizie jambo moja tu. Ni jambo jema sana kuwaambia wavuvi watunze mazingira na mimi naunga mkono, samaki niliokuta Ziwa Viktoria, ningependa nikafa na watoto wangu na wajukuu zangu na wajukuu zao wakaendelea kukuta samaki katika Ziwa Viktoria, lakini njia gani inayowawezesha sasa ya kumfanya baada ya kuwa ameshanyang'anywa ule wavu wake aliokuwa anautumia ambao unaitwa ni haramu sasa anasaidiwa kifaa gani? Kwa sababu kile alikinunua kwa pesa na kuna kiwanda kinatengeneza na kimeonekana hakifai na kinapoonekana hakifai, unapomnyang'anya mtoto wembe anapokuwa anacheza unampa mti wa kuchezea, kumnyang'anya wembe ukamuacha peke yake, mtoto atalia, sasa na wavuvi wanaponyang'anywa wavu wapewe kitu kingine mbadala hata kama ni kwa mkopo wasiachiwe tu kwamba kwa sababu nyavu zimechukuliwa hazifai ni haramu basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba Serikali idhibiti watu wake, kwenye Ziwa Viktoria, kuna watu wabaya sana, wanajiita sijui Maafisa Maliasili, sijui wanaitwa akina nani, hata jana walikuwa kwenye Visiwa vya Ngumbile, wanafanya vurugu. Wamefika pale tena nyuma tu ya Mkuu wa Mkoa nao wanaanza kunyanga'nya watu mali zao, wanatoza shilingi laki moja moja, hamna hata risiti, mimi naamini kabisa huu siyo utaratibu wa Serikali, ni utaratibu wa watu ambao wanapenda kutumia vibaya jina la Serikali yetu. Kwa hiyo, mimi ninaomba wavuvi waangaliwe na taratibu pia ziwe, wasiachwe tu kuendelea kutumia vifaa haramu lakini hawaelekezwi watafanya nini na wala hawapewi msaada wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nakiomba, ni suala la Kilimo Kwanza litiliwe umuhimu mkubwa sana. Sisi tunaokaa karibu na Ziwa, nataka nijumuushe na suala zima la maji, ni mionganoni mwa watu ambao tuna matatizo makubwa ya maji. Mradi wa Kilimo Kwanza unasema kwamba mionganoni mwa mambo yatakayofanyika ni pamoja na kuimarisha na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, mabwawa yatachimbwa, pamoja na uvuvi wa kuvuna maji ya mvua, lakini sisi tunaopakana na Ziwa Viktoria mbona tunaendelea kuwa na shida ya maji? Tulizoea kutumia maji yale yatokanayo na mito yetu ya asili, sasa hivi mito ya asili hatuna, imekauka kwa sababu ya uharibifu wa mazingira, ninaomba masuala haya yaende pamoja, Kilimo Kwanza kitusaidie na maeneo yanayofaa kwa kilimo yatambulike na waweze kutusaidia kufanya kazi. Vilevile ninaomba suala la maji kwa watu wanaozunguka Ziwa na wale wanaoishi ndani ya Visiwa wawe na maji yaliyosafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nimalizie kwa kuomba nyenzo moja muhimu sana, umeme wa vijijini. Umeme wa Vijijini pale ambapo umeshafika kama Muleba sioni kuna sababu gani inayachelewesha watu wa Kagoma wasipate umeme, sioni kuna sababu gani inayachelewesha watu wa Mshabagu wasipate umeme. Hizi ni *center* kubwa ambazo zimeibukia na zinakua, umeme upo kilomita kama 10-11 kutoka Muleba, sasa kama kuna watu ambao wako tayari kuutumia na wanaonekana wana nia kwa miaka na miaka, naomba *REA* au *TANESCO* kwa pamoja wajipange kuhakikisha kwamba wananchi katika maeneo ambayo umeme ulishafika karibu wapate umeme. Kinachobaki sasa wahamasishwe kuweka vitu ambavyo vitawezza kuwa ni vya kuzalisha kuipa pato *TANESCO* ili isije kuwa wamepeleka tu umeme kwa ajili ya huduma tu. Lakini naomba suala hili lisiendelee kuwa ni la kusuasua, hawa watu wetu wanafikiria kuwa labda sisi tunazungumza hapa tunazungumza kwa kujifurahisha, tunatamani kuona umeme unawaka katika maeneo yote ambayo yanaweza kufikiwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Kuna Mheshimiwa Mmoja ameniandikia hapa, amesema hebu jionee mwenyewe jinsi vijana wanavyopenda mpira, ukiona waliomo humu ndani ni watu wenye umri mkubwa tu, umri mkubwa nao una umuhimu wake katika mambo mengine, ahsante. (*Kicheko*)

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kweli dakika zenyewe ni chache mno, utanisamehe, shukrani hazitakuwa nyingi sana lakini nia yangu ilikuwa ni kuzitoa nyingi hasa. Kwanza, kwa Serikali ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, inafanya kazi vizuri sana, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri wote wanafanyakazi vizuri sana. Pili, niwapongeze Waziri na Naibu wake pamoja na wafanyakazi katika Wizara ya Fedha, kwa kutuletea hotuba nzuri sana. Kwa hiyo, ninataka kuwahakikishia kwamba toka mwanzo naunga mkono hotuba hii. Ni hotuba nzuri sana lakini imekuja katika wakati mgumu. Wakati mgumu wenyewe ni kwa sababu mfumuko wa bei sasa hivi uko juu sana, asilimia 9.4 ni kubwa wakati tulikuwa tumesharudi mpaka asilimia 4.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hali ya maisha kwa vyovyyote vile hasa kwa chakula na usafiri, yote yanakuwa magumu. Kwa hiyo, bajeti hii inajaribu tu kusaidia kidogo lakini kusema kweli, hali ni ngumu. Hapo hapo wenzetu wahisani wametukacha, wamepunguza kiasi cha dola milioni 297, ni kiasi kikubwa sana cha fedha, sisi hatukuwa tumejiandaa. Sasa mimi hapo sijui nia yao hasa, sijui ni kwa sababu ya uchaguzi huu ndio watushike pabaya! Lakini pamoja na hayo, tutakwenda na uchaguzi wetu vizuri na CCM itashinda hata kama hawaipendi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumze katika hali ngumu kwamba Serikali ijitahidi sana kuendeleza yale yaliyoanzwa na hasa nilitaka kuzungumzia juu ya kuimarisha nguzo kuu za uchumi wa Kusini. Kule Kusini tulitaka tuliweke pembedi suala la miundombinu ya barabara kwa sababu sasa hivi kazi kubwa imeshafanywa na Serikali. Lakini kuna kipande kilichobaki pale Muhoro kutoka Daraja la Mkapa mpaka Somanga, sehemu hii inatupa shida kweli kweli kiasi kwamba magari mengi yanakwama pale ingawa Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba tunapita lakini tunapita kwa hali ngumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema inawezekana kabisa kwa eneo lile la *Mkapa Bridge* kwenda Somanga wafanye kazi usiku na mchana hakuna simba pale, hakuna wanyama wakali, wakifanya hivyo, tunaweza kumaliza upesi ili nasi tujikomboe upande wa Kusini kuwa na barabara yenyе uhakika inayoweza kwenda wakati wowote ule bila wasiwasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika hayo, ni umeme. Naishukuru sana Serikali kwamba umeme wa *gas* kutoka Mnazibay, Mtwara hivi sasa umeshafika Lindi, umeshafika Masasi na sasa kutoka Mtwara unapelekwa kwenda Tandahimba, Newala mpaka Masasi tena. Mimi nawaambia umeme huu ni mzuri mno haujawahi kutokea Tanzania, ni masaa 24. Kwa hiyo, wenzeni hivi karibuni kwenye mwezi Juni, Julai, August, tutakuwa nchi iliyoendelea kwenye upande wa umeme, kipande kile kitakuwa na mambo ya ajabu kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa sijui kwa nini wakati mambo haya yanavyokuwa mazuri basi kunakuwa na vikwazo. Sasa hivi kampuni ya Artumas, ina shida sana ya kupewa fedha zozote kutoka kwa wahisani au wafadhili kwa sababu

haijatimiza masharti ya mikataba iliyomo katika leseni ya kuleta umeme kule. Hapa nataka kusema Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuna hii taasisi yetu inayoitwa *EWURA*, *EWURA* inakwamisha sana maendeleo ya kuleta umeme kule Kusini. Hawa mpaka sasa hivi hawajatoa leseni ya kuwaruhusu *Artumas* waweze kusambaza umeme katika maeneo yote. Katika kufanya hivyo, maana yake ni kwamba Waholanzi hawawezi kutoa karibu shilingi bilioni 35 au dola milioni 30, kwa Tanzania mpaka *EWURA* itoe leseni kamili ya kuendesha biashara ya kusambaza umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hebu angalia dola milioni 30 tunazikosa kwa sababu ya saini tu ya *EWURA* katika upande wa *tariff*. Sasa hizi *tariffs* wakati wa mwanzo *EWURA* hawakuwa wanahudhuria mikutano ya majadiliano ya awali, sasa mambo yamekamilika lakini *EWURA* wanatukwamisha. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hebu tukwamue bwana hata kesho ikiwezekana watie saini. Hivi ugumu uko wapi? Kama mkipenda basi mimi Mrope niende nikawashikishe peni hiyo ili watie saini, ili wananchi wa Mtwara waweze kuhakikishiwa fedha hizi zinapatikana. Fedha hizi ndio zitakazotuwezesha kusambaza umeme sehemu kubwa vijijini kwa sababu sasa hivi umeme *TANESCO* inaunganisha kwa shilingi 475,000. Sasa hebu fikiria kule vijijini nani atawenza? Kumbe kwa mpango huu wa msaada wa *Artumas*, tutakuwa tunalipa shilingi 60,000 mpaka 80,000. Sasa inaonekana kuna mtu pale ametukalia vibaya na hatutakii mema hata kidogo. Mimi nalia kabisa na jambo hili, Serikali hebu ingalieni, mhakikishe kwamba suala hili linakamilika na umeme wa watu wa Kusini unakuja ili nasi tuweze kuendelea. Hili naamini kabisa kesho, Waziri wa Nishati yupo, hapa bila shaka mtalishughulikia kuhakikisha kwamba masuala haya yanakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, ni kuhusu maji. Nashukuru sana Waziri wa Maji asubuhi amezungumza vizuri juu ya kuleta maji Masasi kutoka Mbwinji na ametuhakikishia kabisa kuwa mwisho wa mwaka 2011 mambo yatakuwa yamekamilika. Jamani chonde chonde, Masasi tumekuwa tukilalamika kwa muda mrefu, sasa kama Serikali imeamua kutoa fedha hizo shilingi bilioni 35 ili mradi huu ukamilike, tunaomba iwe kweli kweli ili wananchi wa Masasi waondokane na shida waliyokuwa wanaipata kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, katika masuala ya uchumi, Mtwara inakua upesi sana kiasi kwamba Serikali au watu wengine bila kuwekeza katika Bandari ya Mtwara, itakuwa ni hasara kwetu. Kuna makampuni makubwa yanataka kuja, umeme wa uhakika na kadhalika upo lakini bandari bado miundombinu yake haijakamilika. Naomba sana Serikali ijikite hapo kuhakikisha kwamba bandari ile inatumika kwa ajili ya ukombozi wa Kusini mwa Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ndugu yangu Mheshimiwa Wasira, Waziri wa Kilimo, pale Ndanda Masasi kuna kilimo cha umwagiliaji, tafadhali sana mradi wa Ndanda ambao Waziri Mkuu aliahidi kutoa shilingi milioni 250, tumeomba ziletwe upesi ili kukamilisha mradi wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja na mimi nina imani hata katika hali ngumu hii nahata kama Wapinzani wanabeza, wanabeza

kitu wasichokifahamu, hata wao wangekuwa kwenye Serikali wangefanya nini? Kwa hiyo, wanyamaze wasije wakatuondolea matumaini yetu katika kuendeleza Taifa hili. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru. Lakini kabla sijaanza, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Nampongeza sana Waziri, timu yake na Serikali, kwa bajeti ambayo ni nzuri na wale wanaosema bajeti hii itawanyonga Chama cha Mapinduzi mwaka 2010 walie kwa sababu bajeti hii ndiyo itapunguza idadi ya Wapinzani kwenye Bunge mwaka 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kazi nzuri ya Rais. Mnasema hatujafanya kitu, Mkoa wa Dar es Salaam miaka miwili tumejenga sekondari 90. Wilaya ya Ilala mwaka huu imeingiza wanafunzi 14,000 Kidato cha Kwanza, bado hatujafanya kitu? Watoto wenu ndio wanasoma shule hizo hizo, hata haya hamna jamani! Njooni mtazame mambo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza mpango wa Kilimo Kwanza. Nilitaka nitoe tahadhari kidogo. Watu wasitegemee fedha hizi ziende zikatumike ovyo. Kwa mfano, kuna masuala ya miundombinu ya maji, hatuwezi kuanza kutumia fedha hizi kwenye miundombinu ya maji wakati tuna Mikoa haina shida ya mvua. Fedha hizi ziende kwenye Mikoa ambayo haina shida ya mvua zizalishé mwaka huu wapewe malengo, mchele tani milioni moja, mahindi tani milioni mbili, ngano tani milioni, waanze kulima, wakishaanza kulima watakaposopata mazao mazuri mfumuko wa bei utakaposhuka wakati watalaam wanaandaa *program* za umwagiliaji katika maeneo mengine ambayo yana shida ya kupata mvua za uhakika. Sasa mtakapoanza kuwa na mipango ya kwenda tu kwenye *irrigation*, mnapoteza muda na mnapoteza nafasi ya Mikoa ambayo haina shida ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka kusema hilo. Huwezi ukawa unataka Kilimo Kwanza unavuna mara moja mchele, lazima tuvune mara tatu kwa mwaka. Tuwe na program kama hizo. Lazima tu-*champion* Mikoa ambayo itagusa na kuona sasa kilimo ndicho kinapewa kipaumbele katika Mikoa hiyo wakati watalaam wanaandaa *program* za miundombinu za maji kwenye Mikoa ambayo haina mvua. Naomba Waheshimiwa Wabunge, hizi fedha msizitumie kisiasa, kila Mkoa wapewe kwa sababu kila mtu anataka hizi fedha ziende, tutaharibikiwa, ziende kwenye eneo ambalo zitaleta *quick win* na zitaleta *impact*, kipindi cha miezi 12 tutaona tofauti ya chakula. Usalama wa nchi siyo Majeshi peke yake ni *food security*. Tukiwa na chakula cha kutosha usalama wa kutosha utakuwepo kwenye nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nazungumzia Dar es Salaam. Watu wengi tunalamika foleni, lazima Dar es Salaam itazamwe tofauti na Mikoa mingine. Sisemi ipendelewe Mikoa mingine ikanyimwa, tukiiboresha miundombinu na mipango ya Dar es Salaam, tutakuwa na uwezo wa kuwapatia *TRA* kukusanya zaidi na kurudisha katika Mikoa mingine. Kwa hiyo, Dar es Salaam lazima ipewe *extended autonomous*. Mpango wa Bunge hili ambaa walifuta leseni, ifikiriwe upya, Dar es Salaam iruhusiwe kukusanya

leseni za biashara ili tuweze kupata makusanyo ya kutosha na kuweza kuleta maendeleo mazuri. Tukishaboresha miundombinu, nyumba hizi zitapanda thamani, nyumba zikipanda thamani, tutakuwa na uwezo wa kuzitoza zaidi kodi za majengo ili kuleta maendeleo mengine zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna mpango ambao tulipewa, tuliambiwa kinadharia kuwa Mkoa wa Dar es Salaam, hospitali tatu za Mwananyamala, Ilala na Kinondoni zina hadhi za Kimkoa. Lakini hizi hadhi za Kimkoa bado haziendi kisheria tunapata matatizo ya kupata dawa za kuzipeleka kwenye hospitali kwa sababu wanaotoa dawa hawatambui hospitali hizi kwamba sasa hivi tayari zina hadhi za Kimkoa. Kwa hiyo, nataka niombe Serikali wakati inapofanya maamuzi basi iambizane wenyewe kwa wenyewe, *in house information*, hizi hospitali ziweze kuangaliwa kwa sababu dawa zinazokuja kwenye hospitali tatu za Mkoa wa Dar es Salaam, ni ndogo sana kufuatana na idadi na huduma zinazotoa. Temeke wagonjwa wengi, Ilala wagonjwa wengi na Kinondoni wagonjwa ni wengi sana. Serikali ijaribu kutazama upya, isitazame idadi ya wakazi wa Dar es Salaam, itazame vile vile na mahitaji yenye. Sasa hivi hospitali hizi tatu zinahudumia mpaka Mikoa mingine katika nchi hii, wanatoka mpaka nchi nyingine wanakuja Amana kutokana na huduma bora ambazo tunazo pale. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali wajaribu kulitazama suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu namshukuru sana yeche na Katibu wake na watalaa wake kwa kuichukua barabara ya Uhuru na sasa hivi wameshaanza kuiwekea fedha. Lakini bado kuna mgongano *TANROAD*, hawajui kama hii barabara Serikali imeichukua. Kwa hiyo, bado kuna mvutano kwamba barabara hii ni barabara ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, hapana. Hii barabara sasa hivi inataka ihudumiwe na mipango ya Serikali ambayo ipo ya kupunguza foleni isiwe tu Mwananyamala, Sinza, hata huku barabara ya Uhuru vile vile kuna foleni, tunaomba na Waziri wa Miundombinu yupo hapa, tunaomba alielewe hili na awaambie watalaa wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matumizi ya Serikali, Waziri wa Fedha amesema katika kitabu chake kuwa watapunguza ununuzi wa magari. Mimi nasema siyo kupunguza ni kuacha kununua magari. Magari yanayotakiwa yanunuliwe sasa ni magari maalum ambayo yataweza kutoa huduma vijijini. Hivi kiongozi unakwenda kijijini, unakwenda Mikoani unakuta wajawazito wanapelekwa kujifungua kwa kutumia baiskeli, wewe umekaa kwenye gari kubwa, hata mwenyewe kusema mnakwenda wapi hamna, huoni hata aibu? Naomba Serikali iache kabisa, inunue magari yale tu ambayo yatahitajika, magari ya Zimamoto, *Ambulance* na magari ya Majeshi yetu na vyombo vingine vya usalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mpya inaingia mwezi wa kumi...

NAIBU SPIKA: Mwezi wa 11 bwana.

MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU: Yako mazoea kila wanapoingia katika Serikali mpya au vyeo vipyta wanataka wabadilishiwe magari, wabadilishiwe na

furniture, matumizi haya ni makubwa mno. *Furniture* zilizonunuliwa na magari haya yaliyokuwepo, yanafaa yatumike na uongozi unaokuja. Kama kuna *furniture*, cha kubadilisha labda ni godoro kwa sababu litakuwa limetumika kidogo sana lakini vitanda na vitu vingine visinunuliwe kwa sababu vinapoteza fedha nyingi sana za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali ingeli-*revisit* tena watalaam wake au viongozi ambao wanastahili kusafiri kwa kutumia *first class*, kuna *abusement* kubwa sana kwenye mashirika na Serikali kusafiri kwenye daraja la kwanza na kutumia fedha nyingi sana. Kwa hiyo, naomba hili nalo litazamwe katika maeneo ya kupunguza matumizi ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipitisha Sheria ya *National Housing*, wananchi walifurahi sana ambao ni wanyonge, baada ya kuona kuwa sasa Serikali yao itawauzia hizi nyumba. Toka tumepitisha hii Sheria, ni zaidi ya mwaka mmoja hakuna chochote kinachofahamika au kinachoendelea. Nashangaa hizi *regulations* zinatumia miaka mingapi kuwa tayari. Lakini vile vile nyumba hizi zitakazouzwa, kwanza, wasiziuze kwa bei ya kukomoa wakati wanajua hawa wamekaa kwenye nyumba hizi kwa zaidi ya miaka 40 na walikuwa wanalipa kodi. Pili, kuwe na muda, wasishtukizwe tu au labda wafanyiwe njama watoke ili waingie wengine wenyewe fedha. Tunaomba hawa waliopo sasa hivi ndiyo wauziwe kwa bei ya nafuu kutokana na wao wenyewe kuishi humo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira, mfumo wa Serikali wa ajira utazamwe upya. Huu mpango wa *permanent* na *pensionable*, unafanya watumishi wa Serikali au watumishi wa umma kutokujibika kufanyakazi sawa sawa. Wanakuwa na *excitement* ya vyeo lakini hawana uwajibikaji kwa watu na hasa watu wa kipato cha chini. Yote kwa sababu akiharibu hapa anahamishiwa sehemu nyingine. Watumishi wa umma wafanye kazi kwa mikataba, anashindwa *ku-deliver*, anarudi nyumbani kwa mke wake au kwa mume wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna wanafunzi wengi sasa hivi *graduate* ambao wamehitimu katika vyuo mbalimbali, wanakosa maeneo ya kufanya kazi kwa sababu tayari watu wameshajikita na wanaendelea kuharibu kazi na wala hawawajibishwi. Kwa hiyo, naomba mfumo wa ajira ya Serikali utazamwe upya watu wafanye kazi kwa mikataba.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Naona kengele ya pili imelia, ahsante sana kwa mchango wako mzuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kila mmoja anaelewa kuwa nchi yetu ni masikini katika hali ambayo hata bajeti yake ni tegemezi. Lakini pamoja na kuelewa ukweli huo, bado nchi yetu iko mstari wa mbele katika kutoa msamahama kwa baadhi ya kodi na Wabunge kwa muda mrefu. Kwa kweli tumelisema

hili katika Bunge lako Tukufu kuwa kufanyike marekebisho ili pale tu ambapo kuna ulazima mkubwa watu hawa au mashirika hayo yasamehewe kodi na Serikali ilikuwa inajibu kwa vipindi tofauti kwamba itafanya marekebisho. Sasa ni vyema tuone toka lianze Bunge hili, Serikali ilikuwa na kauli gani kuhusiana na kadhia hii ya msamaha wa kodi ambao unachukua sehemu kubwa katika kuvujisha mapato kwa kweli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2006, Serikali katika kulieleza hilo ilisema hivi; kupitia upya misingi na taratibu za misamaha ya kodi kwa lengo la kuziba mianya ya kukwepa kodi. Hiyo ilikuwa ni kauli ya mwaka 2006 ya Serikali ilikuwa inaeleza kuhusiana na malalamiko au matakwa ya Wabunge kuhusiana na suala zima la kuziba mianya ya misamaha ya kodi.

Vile vile Serikali katika mwaka 2009, katika hii bajeti ambayo inaishia sasa, Serikali ilisema kuendelea kupanua wigo wa kodi, kupunguza misamaha ya kodi na kuendelea kuimarisha uchumi tulivu na mwisho hii bajeti ambayo tunaijadili, Serikali inasema kuwa kuendelea kuchukua hatua za kudhibiti misamaha ya kodi ili kuongeza mapato. Hizi ni kauli za Serikali zimetolewa katika vipindi tofauti kuhusiana na kadhia hii, lakini hali halisi ikoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika mwaka 2006 kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika mwaka huo wa 2006, fedha ambazo zimesamehewa au kodi ambayo imesamehewa ilikuwa ni Sh. 15,970,913,769/=, huo ndio mwaka wa mwanzo ambao Bunge lako Tukufu lilianza muda wake ambao unaishia katika mwezi wa Desemba. Tulitegemea Serikali kwa sababu katika kauli zote tatu ambazo ilizisema hapa kuwa wanajianda, wanaangalia utaratibu ili kupunguza sasa ilitegemewa kiwango hicho pengine kipungue au kuongezeka, basi kisiwe kiasi kikubwa lakini jambo la kusikitisha ni kuwa, kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya tarehe 30 Juni, 2009, kodi ambayo imesamehewa ni Sh. 752,398,800,000/=.

Hapa ikumbukwe kuwa mwaka 2006 ilikuwa shilingi bilioni 15, sasa kinachoonekana, hizi lugha katika hotuba hizi nyingine ni lugha za kawaida tu, kwa sababu haiwezekani kiasi hiki kikubwa cha fedha ambacho kinasamehewa, huku hii hali ya bajeti zetu inabidi zipate wafadhili au wahisani na maendeleo yetu hadi tupate wahisani huku sisi tunasamehe fedha. Kwa kweli hili haliridhishi na itabidi labda Waziri wa Fedha atupe lugha nyingine kwa sababu kama ni ahadi, tayari nimeisoma ahadi ambayo Serikali imesema kuhusiana na kadhia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua pengine nusu tu ya pesa hizi ambazo ni karibu shilingi bilioni 300 na kidogo na ukazinunulia *power tiller* aina ya *AMECK* ambayo moja inauzwa Sh. 4,500,000/=, basi Serikali au kwa kupitia pengine ingepelekwa katika Benki ya rasilimali ya Tanzania (*TIB*) wakulima wangeweza kupata *power tiller* yenye kabila ya *AMECK* 83,599, nusu ya fedha hizi. Vile vile nusu ya fedha hizi zilikuwa na uwezo wa kuiongezea bajeti karibu Wizara tatu kwa wakati ule ikiwemo Wizara ya Maji na Umwagiliaji ambayo kwa wakati ule ilikuwa na bajeti ya Shilingi milioni 230.6.

Sasa kwa kweli hili ni tatizo kubwa na Serikali inaonekana haiko makini kwa hili na wakubali kwa kuwa hili kwa kweli limewashinda. Badala yake wanabanwa, wafanyabiashara wa kati ambao hali zao kwa kweli sio nzuri kimapato na kawaida ya TRA unapoanzisha duka kwa mfano katika maeneo kama ya Kariakoo wakishakuwekea kiwango, basi hawajui kama duka linaweza likapata faida au likapata hasara, wao wanabakia na kiwango chao tu. Kwa kweli hili sio sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakaa katika Bunge hili, Serikali inaomba tujadili na kupidisha makadirio ya mapato na matumizi, lakini mara tu ikishapitishwa bajeti kunatokea wajanja wanakuwa wanaitia Serikali katika miadi na madeni na hili limedhihirika katika ukaguzi aliofanya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi cha tarehe 30 Juni, 2009. Serikali inasema bajeti yake ni ya fedha taslimu, yaani *cash budget*. Unachopata ndio unachotumia lakini kuna wengine wanatumia kile ambacho hakipo. Huu ni mzigo kwa wananchi kwa kweli na haistahiki.

Katika kipindi hicho, wajanja, hawa maafisa hawa au Serikali kwa ujumla wametumia, wameitia Serikali madeni na miadi ya Sh. 493,455,657,616/. Hizi hazikupitishwa na Bunge, hazikuidhinishwa na hizi zimetumika kwa kununulia vifaa, huduma za mafao ya watumishi. Sasa hata Mdhibiti kwa kweli kashauri kwamba wale wote ambao wamehusika na kadhia hii, basi wachukuliwe hatua za kinidhamu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hapa atatuhalikishia vipi kuhusiana na habari hii kwa sababu Bunge limepitisha vingine lakini matumizi yanafanya kwa kila mtu anajiona yeye kajitawala, kila mtu ana Serikali yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa fursa hii. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kwa kuitumikia Wilaya yangu ya Lushoto na nchi yangu katika kipindi hiki cha miaka mitano kwa nafasi ya Ubunge. Vile vile nimwombe Mwenyezi Mungu aendelee kuwaweka mahali pema Peponi wale wenzetu ambao tulianza nao Desemba mwaka 2005 lakini kwa uamuzi wa Mwenyezi Mungu wametangulia mbele ya haki.

Namshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuliongoza Taifa letu vyema na kupata mafanikio makubwa. Katika miaka mitano iliyopita, nilibahatika kusafiri na Mheshimiwa Rais katika Mikutano ya Wakuu wa Nchi za Afrika na Wakuu wa Nchi za Dunia, nilishuhudia kwamba Mheshimiwa Rais Kikwete anareshimiwa sana na kupendwa sana na Mataifa yote ya dunia na kupitia kwake Tanzania imeendelea kupata heshima kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe, Naibu Spika na Wenyeviti kwa umahiri mkubwa mliotuendeshea Bunge hili kwa viwango vyya Kimataifa. Ahsanteni sana na natumaini kwamba tutaendelea na utaratibu huo. Nichukue fursa hii pia kuwashukuru Wabunge wenzangu wa Wilaya ya Lushoto, Jimbo la Mlalo na Bumbuli, Mheshimiwa Ngwilizi naMheshimiwa Shelukindo, Madiwani wote, wenyeviti wote wa vijiji vyote tumeshirikiana vizuri sana kufanya maendeleo ya maajabu kwa kushirikiana na Serikali

yetu kuu na Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto. Vile vile namshukuru Mkuu wa Wilaya ya Lushoto Ndugu Sofia Mjema na watendaji wote wa Wilaya ile kwa ushirikiano mkubwa ambao ulituwezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi.

Nachukua nafasi hii vile vile kuwapongeza sana wapigakura wa Jimbo la Lushoto. Tumebuni mambo mengi pamoja, tumeshikamana na tumefanya mambo ambayo naweza kusema hayajawahi kutoke. Mwisho katika shukurani, nimshukuru mke wangu – Mariam, watoto wangu watano na wajukuu maana wakati wote nikiwa kule Jimboni au nikiwa huku mke wangu amenisaidia sana kuhakikisha kwamba kazi za Ubunge katika Jimbo la Lushoto zinafanyika kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya kipindi cha miaka mitano nimekuwa nikijiuliza, hivi Serikali yangu, Chama changu mimi mwenyewe na viongozi wenzangu tumewafanya yapi wapigakura wa Lushoto na nchi yangu kwa jumla? Niliona nichukue mifano tu katika maeneo yale ambayo yanawagusa wananchi kwa karibu sana. Katika eneo la elimu kipindi cha Ubunge 1996-2000, Jimbo letu halikubahatika kujenga Sekondari hata moja. Watoto wetu walipata ufadhilli kwa wenzetu Jimbo la Bumbuli na Jimbo la Mlalo. Mheshimiwa Shelukindo, ahsante sana.

Kati ya mwaka 2000 na 2005 tulifanikiwa kujenga Sekondari nne tu. Pamoja na Sekondari ya Wilaya ya Shambalai, uwezo wetu ulikuwa wa kuchukua wanafunzi 400 tu wengine walibaki majumbani. Wazazi wachache wenyewe uwezo waliwapeleka watoto wao shule za kulipia. Lakini katika kipindi hiki cha miaka mitano kwa kushirikiana na Serikali Kuu, Halmashauri na wananchi wasikivu sana wa Jimbo la Lushoto tumewenza kujenga sekondari mpya 22 na hivyo kufikia idadi ya sekondari 27 zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,500 kila mwaka, sawa na nyongeza ya nafasi 3,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ifuatayo inajieleza yenye. Wanafunzi 14,000 ambao wamejiunga shule hizi katika kipindi cha miaka mitano kwa elimu ya miaka minne ama wasingekwenda shule au wazazi wao wangelipa kati ya Shilingi bilioni 52 na bilioni 78 shule binafsi. Kwa hiyo, pamoja na faida hii endelevu tumewatoa watoto wetu kutoka kundi la watoto wa Mitaani na kuwaingiza katika kundi la watoto wasomi, wenyewe taaluma na ajira na vile vile kujenga hazina ya wataalamu wa Afya, Elimu na kadhalika.

Katika sekta ya afya huduma ya afya inapatikana katika Kata zote za Jimbo la Lushoto. Nawashukuru sana wenzetu wa Wizara ya Afya, tumesaidiana nao vizuri kurekebisha zahanati zetu kuwa Vituo vya Afya na tumeanzisha kujenga Zahanati mpya katika vijiji vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji bado inatusumbua, lakini bandu bandu humaliza gogo. Hatua kwa hatua tutafika. Kwa upande wa barabara, nashukuru TANROAD, Mkoa na Halmashuri ya Wialya ya Lushoto barabara zote zinapitika kipindi chote cha mwaka. Ni dhahiri maboresho yanahitajika hapa na pale, lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Mbunge wao na wananchi tumeshirikiana vizuri, kazi ni nzuri imefanyika. Niombe tu Wizara ya Miundombinu kwa vile iko hapa, ile barabara ya

Mlalo kwenda Mlola kwenda Mashewa tusaidiwe ili iboreke ipitike kipindi chote cha mwaka.

Sehemu ya mawasiliano, naomba tu kumkumbusha ndugu yangu Waziri wa Mawasiliano kama yupo hapa, ahadi yake ya kuvisukuma vyombo vyaa mawasiliano kujenga minara ya mawasiliano, Tarafa ya Mlola. Hiki ni kilio kikubwa kwa wananchi wa maeneo hayo. Ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja nilimwona pale, sijui katoka! Lakini iko ahadi ya Serikali kwamba mradi wa kufikisha umeme Tarafa ya Mlola utatekelezwa mwaka huu 2010/2011.

Naomba sana katika ile *single line budget* ya umeme vijiini, mradi wa kufikisha umeme Ngwelo, Malibwi, Mlola na kwingineko Tarafa ya Mlola ufanyike mwaka huu. Kuhusu kilimo, nilifurahishwa sana na kauli ya Mheshimiwa Mwandosya kuhusu umuhimu wa kujenga mabwawa madogo madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wilaya ya Lushoto tukisaidiwa mabwawa madogo madogo tukalima kilimo cha mboga na matunda tutapata faraja kubwa zaidi.

Mwisho, nzungumzie suala la ajira na uwezeshaji. Wilaya yetu haina viwanda, tunaomba sana wenzetu wa Wizara husika watusaidie kuanzisha viwanda vidogo vidogo, hasa viwanda vyaa matunda ili ajira iweze kupatikana kwa vijana wetu ambao hawakubahatika kwenda shule kipindi cha nyuma.

Nirudi tena kwenye barabara kuu, namshauri Mheshimiwa Kawambwa kwamba barabara zetu kuu ziwe na *loops* ili zisijifunge ikitokea ajali.

Hizi barabara za *loop*, Mheshimiwa Kawambwa hata kama ni za udongo zitasaidia sana angalau inapotokea ajali angalau tuweze kuchepuka kupitia maeneo mengine. Hilo lilikuwa ni ombi langu na sisi wa Lushoto kuna hii barabara ya Duchi Mombo, ikitokea tatizo katika barabara kuu hii ya Mombo – Lushoto, basi sisi ndio hatuna njia mbadala. Kwa hiyo, suala hili la njia mbadala naona kama ni muhimu sana. Nikirudi kwenye Wizara yetu ya Fedha ambayo nilibahatika kufanya kazi kwa miaka 20 na Mheshimiwa Mkulo alikuwa pale, niseme hongereni kwa kazi nzuri. Mchango wangu nimeutoa kwa maandishi, nakutakia kheri Mheshimiwa Mkulo urudi tena katika Wizara hiyo,

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kusimama katika Bunge hili wakati huu nikiwa mzima na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nakushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa maoni yangu. Nampongeze Mheshimiwa Waziri kwa namna alivyozisoma hotuba zote mbili, lakini kipekee

nampongeze sana Mheshimiwa Hamad Rashi Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kutoa hotuba nzuri ambayo ina utafifiti wa kina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu ambazo tumezipata hivi karibuni kutoka kwa Mkurugenzi wa Vitambulisho vya Taifa ni kuwa Watanzania tayari tumeanza kufikia watu milioni 43. Katika watu wao milioni 43 tumeelezwa kuwa milioni 21 ndio nguvukazi, yaani waliokuwa wana uwezo wa kufanya kazi. Lakini katika milioni hizo 21 unatoa milioni saba za wale watu ambao hawawezi kufanya kazi, wengine bado ni watoto, wengine ni vilema, wengine wana matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini watu milioni 14, Watanzania tunatakiwa tuchangie pato la Taifa, yaani kwa kulipa kodi. Lakini jambo la kusikitisha ni kuwa Watanzania ambao wanalipa kodi ni 1,550,000 kwa mujibu wa takwimu ambazo zimetolewa na *TRA*. Sasa watu ambao wanachangia kodi wameelezwa kuwa ni 400,000 ambao ni wafanyakazi wa Serikali; 600,000 wanatoka katika sekta binafsi; na 570,000 hawa ni wafanya biashara yaani wenye *TIN*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa katika milioni hizo 14 zilizotajwa, watu 1,550,000 ndiyo wanaochangia kodi ya Taifa na watu ambao kuwa wanapata milioni 12.7 hawa hawachangii kodi. Sasa hili ni jambo la kusikitisha na linafaa lifanyiwe kazi. Watu hawa wote kutokulipa kodi ndiyo wanaosababisha. Naomba nikuchukue pale kwenye ukurasa wa 73, Mheshimiwa Waziri anapozungumza kuwa washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuendelea kuisaidia bajeti yetu mwaka 2010/2011 kwa kutupatia misaada na mikopo ya jumla ya shilingi trilioni 3.27.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi ni nyingi sana kwa kutegemea msaada. Kwa hiyo basi, mimi naseme nchi yetu siyo masikini kiasi hicho. Tuna sehemu nyingi ambazo tukizifanya kazi zinaweza kutuongezea pato la Taifa. Hebu tufanyeni kazi katika bahari. Tuiangalie bahari. Bahari kule siyo sawasawa na kulima, kwamba kwanza ulime halafu upalilie, halafu uvune. Bahari unapokwenda, unavuna tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa tutanunua meli za kuvulia, meli za kisasa kabisa, tukavua samaki, tutapata samaki wa kutunufaisha sisi wenyewe kwa kupata chakula pamoja na samaki wengine wa kusafirisha nchi za nje na kujiongezea pato la Taifa. Vipaumbele vingi sana tumevitoa katika bajeti yetu ya Kambi ya Upinzani. Tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mawaziri wengine watakaokuwepo kwamba bajeti ile tulioitoa sisi hatukutoa kwa sababu ya kujisifu au kutaka kuonekana kuwa tunajua, sijui vipi, sisi tunatoa kwa sababu ni wazalendo. Tunataka kuisaidia nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa tutaamua hasa kufanya kazi katika bahari, basi nchi yetu itanufaika. Tukitoka hapo, kila siku tunakuwa tunalalamika kuwa bajeti zetu ni tegemezi, bajeti yetu ni finyu. Bajeti yetu inachelewa kupata pesa za maendeleo kwa sababu ya kuwategemea watu. Wao wenyewe wakusanye bajeti zao mpaka wenyewe watumie halafu tena waangalie namna ya kutusaidia na sisi wakati kuna watu nguvukazi

milioni 12, hawa hawachangii pato la Taifa. Ni aibu! Inabidi tujirekebishe kutokana na hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nilichangie hapa ni kuhusiana na vipaumbele vya bajeti. Vipaumbele vya bajeti viliviyowekwa mimi sipingani navyo, lakini naomba na hizi Wizara ambazo sio vipaumbele, hazijawekwa katika vipaumbele, nazo bajeti zao zisipunguzwe mpaka zikawa ndogo wakashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda bajeti hii ya Mahakama iwe ina fedha za kutosha ili Majaji pamoja na Mahakimu waweze kufanya kazi zao ipasavyo. Mimi nilitegemea kuwa Idara hii safari hii itapewa Mfuko wake kwa sababu Mheshimiwa Rais alitangaza kuwa Idara ya Mahakama itapewa mfuko wake kama vile Bunge, lakini nashangaa haijafanywa hivyo. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwa nini isifanyiwe hivyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninapenda nilizungumze ni ile asilimia 4.5 tunayopewa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoka kwenye mapato ya Muungano. Kila siku hapa tunaambiwa kuwa suala hili linashughulikiwa. Vuteni subira, fanye hivi, kila siku suala hili halipatikani jawabu. Kwa nini kila siku tunakuja hapa tunazungumza jambo hili hili? Kila tunapozungumza, mara tunaambiwa sijui kuna Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano imekaa, karibuni itatoa matokeo. Lakini mpaka leo kila tunapoingia kwenye bajeti, ndiyo ile ile asilimia 4.5. Sasa Mheshimiwa Waziri, tunaomba hebu utupe ufumbuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nitapenda kulizungumzia ni kuhusiana na fedha ambazo zinapotea kutokana na Taasisi, Wizara za Serikali pamoja na Idara za Serikali kutokupeleka kazi zao kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na badala yake zinapelekwa kwa watu binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linasikitisha kwa sababu ipo Taasisi ya Serikali, lakini watu hawaendi kwenye Serikali, wanapeleka kwa watu binafsi. Kuna nini huko kwa watu binafsi hata watu wakapeleka huko, wakaacha kupeleka kwa Serikali? Kuna jambo gani linalowavuta kule hawa waende kule? Kuna jambo huko Mheshimiwa Waziri, tunaomba mfuatilie. Fedha nydingi zinakwenda kule haziji kwenye Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kutokana na msongamano wa magari ambayo yako Dar es Salaam. Suala la magari Dar es Salaam limekuwa ni kero hasa unapoendesha gari, hata ukifika nyumbani umechoka, safari ndogo tu inakuwa kubwa. Tatizo kubwa magari yamekuwa mengi na barabara hakuna. Matatizo ya barabara yanakuwa pale kwenye *junction*, yaani kwenye viungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napendekeza kuwa tujenge *fly overs*. Mambo mengine yote tunayosema hayatatusaidia. Ukitisema utaleta mabasi yanayokwenda kwa kasi, yatapita barabara ile wanayokwenda kwa kasi, lakini magari mengine yaliyokuwa

hayaendi kwenye barabara ya kasi yatakuwa pale pale kwenye foleni. Uwezo wa kujenga *fly overs* upo, tunajenga madaraja marefu sana.

Kuna daraja la Mkapa kule, refu! Kuna madaraja mengine huko ya kuunganisha Tanzania na Msumbiji, hata daraja la Mto Ruvu lile nalo unaweza ukajenga *fly over*. Lakini tunasema hatuna uwezo, wakati uwezo tunao. Fedha zipo, hizo hizo tulizonazo, naomba tuliangalie Jiji letu, linatupotezea nguvukazi nyingi, watu wanachelewa kwenda kwenye kazi zao. Nashukuru sana. (*Makofî*)

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii nami niweze kuchangia katika hoja ya hotuba ya Waziri wa Fedha ambayo iko mbele yetu. Naomba nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini ambao wamenifikasiha hapa ambapo leo ni miaka mitano sasa kwa upande mmoja wa Jimbo lile, lakini miaka 10 niko nao nafanya nao kazi vizuri na kazi inakwenda vizuri zaidi na zaidi kadri siku zinavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda niwapongeze na niwashukuru kwa ushirikiano mzuri ambao katika miaka hii waliyonipa. Pia niipongeze au niishukuru familia yangu vile kwa ushirikiano, kwa uvumilivu waliokuwanao katika muda wote ambapo nilikuwa na majukumu ya kushughulika na wananchi. Labda niende moja kwa moja kwenye hoja mbalimbali ambazo zipo mbele yetu, nikianza na suala hili la uwekezaji.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tumeambiwa kwamba uwekezaji wa mitaji ya kigeni ya moja kwa moja, yaani wanaita *Direct Foreign Investment* katika nchi yetu inazidi kupungua. Hivyo hivyo mazingira ya kufanya biashara katika Tanzania inazidi kuwa siyo *conducive*, yaani siyo ya kuvutia. Sasa mimi nadhani kuna haja ya kuangalia sababu ni zipo. Naambiwa kuna taarifa ya Benki ya Dunia ambayo imeelezea kwa nini mazingira ya kufanya kazi au biashara katika Tanzania yanakuwa siyo rahisi, gharama ni kubwa katika uwekezaji katika nchi yetu. Nilidhani ni vizuri Serikali ikaangalia kwa makini zaidi ili tusiende wakati tunalenga malengo ya kwenda mbele, lakini huku tunaweka *reverse gear* katika mipango yetu mbalimbali. Kwa sababu tunaamini pamoja na mengine, basi kutakuwa na suala la kutowajibika ipasavyo suala la urasimu na suala la rushwa. Mambo hayo yakiangaliwa, naamini wawekezaji watakuja kwa wingi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la kilimo. Kilimo katika nchi yetu kila mmoja anafahamu ni uti wa mgongo wa uchumi wetu na kwamba tumefikia hatua sasa ya kusema Kilimo Kwanza, yaani kauli mbiu ambayo inatuhamasisha wote tuone kwamba kilimo ni msingi ambao lazima tuegemee katika kujenga uchumi wetu. Lakini niseme tu kwa haraka haraka kwamba uchumi, kilimo chetu; kwanza niipongeze Serikali, inafanya vizuri na vile vile kuja suala la ruzuku kwa wakulima katika eneo la pembejeo. Lakini eneo hili la ruzuku linahitaji kurekebishiwa.

Kwanza ruzuku hii kwa mfano kwa njia ya vocha inapashwa kwenda kwa wakati. Mara nyingi wakulima wetu kwa miaka miwili mfululizo sasa wamekuwa wakilalamikia

juu ya ucheleweshwaji wa pembejeo hizi kwamba hazifiki kwa wakati. Lakini pia kumekuwa na hitilafu za hapa na pale katika kuendesha shughuli hizi za kugawa zile vocha na kadhalika. Mojawapo ni pamoja na *forgeries*, unaweza kukuta kuna majina ya watu yaandikwa lakini kumbe siyo wahusika katika kugawiwa hizo vocha.

Lakini pia kuna mbegu bandia, nadhani Serikali ni vizuri ikachukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba hakuna mpenyo wa hitilafu kama hizo. Suala lingine katika hili ni kwamba kuna wakulima wengine hawahitaji mbegu pamoja na mbolea. Unakuta mtu ana shamba lenye rutuba ya kutosha, anahitaji mbegu tu. Sijui kama Serikali inalionna hili! Lakini ni vizuri kama mtu anaweza kuwa na *option* ya kuchagua, basi apewe nafasi hiyo.

Lingine katika kuboresha kilimo, kwa mfano katika Jimbo langu la Babati mwaka huu tunatarajia kuvuna kwa kiasi cha kutosha mahindi na mbaazi. Sasa linakuja suala la soko, lakini suala la soko kwa wakati huu linagubikwa na suala zima la vibali. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Serikali itoe ruhsa kwa wakulima kuuza mazao yao *freely*, yaani kwa uhuru na kuweza kujipatia fedha za kusomesha watoto wao, kujitafutia riziki zao na kujiendezea kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka nilizungumze ni suala la ardhi ambayo ni msingi mmojawapo katika njia kuu za uzalishaji katika nchi yetu. Sasa ardhi katika jimbo langu la Babati Vijijini limekuwa ni tatizo kubwa lina mgogoro mkubwa wa miaka mingi, mgogoro kati ya Chama cha Ushirika *RIVACU* na wakulima ambao wanaishi maeneo ya Gembensabo, maeneo ya Dohomu kote huko kuna migogoro. Lakini vile vile kuna wawekezaji wa *Breweries* ambao wana mzozo na wakulima wa Vijiji vya Ari na Gembensabo vile vile.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba kwa vile migogoro katika Jimbo la Babati Vijijini ni la muda mrefu na imeshindikana kutatuliwa; nasema imeshindikana kwa sababu ni ya miaka mingi. Mimi nina miaka 10 katika shughuli hii, lakini siku zote tunazungumza habari ya migogoro badala ya wananchi kufanya kazi yao ya kawaida ya uzalishaji, wamebaki katika kuhangaikia migogoro, inapoteza muda kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa niliongelee labda katika hilo, ningeomba sasa kwa sababu inaonyesha kwamba Wilaya, Mkao wote, hawa hawajafanikiwa. Ni vizuri basi hata kikaundwa kikosi fulani au Tume ikachunguza suala zima la ardhi na ninaamini kabisa Wizara ya Ardhi pia inafahamu jambo hili kwa sababu sio mara ya kwanza kulifuatilia. Naomba waendeele kulifuatilia, lakini kufikia ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo ningependa pia nilizungumzie ni suala la miundombinu ya barabara na reli. Katika suala zima la kujenga uchumi, barabara na reli, ni miundombinu ambayo ni muhimu sana kujenga uchumi wa nchi yoyote ile duniani. Niseme tu kwamba barabara na reli ni vitu ambavyo vinasaídiana katika kujenga uchumi siyo kwamba moja ni bora kuliko nyingine na kwamba ukijenga reli basi barabara inakuwa haina kazi, au ukijenga barabara basi reli inakuwa haina kazi, hapana.

Vyote vinahitajika katika uchumi ambao umeendelea, mifano ipo katika nchi zilizoendelea kwamba barabara ni mambo ambayo yanahusiana. Niseme tu kwamba katika hili niipongeze Serikali kwa ujenzi unavyoendelea vizuri katika Wilaya yangu ya Jimbo la Babati Vijijini ambapo katika barabara ya Minjingu-Babati-Singida kazi nzuri inaendelea kwa *speed* kubwa, mkandarasi wa Kichina anafanyakazi nzuri sana. Naipongeza sana Serikali na kuishukuru Serikali. (*Makofi*)

Lakini vile vile ningependa kufahamu nini kinaendelea kuhusu barabara kati ya Babati-Kondoa-Dodoma hadi Iringa. Nimeangalia katika bajeti ya maendeleo ya mwaka huu unaoendelea sawa, tuna shilingi milioni 45 zilitengwa mwaka jana. Sijui zinafanya nini! Maana bado hatujaona nini hasa kinaendelea. Lakini kwa upande wa Dodoma kuelekea Iringa tunafahamu kuna hela zimetengwa, lakini huku kati ya Dodoma na Babati sijafahamu nini hasa kinaendelea.

Ningependa Mheshimiwa Waziri anayehusika, anisaidie kufahamu nini hasa kinaendelea. Lakini kwa upande mwingine kwa barabara za vijijini ambazo pia ni muhimu katika suala zima la kuendeleza Kilimo Kwanza, kuna kazi nzuri zinaendelea katika Wilaya zetu, katika Halmashauri zetu, kazi ya ujenzi na matengenezo ya barabara vijijini. Sasa katika ujenzi huo, kuna suala zima la madaraja makubwa ambayo yanazidi uwezo wa Halmashauri. Nilikuwa napenda kuishauri Serikali kuweka *mechanism* au utaratibu ambao utawezesha pale ambapo Halmashauri inazidiwa kibajeti, basi Serikali Kuu iweze kuingilia kati. Kwa maana hiyo basi, naishauri Serikali Kuu iweze kuwa inafanyakazi pamoja na Halmashauri zetu za Wilaya katika kuhakikisha miundombinu hii ya kule vijijini inafanya kazi vizuri. Maana hiyo itasaidia mazao ya wakulima kufikia soko. Itasaidia vile vile wananchi kwenda kwenye zahanati zetu, wananchi kwenda kwenye maeneo ya elimu na kadhalika. Naomba niunge mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hoja iliyokuwa mbele yetu. Naanza kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa akina mama wa Mkoa wa Kaskazini kwa ushirikiano walionipa katika kipindi changu cha Ubunge wa miaka mitano na upendo mkubwa walionionyesha na naamini tutaendelea kushirikiana na wataendelea kunionyesha upendo huo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Napenda kutoa pongezi kwa Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kutekeleza Ilani yake kwa asilimia kubwa sana. Chama Cha Mapinduzi kikitua ahadi kinatekeleza ahadi hiyo kwa vitendo. Ni imani yangu kwamba Watanzania wameona jitihada hizo na watatumia busara zao kwa kipindi kijacho ambacho tutakuwa na uchaguzi mwezi wa Oktoba, kukirudisha tena Chama Cha Mapinduzi madarakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Wizara kupitia Waziri wa Fedha na Manaino wake na watendaji wao wote kwa kutuletea bajeti hii ya mwaka 2010/2011, bajeti ambayo imeweka vipaumbele ambavyo vimewagusa wananchi wote na zaidi wale wa ngazi ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, demokrasia ni gharama, kwa hiyo, Serikali ni lazima igharamike ili kutekeleza demokrasia kwa manufaa ya wananchi wote. Mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, kwa hiyo, Serikali imetenga fungu kwa ajili ya kutekeleza demokrasia hiyo ya uchaguzi. Ndio maana hata sura ya bajeti ya mwaka huu, hailingani na sura ya bajeti ya miaka minne iliyopita ambayo ilikuwa hakuna uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vingine vilivywewekwa ni elimu. Bajeti ya sekta ya elimu imechukua asilimia 17.62 ya bajeti nzima. Elimu inakuwa Tanzania. Mashule mengi yamejengwa katika ngazi ya Kata, tangu mashule ya awali, ya msingi, sekondari na vyuo vikuu na hata Chuo Kikuu cha Dodoma, ambacho Mheshimiwa Zitto amekitaja kwamba hakimo kwenye Ilani, kwa kuwa hakikutajwa *specifically* kwenye Ilani lakini kama sekta ya elimu, Chuo Kikuu Cha Dodoma kimo na kimejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kuna matatizo mengi katika sekta hii kwa sababu mbali ya shule, kuna matatizo ya walimu. Kuna shule nyingine zina walimu wawili tu, walimu watatu; hakuna maabara za kutosha, hakuna vitabu vya kutosha, kwa hiyo, ni sahihi kabisa kwa Serikali kuweka kipaumbele hiki. Sasa hivi mkakati ni kuboresha elimu ya sayansi, kwa hiyo, maabara ni muhimu na vitabu ni muhimu. Tunaipongeza Serikali kwa hilo. Lakini vile vile tuisihau nyumba za walimu. Walimu wanakwepa kwenda kufundisha katika baadhi ya vijiji kwa sababu hakuna nyumba. Kwa hiyo, Serikali itilie mkazo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imependelewa na Mwenyezi Mungu. Ametupa neema tele, ametupa fursa mbalimbali za kimaumbile na fursa mbalimbali za Kijiografia. Nchi yetu ina ardhi ya kutosha kulima, ina maji ya kutosha ya juu ya ardhi na chini ya ardhi, ina eneo kubwa la bahari ambapo tunaweza tukajenga bandari mbali mbali, pia nchi yetu imezungukwa na nchi ambazo ni *land locked*. Nchi yetu ina kisiwa cha Zanzibar ambacho kikitumika vizuri kinaweza kuwa chanzo kikubwa sana cha kukuza uchumi wetu, kwa mfano tunaweza tukaanzisha bandari huru pale Zanzibar, kwa maana ya *free port*. Lakini vile vile nimetaja haya kuunganisha na kipaumbele cha miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yote niliyoyataja hayawezi yakatunufaisha kama hatukujenga au kuboresha miundombinu tuliyonayo. Tunazungumzia bahari. Kama hatukujenga bandari zetu kwa hali ya juu tukazifanya zile nchi zinazotuzunguka kutumia hizo bandari zetu, kwa hiyo, ile bahari inakuwa kama kitu cha kwenda kujifurahisha tu na kuangalia samaki wanavyotembea mle na wala isitunufaishe chochote. Lakini vile vile kama hatukuwa na barabara zinazounganisha bandari hizo mpaka kwenye zile nchi, hatutapata manufaa ya maumbile ya nchi yetu. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kuwa miundombinu bado ni kipaumbele kilichowekwa. Kwa hiyo, tuiendeleze miundombinu yetu, tutumie fursa za kimaumbile tulizopewa na Mungu, tupate manufaa ya kiuchumi na ya kijamii ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, afya ni kipaumbele namba tatu, kimechukua asilimia 10.4 ya bajeti. Tunajua tuna matatizo ya watalaamu wa afya, kwa hiyo Serikali iendelee kuwafundisha wataalam hawa wa afya ili tuwe na madaktari wa kutosha. Daktari mmoja

kuhudumia wananchi 20,000 hawezi kuwahudumia ipasavyo kwa idadi hiyo. Kwa hiyo, tuweke kipaumbele cha kufundisha madaktari wetu. Lakini nyumba za madaktari ziendelee kujengwa ili nao wanapopelekwa mahali wabakie huko na kutibu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia Kilimo Kwanza. Azimio la Maputo limesema tuweke angalau asilimia 10 ya bajeti yetu, lakini bajeti yetu ya mwaka huu ni asilimia 7.78 tu, bado tuko mbali. Malengo ya Kilimo Kwanza yamewekwa pale. Tunahitaji fedha za kutosha, tunahitaji fedha nyingi kwa ajili ya umwagiliaji, tunahitaji fedha nyingi kwa kutafuta mbegu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti, utafiti ulikuwa lengo ni kutenga asilimia moja ya bajeti yetu kwenda kwenye utafiti, lakini bahati mbaya takwimu zinaonesha ni asilimia 0.0026 ya bajeti ndio imekwenda kwenye utafiti na tunasema utafiti ni moja ya *factor* ya maeendeleo. Sasa hivi dunia imebadilika, watu wanafanya tafiti mbalimbali. Kuna tafiti za mambo ya *Biotechnology*, kuna mambo ya *GMO*, yanafanyiwa utafiti, kwa hiyo, sisi tunahitaji fungu kubwa la fedha katika kufanya tafiti ili tuendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi mmoja wa *WEMA*, wanasesma *Water Efficiency Maize for Africa*. Labda Mheshimiwa Waziri wa Kilimo akija hapa atueleze, huu mradi malengo yake ni nini? Na manufaa yake ni nini? Na mara hii imetengewa kiasi gani? Kwa sababu, kwa mimi ninaona hawa watafiti wanafanya kazi nzuri na ni lazima wapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwezeshaji wa wananchi na hasa akinamama, tunapoongeza hii mifuko yetu tuliyonayo. Mfuko wa *JK, AK*, lakini na Mfuko wa *SELF* lakini haujawafikia walengwa, hasa wale walengwa wa mfuko huu, akina mama wale wa kipato cha chini, hawajafikiwa, kwa hiyo, taratibu ziangaliwe. Kwanza mfuko uongezewewe fedha halafu taratibu ziangaliwe upya ili kuhakikisha wale walengwa hasa wanafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa nizungumzie kuhusu mapato. Ukiangalia *tax effort* kwa maana ya kodi kwenye *GDP*, halafu ukiangalia matumizi ya ndani kwenye *GDP*, utaona ile *gap* iliyopo na ndio maana hata ile sura ya bajeti inaonesha pale kuna *deficit* hata katika matumizi ya kawaida, inabidi tutumie mkopo. La msingi ni kupanua vianzio vya mapato, kupanua wigo.

Tulikuwa na semina ya Vitambulisho vya Mtanzania, pale wamesema vile vitambulisho tu vikiweza kutolewa tunaweza tukapata fedha karibu trilioni tatu za kodi kwa maana kila mmoja atajulikana anaishi wapi, anafanya shughuli zipi na kwa hiyo, walipa kodi wanaweza wakaongezeka kwa njia hiyo kuliko hali ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ninaipongeza Serikali kwa ukusanyaji mzuri wa mapato. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kupata nafasi hii kutoa mchango wangu mfupi katika bajeti hii

tunayokwenda nayo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake pamoja na wataalamu wote kwa kutuletea bajeti hii ambayo tutasema ni bajeti ya lala salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba Dola ina mihimili mitatu, tuna Serikali, tuna Bunge na tuna muhimili mwengine ambao ni Mahakama. Sasa baada ya kuona Bunge mambo yanakwenda kidogo kombo, tukafanya utaratibu tukapata mgawo wetu; ikawa Bunge halitegemei tena kupewa mafao yake kutokana na fungu la Waziri Mkuu moja kwa moja. Sasa mara nyingi ilikuwa linazungumzwa suala hili la Mahakama na mwenzangu mmoja amezungumza kwamba nao muhimili huu ni lazima utazamwe kwa jicho la aina yake kwa sababu nao ni mmoja kati ya mihimili ya dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hali hiyo mimi ninataka nizungumze suala hili la mhimili huu ndani ya Wizara nzima ya Sheria na Katiba, kwa vile ni muhimili au ni Wizara ambayo inashughulikia kiujumla utoaji wa haki. Sasa nazungumzia Wizara hii kutokana na huu umuhimu wenyewe wa dola uliopo.

Kutokana na kwamba mhimili huu bado haujapatiwa mfuko wake binafsi, nilitegemea Wizara au Serikali kupitia kwenye Wizara yake ya Fedha, itafanya utaratibu mzuri kiasi ambacho hii Wizara nzima ya Sheria na Katiba iweze kupata fungu ambalo litaiwezesha kufanya kazi yake na ile haki ambayo inategemewa ipatikane kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, naomba nilizungumze hilo kwanza. Sasa badala ya kwamba Wizara ya Fedha iitizame Wizara hii kwa jicho ambalo litakuwa ni zuri zaidi, mambo yamekuwa ni kinyume. Kwa mfano, katika Wizara nzima hii ya Katiba na Sheria, bajeti yake ni shilingi bilioni 117.9 Wizara ambayo ina mafungu 11, likiwemo hili la mhimili mzima wa Mahakama. Lina mafungu ya Haki za Binadamu, Tume za Kurekebisha Sheria na Mafungu engine. Sasa katika kufanya mahesabu yangu mafupi tu, nimejaribu kutazama baadhi ya Mikoa na nina orodha ya Mikoa kama 11, bajeti ya kila Mkoo ni zaidi kuliko bajeti nzima ya Wizara nzima ya Sheria. Jambo ambalo ni kweli kwamba, hata Mkoo uwe ni mkubwa kiasi gani ni dhahiri kwamba na hizi shughuli za kutoa haki kiujumla ni lazima nazo zitakuwa ni kubwa. Sasa ni jambo la kushangaza katika hali hiyo na sijui Wizara ya Fedha ililitizama vipi suala hili; kwa mfano kuna mko wa Tanga una shilingi bilioni 148.2, Kagera shilingi bilioni 135, Dar-es-Salaam shilingi bilioni 145, Dodoma shilingi bilioni 127, karibu mikoa 11.

Mheshimiwa Naqibu Spika, sasa katika hali kama hiyo, ile haki tunayoitegemea kwamba Mahakama zetu hazitoi haki; kwanza tukubali kwamba Majaji na Mahakimu wameboreshewa maslahi yao, lakini kuboreshewa huko ni lazima waboreshewe na mazingira yao ya kufanya kazi. Nimetembelea karibu sehemu nyingi sana, Mahakama hazifai, haziridhishi. Mahakima za Wilaya zina upungufu wa zaidi ya Mahakimu wa Wilaya 300. Mahakama za Mwanzo zina upungufu wa Mahakimu zaidi ya 1,000, wakati huo huo tunataka kutengenisha *State Attorneys*, wawe wanashughulikia kesi na bado wana upungufu mkubwa wa watu hawa ambao watayashughulikia mambo hayo.

Sasa katika hali kama hiyo, ile haki ambayo tunaitegemea itolewe itakuwa iko mbali sana. Sasa nafikiri Wizara ya Fedha watatuambia wanalitizama vipi suala hili katika kuhakikisha huu mhimili wa tatu ambao umo ndani ya hii Katiba na Sheria nao unapata nafuu na ile haki tunayoitegemea iweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Zanzibar, juzi walisoma bajeti yao na mionganoni mwa kilio chao kikubwa kilikuwa ni mgawo wa asilimia 4.5 kwamba bado ni mdogo na hautoshelezi. Sasa vile vile mwenzangu ameshazungumza kwamba kwa kweli mchakato huu umekuwa ni wa muda mrefu na hatujui umefikia wapi. Sasa wenzetu wanadai wapewe mgawo zaidi ya huu uliopo, sasa kwa vile inachukua muda mrefu kwa ule msemo wa watu wa sheria, inaelekea *justice delayed is a justice denied*. Sasa ikiwa hali ni hiyo, ni vipi tunawafikiria wenzetu wa Zanzibar? Wao tayari wameshaliona hili suala, kwamba jamani hili suala la asilimia 4.5 kwetu sisi bado ni dogo na ni lazima lifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusilidharau hili suala. Mimi ninashauri hatua za haraka sana zifanyike kuhakikisha suala hili linamalizwa. Bila ya hivyo, wakati wenzetu wameshaanza kuliona zaidi, huenda pengine likaleta athari kubwa mno. Sasa ni vizuri tulipatilize kabla hali haijawa mbaya zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha bajeti cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 44, hapa amezungumza kwamba kuanzia mwaka 2010/2011 Halmashauri zitatakiwa kuonesha bakaa katika akaunti ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha na zijumuishwe kwenye bajeti ya mwaka unaofuata. Hii ni kwamba sasa hivi, tunavyoelekea Serikali Kuu ile bakaa au zile fedha ambazo huwa zinabaki, zinaingia katika mfuko wa Serikali.

Lakini pia nafikiri ni vizuri, pamoja na kuingia kwenye mfuko wa Serikali kwa ajili ya kufanya ile *transparency* kwenye jedwali hili ambalo siku zote linaonesha yale mapato na matumizi ni vizuri sana ile bakaa nayo ioneshwe humu ili tujue kwamba kwa wakati huu au mwaka huu, Serikali imesaliwa na kiasi fulani cha fedha. Ina maana Halmashauri kwa muda mrefu, suala hili walilifumbia macho na ni kweli kwamba kwenye Halmashauri kuna fedha nyingi sana zinazopelekwa tena wakati mzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tulipata taarifa kwamba kama fedha za maendeleo ya miradi ya maji, pengine zinapelekwa mwezi wa tano au wa sita, sasa tunategemea Halmashauri ifanye miujiza gani kuhakikisha kwamba imemaliza kutumia fedha zile kwa wakati? Kinachofanyika ni ubadhirifu na madudu mengi yanayoendelea.

Lakini sasa fedha kama zile ikiwa hakuna tena uwezekano wa kuzitumia ndani ya kipindi kile, ni vizuri ziwekwe na zije zitumike katika kipindi cha bajeti kinachofuata. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali itoe uamuzi huo na vilevile ni vizuri na ninashauri kwamba ile bakaa itakayotokea kwa Halmashauri na Serikali vilevile ioneshwe katika kitabu chetu cha bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la wafanyakazi wa *TRA*, wale wameagizwa kila anayekusanya makusanyo makubwa anapata asilimia tano. Sasa kinachojitokeza ni kutaka mtu akusanye mapato makubwa na matokeo yake ni kuwakandamiza wale wanaotoa kodi. Sasa kwa hili, naomba sana Wizara ilitizame tena kwa makini ili kuhakikisha kwamba hao watoa kodi wasichoke au wasibanwe sana na wafanyakazi wa *TRA*. (*Makofi*)

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie katika hotuba hii ya bajeti. Awali ya yote, ninataka kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Rufiji kwanza kwa kunichagua.

Pili, kwa kushirikiana na mimi kufanyanao kazi pamoja na hata kufikia sasa tuna mpango wa kupiga kura, nadhani hawatanisau.

Pili nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake na Katibu Mkuu na Manaibu wake wawili na watumishi wote wa Wizara hiyo kwa kuleta Bajeti hii katika wakati huu mzuri kabisa katika maendeleo ya nchi yetu hasa kwa vile tumejitishwa mzigo wa Uchaguzi Mkuu, tumejitishwa mzigo wa vitambulisho na vilevile hapo wameweza kufikiria mambo muhimu hasa uanzishwaji rasmi wa Benki ya Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri iliyofanya katika jimbo langu, hakika katika mwaka 2006 Mheshimiwa Rais alitembelea jimbo lile na akajionea mwenyewe na kwa kweli alitamka na Serikali imetimiza. Kwa mfano barabara zote kubwa kwa mfano ya Kibiti, Mkogo, Utete, Nyamwagi pamoja na kivuko cha Utete sasa inapitika wakati wote na hicho kivuko ilikuwa ahadi ya Rais, nafahamishwa kwamba tayari kivuko hicho kimeshafika Dar es Salaam bado kupelekwa Rufiji na gati pale Utete limeanza kujengwa. (*Makofi*)

Pili, iko barabara inayotoka Ikwiriri mpaka Mkogo mpaka Mloka mpaka Vikumbulu mpaka Kisarawe barabara hii zamani iliachiwa Halmashauri yetu. Halmashauri kwa kawaida ina ubavu mdogo lakini Mheshimiwa aliamuru kwamba barabara hii kwa ajili ya faida kubwa ya kufungua Selous yaani baada ya daraja la Mto Ruvuma kufunguliwa watalii waweze kufika Selous kwa kuititia Ikwiriri, Mkogo, Mloka, Selous na jambo hili litapanua biashara litapanua uchumi wa Rufiji na uchumi wa Taifa lote. (*Makofi*)

Tatu ni kwamba Halmashauri Wilaya na *RCC* ya mkoa baada ya kutazama vizuri hali ya barabara ya Utete Nyamwale iliamua kuiomba Serikali kwamba barabara hii sasa iwekewe lami na sisi tunaona umuhimu wa barabara hii ni kwamba kama unaenda Kusini ukipita Ikwiriri, daraja la Mkapa, barabara hiyo inayoongoza Kusini lakini ikitokea hatari wakati wowote katika daraja lile barabara ambayo inaweza kufanya kazi hiyo barabara mbadala ni barabara Kibiti, Utete Nyamwage kwa hiyo, hapa tunaiomba Wizara ya Miundombinu suala hili liko mezani kwao kwamba barabara ya Utete Nyamwage sasa ifikiriwe kwa dhati kabisa kuwekewa lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija katika huduma za maji, Serikali na namtazama hapa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya alifika Rufiji kuangalia mwenyewe kwa macho yake maendeleo yaliyoletwa na Wizara yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunazungumzia maji vijiji vya Rufiji tumefikia asilimia 80 na katika miji mikubwa, miji midogo ya Wilaya, Wilaya ya Rufiji tukianza na Makao Makuu ya Wilaya tuna miradi mikubwa ya maji ya bomba na inaendelea vizuri na ile ya Utete inatazamiwa kufunguliwa labda tarehe 19 Juni, 2010 na mwenyewe Mheshimiwa Rais wa nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza vilevile kujenga miundombinu ya maji na inaendelea katika mji wa Ukwiriri na vilevile hata mji wa Kibiti katika jimbo la mwenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za umeme tunashukuru Serikali kwa sababu sasa hivi Ikwiriri imeanza kupata umeme tangu miaka ya 1970 lakini mji mkubwa wa Utete, Mji Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Utete imeahidiwa kupata umeme na mambo yanaendelea vizuri na kwamba Utete itapata umeme mwezi Juni kwa kupata taratibu kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini na hata Waziri wenyewe na kwamba vijiji vya Mhulo, vijiji vya Nyamwage, vijiji vya Kigwiki na Utete vyenyewe vitapata umeme kwa wakati mmoja kutoka umeme wa *SONGAS*. Tumeahidiwa vilevile kwamba kijiji cha Uchumbi na kijiji cha Utonge na Mloka vitapata umeme baada ya kupata vijiji hivyo vya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya afya Serikali ya Wilaya na Serikali Kuu imekarabati vituo vya afya vyote katika jimbo langu na vilevile wamewekewa vyombo vipyta na kwamba hospitali ya Utete imepata ukarabati mkubwa na imepata wodi ya akina mama pamoja na *theatre* mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa mpaka leo tukitembelea jimbo ni kwamba kuna upungufu mkubwa wa dawa na vilevile kuna upungufu mkubwa wa watumishi, naomba Serikali ijitahidi sana katika mambo haya mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu ni muhimu na katika jimbo langu kata zote zinazo shule za sekondari, tunashukuru lakini kwa bahati mbaya bado hatujafungua *high school*, kwa hiyo, tunaomba Serikali ilipobakiza hapa iweze kumalizia. Tatizo kubwa katika elimu popote katika jimbo ni upungufu mkubwa wa walimu na vilevile sekondari hizi hazina maabara na hazina vyombo vya maabara na vilevile zinahitaji hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakuja katika suala la kilimo, kilimo kwanza *alhamdullah* imeonekana katika Bajeti kwa asilimia 35 na tunampa hongera sana Waziri Mheshimiwa Mustafa Mkulo, lakini bado haitoshi. Kwa sababu tunapozungumzia kilimo tuna maana kwamba kupanua kilimo chenyewe kwa maana ya *mechanized agriculture*. Utaona fedha zilizotengwa kwa ajili ya *mechanization of agriculture* ni kidogo sana ni kwamba kwa mfano hapa katika mwaka wa 2008 ilipangwa shilingi bilioni 1.4 lakini

mwaka huu imepangwa shilingi milioni 600 karibu nusu ya zilizopangwa miaka miwili iliyopita na watu bado wanahitaji matrekta, wanahitaji *power tillers* na pembejeo zingine. (*Makofi*)

Halafu ningependa kabisa kumshukuru Waziri wa Kilimo na Chakula ameitungia jicho Lubada, sasa Lubada nataka nieleze na mimi ni mjumbe wa bodi ya Lubada. Lubada ina mipango mizuri na ikipata fedha za kutosha tunaweza kabisa kuonyesha tofauti ya Lubada iliyopita na Lubada ya sasa. Na suala kubwa ninalotaka kumsifu Mheshimiwa Waziri ni hilo, tumepeata shamba la mbegu...

NAIBU SPIKA: Ahsante Mkurugenzi wa Lubada. (*Makofi*)

MHE. PROF. IDRISA A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nataka kuanza kuzungumzia hii Bajeti kwa kusema kila Mheshimiwa Mbunge ambaye yuko katika Bunge hili ambalo tunamalizia sasa anapaswa kujipongeza, kusema kweli tumekuwa na Bunge zuri na tunamaliza vizuri hatujapigana ngumi na tumeweza kuangalia mambo mengi ambayo yamekuwa changamoto na tumendelea katika kuwasaidia wananchi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, fikisha salamu kwa Mheshimiwa Spika kwamba amekuwa na Bunge lililokaribia *top standards* hiyo ndiyo mimi ningependa kila mmoja aondoke hapa anajivuna kwamba amekuwa Mbunge mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kuna changamoto, sisi tumejenga msingi katika Bunge hili la Ishirini kwa ajili ya Bunge ambalo linalofuata na mimi nategemea wengi wetu tutakuwa humu pamoja na mimi Waheshimiwa kwa hiyo, tunajenga hiyo misingi lakini bado tuna changamoto lukuki. Changamoto yetu ya kwanza kubwa ni namna ya kuwasaidia wakulima wetu, bado hatujapata namna ya kuwasaidia wakulima ilivyo sawasawa. Kweli *speech* imezungumza, imesema kwamba zaidi ya watu 73 ndiyo wanategemea kilimo ni kweli kabisa, lakini bado uhuru wa mkulima. Mkulima bado ameshikiliwa mno na Serikali yake aliyochagua, Serikali inaanua auze wapi mahindi yake au asiuze kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapofanya hivyo ungekuwa unampelekea na *cheque* kwamba badala ya kuuza Msumbiji au Lusaka ukae na mahindi hapa Sumbawanga basi chukua hii *cheque* ili mwaka kesho uweze kuendelea kulima, hatujafika hapo. Sisi tunajua amri moja tu hatutaki chakula kitoke nje basi kama nitaingia hasara sitaingia hasara hilo ni shauri langu. Kwa hiyo, hali hiyo hatujaweza kusaidia kilimo hata kidogo na ndiyo maana kilimo hiki hakikui, lazima uwe mwendawazimu kwenda kuweka fedha yako kwenye chakula ambapo huna hakika kikiiva utakipeleka wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ambayo bado hatujaiweza ni mambo ya pembejeo, pembejeo tunashukuru kwamba Bajeti inaongezeka na imeonekana

hana lakini ukweli ni kwamba namna pembejeo zetu zinavyogawanywa kwa wakulima bado hatujaweza kabisa ni wizi mtupu. Juzi hapa sisi kule Kanda ya Ziwa tumepewa vocha ya mbegu, watu wameiba, watu wameandika majina Maduhu Masanja na anaweka mtu mmoja na hakuna Serikali iliyo na uwezo wa kukamata mtu yejote, mimi naona baadhi ya watumishi wa Serikali ni washiriki kabisa katika mchezo huo.

Kwa hiyo, Serikali inatoa fedha upande huu wengine wanazichukua wanaweka mfukoni mwao, bado Mheshimiwa najua rafiki yangu ananisikiliza pale weka utaratibu ulio mzuri, pembejeo iwafikie kweli wakulima kama ni kwa nusu bei sio mwingine anapata kwa shilingi mia tano kwa viua, wadudu wa pamba na wengi 1500, wengi 4500 ni fujo tu kwa hiyo hatujaweza ku-*manage*. Kwa hiyo, natumaini kwamba Bunge linalokuja na Serikali inayokuja itakuwa inahakikisha kwamba tunaangalia haya mambo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine imeonekana wapi kabisa kuwa tuna changamoto kubwa sana ya tabia nchi zamani tulikuwa tunajua tulime wakati gani, tulikuwa tunajua mvua itakuja mwezi gani, leo hii hatujui. Kwa hiyo, ndiyo kusema kwamba uwekezaji wetu katika kilimo ni lazima uhusishe sana uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, tuweke fedha nyingi kwa ajili ya miundombinu na Mwenyezi Mungu katupa kila kitu, katupa Mito kibao maji yetu yanaishia baharini tu, yanaishia *Lake Victoria* tuweke kilimo cha kumwagilia, hiyo ndiyo itaweza kutusaidia kuweza kupambana na changamoto ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine kwenye *activity* wazungu wanasesma miundombinu ya barabara hii ni muhimu sana kwa mkulima na zaidi barabara ya vijijini, mimi kule nafurahi kusema kweli nimepata bahati na bwawa langu la Simiwi liko sawasawa linaendelea kujengwa, natumaini mwaka unaokuja nitapata Gamaroa, nitapata Ukiwamizi, ni mambo lakini bado nasisitiza tuwekeze fedha nyingi sana kwa upande wa barabara. Lakini hili sasa nataka kuliunganisha na jambo ambalo Mheshimiwa Waziri amezungumza ambalo liko kwenye *page 44* linasema juu ya fedha zinazobaki kwenye Halmashauri kama hizi fedha zitaendelea kupokelewa karibu na mwisho wa mwaka halafu ni za barabara na ukijua kwamba ukipeleka pesa Disemba kuna mvua mpaka Machi hatutajenga barabara kama hizi fedha zitarudishwa.

Kwa hiyo, nataka katika ufanuzi wako je, zitarudishwa au watabakia nazo kwa sababu ni muhimu kama watazirudisha waziombe tena ndiyo kusema kwamba hatutajenga barabara vijijini. Lakini kwa upande wangu kitu chochote kinachowenza kufanya kuikutanisha nchi hii kwa barabara kwa reli na njia zingine tuwekeze katika barabara, tuwekeze katika miundombinu hiyo itasaidia sana watu ambao ni wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni utegemezi, Mheshimiwa Waziri mimi unajua mawazo yangu kweli hatuwezi kuendelea kuwa nchi ambayo ni namba tano karibu tunaambiwa kwamba itakuwa namba tano *as a nuclear country*, nchi ambayo ina *uranium* ni namba tatu ya kuweza kupata dhahabu na bado tegemezi na utegemezi huu ni umechukua sura tofauti, zamani misaada ilikuwa kama neno lenyewe kama linavyosema misaada lakini sasa misaada tunayopata kwa wafadhili nawashukuru wanatusaidia sana siku hizi kizungu inaitwa ni *control*, ni utawala wanataka kukuambia

utengeneze sheria gani, wanataka kukuambia ufika hapa wapi na kama ningekuwa na wakati mkubwa ningeweza kukuonyesha hapa katika Bajeti hii *general budget support* kuna mambo lukuki ambayo Serikali imekubaliana na wafadhili ambapo mambo mengine hayakubaliki kabisa kama yangewekwa mbele ya Bunge lako Tukufu hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wao wameshaweka mkono, wameshaanguka hapo, Serikali ya Tanzania itafanya hivi, mimi ninaona kuna haja ya Serikali kutengeneza utaratibu kabla hawajawekeana sahihi na wafadhili hawa kwa vitu ambavyo vinaingilia hata uwezo wa Bunge lako Tukufu kwamba kwanza iangaliwe na Kamati ya Bunge ili kweli yale yanayokubaliwa basi yawe ni mambo ambayo angalau yanaweza kukubaliwa kidogo kidogo na Bunge lako Tukufu hapa.

Bado tuna matatizo sana katika utegemezi, utegemezi huu tungeweza kuondokana nao kwa kuweza kukokotoa kodi kwa mambo ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu kama vile madini lakini juzi hapa tumepitisha Sheria mpya ya Madini, tulichosema kwamba tunataka asilimia nne ya mrahaba upande lakini hapo hapo tukaongeza lakini sio kwa viwanda vilivyoko kwa sasa hivi ni vile vitakavyokuja baadaye, vitakuja lini Mheshimiwa Mkulo? Mbona sehemu zote duniani tunakwenda ona? Tumekwenda Australia watu wameondokana na mambo ya *MDA*, kwa nini sisi bado tunaendelea na utaratibu huu na kila wakati unasikia katika magazeti, katika vyombo vya habari kuwa Waziri wa Madini sijui nini amekubaliana mkataba mwingine na *MDA*, sijui *uranium* sijui ya kitu gani wewe kama Waziri wa Fedha wa kututafutia fedha za kuondoka na utegemezi unapata kitu gani hii ni sehemu ambayo lazima tuiangalie ni changamoto ambayo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu haya ma-*MDA* yanaanza kuwa ni sheria mama hata mikataba hii inakuwa ni zaidi ya sheria ya nchi hii. Bunge hili limenyan'anywa madaraka, Bunge hili haliwezi kutunga kodi kutoka Bulyanhulu limenyan'anywa, tutakulia namna gani kwamba Bunge linyang'anywe tu na *agreement* ambayo ni mbaya na watu wamejifungia mahali wanaweka sahihi na hatujui kwa mazingira ya namna gani halafu Bunge lako unakubali linanyang'anywa madaraka hata ya kukokotoa kodi, hali hii lazima tuifikishe mahali ambapo tunasema haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine nitaisema kwa haraka ni pia Bajeti lazima ifuate sheria. Tumetunga hapa Sheria kwa mfano sheria moja ya kumsaidia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa John M. Cheyo.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nitaandika!
(*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na sasa nitamuita Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Manju S. Msambya, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa ndiyo watakaopata nafasi jioni hii.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nitoe rambirambi zangu kwa Mama Zabibu Rubea wa Masuguru aliyeuawa na tembo tarehe 7 Juni, 2010. Alikuwa anakwenda kuchota maji akakumbana na dhahama hii ya kukanyagwa na tembo. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amin!

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Mheshimiwa Profesa Mark Mwandomsyia kwa kuendeleza hii rambirambi utapeleka huduma ya maji pale kijiji Masuguru. (*Makofi*)

Vilevile naomba nitoe rambirambi kwa wananchi wa Mwangaka waliopata ajali katika gari walilokuwa wakisafiria kwenda Masasi na kupata majeruhi wengi. Naomba Mwenyezi Mungu awanusuru majeruhi hawa waweze kupona haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba fursa hii pia kuwashukuru wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu ambao walini pigia kura mwaka 2005 na kupata ushindi. Nimekuwa nao karibu kwa muda wote wa miaka mitano iliyopita na nadhani tumefanya kazi vizuri katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na hapana shaka yoyote watanipa ridhaa nyingine ya miaka mitano ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nipongeze Wizara hii ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, pamoja na Manaibu Waziri wote na watendaji wote kwa kutengeneza Bajeti nzuri ambayo inawajali sana wazee kwenye majumba yao kwa kuondoa au kupunguza kodi ya majengo, mzigo walio nao wale wazee ambao hawajiwezi kabisa na vilevile Bajeti hii imekuwa ni kwa ajili ya kilimo na mifugo ambayo imepata unaifuu kwenye misamaha mbalimbali. Nasema hongera sana Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa Bajeti nzuri kama hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nanyumbu ni Wilaya mojawapo ambayo iko pembezoni mwa nchi, ni Wilaya ambayo kiwango cha umaskini ni kikubwa sana kwa hiyo, tunachoomba watu wa Wilaya ya Nanyumbu ni kwamba tunaomba uwiano mzuri au uwiano sawa wa maendeleo kwamba wakati wenzetu wanatembea sisi tuwe tunakimbia. Kwa kweli hali ni duni sana, wananchi wanaishi maisha ya taabu kwa sababu tu Wilaya ya Nanyumbu utakumbuka ilikuwa ni uwanja wa mapambano wakati wa vita vya ukombozi na sasa ndiyo tunaanza kujinasua angalau kuganga yale madonda ambayo tuliyapata wakati ule wa ukombozi.

Kwa hiyo, naomba Serikali itupie jicho Wilaya ya Nanyumbu hasa kutokana na hali ile ya umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipate majibu kutoka kwa Waziri hususani kutokana na mambo yafuatayo, la kwanza, kwanza niipongeze Serikali kwa kutujengea Daraja la Umoja pale Mtambaswala, daraja ambalo linaunganisha Tanzania na Msumbiji. Lakini naomba Mheshimiwa Waziri anijibu miundombinu kama ya ofisi za

mapato, benki kwa sababu ni huduma muhimu pale mpakani, naomba aniambie au awaambie watu wa Nanyumbu ni lini huduma hizo zitaanza pale mpakani Mtambaswala?

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo naomba nifahamu kwa sababu Wilaya yetu ya Nanyumbu haina benki, haina ofisi ya mapato, wananchi wanaumbuka kwenda mpaka Masasi umbali wa kilomita takribani 56 au 60 wanalipia nauli kubwa kwa hiyo, naomba atuhakikishie ni lini tutajengewa ofisi ya mapato pale Mangaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nanyumbu kama nilivyosema inakosa miundombinu mingi sana kwa mfano afya, afya ni tatizo kwani tuna vituo vya afya vitatu wilayani Nanyumbu na zahanati ambazo ziko kati ya 14 au 15. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itusaidie na ituwezeshe ili tuweze kupata huduma nyingi zaidi za vituo vya afya na zahanati. Akina mama wajawazito na watoto wadogo wanapata taabu sana kufuata huduma za afya mbali na kwenda kule wanaambiwa hakuna dawa warudi, kwa hiyo, inakuwa ni matatizo makubwa na vilevile kuna uhaba mkubwa wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kilimo Kwanza, kwa kweli watu wa Nanyumbu walitikia vizuri sana dhana hii ya Kilimo Kwanza, lakini tumeangushwa na hali ya hewa kuwa mbaya kwani wananchi walijitahidi sana kulima. Nashukuru kwamba Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu Mheshimiwa Fatma alibuni mbinu mpya ya kuwashimiza wananchi kulima zao la choroko, kwa kweli zao hili limewasaidia sana wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu kwa sababu bei ilikuwa nzuri na wengi walijitokeza sana kulima zao hilo la choroko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo tunaona kwamba vifaa kama matrekta bei yake ni kubwa sana kwani mkulima wa kawaida hawezi kumudu kununua, hivyo tunaomba vitu hivi vipunguzwe bei. Vilevile pembejeo za korosho zile ambazo hazipati ruzuku tunaona kwamba bei yake ni kubwa ambayo mkulima hawezi kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji nimeshasema kwamba ni tatizo kama ulivyoona mwenzetu mmoja amepoteza maisha wakati akitafuta maji, lakini naiomba Serikali yale maji ya Mto Ruvuma yanapotea bure tu, yanapotea bure kutoka huko yanakotoka yanaishia baharini. Naomba Serikali kuitia Wizara inayohusika haiwezi kuona kwamba kuna umuhimu wa kuweka mradi mkubwa wa maji kama ule wa Mwanza ukasaidia siyo watu wa Nanyumbu tu lakini hata watu wa Wilaya nyine kama Masasi, Mtwara na kadhalika kuliko kuyaacha maji yakawa yanapotea tu bure. Kwa kweli tunaomba Serikali itupie jambo hilo macho kwa kuona kwamba inaweza kutatua shida ya maji pale mkoani Mtwara kwa ujumla.

Kuhusu elimu, wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu walijitahidi sana kujenga shule za Kata lakini tatizo ndiyo hilo hilo tuna matatizo ya uhaba wa walimu, vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, maabara na hosteli za wanafunzi, pamoja na matundu ya vyoo. Tunaomba basi Bajeti hii isiangalie upande mmoja tu na sisi watu wa Wilaya ya Nanyumbu tunaomba tuonewe angalau huruma kidogo ili tuweze kupata miundombinu hii kuboresha elimu. Tatizo la mimba limekuwa kubwa kwa sababu ya ukosefu wa hosteli

za wasichana, kwa kweli tunaomba sana Wizara ya Elimu itupie jicho Wilaya ya Nanyumbu. (*Makofi*)

Kuhusu miundombinu naipongeza sana Serikali kwa kutujengea barabara kutoka Masasi mpaka Mangaka kwa kiwango cha lami, nadhani kufikia mwakani barabara hii itakuwa imekamilika. Lakini vilevile naiomba Wizara husika basi itueleze kama ujenzi wa barabara kutoka Mangaka ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji*)

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na ameshaunga mkono, sasa nitamuita Mheshimiwa Manju S. Msambya na kama hayupo nitamuita Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, wamekwenda uangalia mchezo wa Afrika Kusini na Mexico wameshindana moja kwa moja kwa taarifa yenu yaani wametoka *draw* moja kwa moja.

Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa!

MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia mjadala huu wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa 2010/2011. (*Makofi*)

Kwanza naomba niwashukuru wapiga kura wangu na wananchi wangu wa jimbo la Ulanga Magharibi kwa imani na ushirikiano ambao wamenipa katika kipindi hiki cha miaka mitano kilichopita na mimi vilevile natarajia kwamba ushirikiano huu utaendelea katika miaka mitano inayokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nimpongeze Waziri Mheshimiwa Mustafa Mkulo na watendaji wake kwa kazi nzuri waliyoifanya kwanza ya kuandaa Bajeti lakini pili kuiwaisilisha hapa Bungeni na wameiwasilisha vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa kweli nimevutiwa sana na Bajeti ya Serikali kwa maana ya kwamba sisi katika kipindi hiki cha mwaka 2009 tumepitia kipindi kigumu sana kiuchumi, lakini pamoja na haya Serikali imepanga kupata mapato ya shilingi trilioni sita, hicho si kitu kidogo, ni kitu kizuri. (*Makofi*)

Lakini la pili, mimi sipati tatizo kubwa sana la kupata misaada kutoka nje, kwa sababu suala la misaada kutoka nje siyo la sisi tumeanza, historia ya kiuchumi inaonyesha hata Wajerumani walipata msaada mkubwa sana baada ya vita kuu ya pili kutoka kwa Wamarekani. Hivi juzi tu kwa mfano Ireland imepata msaada mkubwa sana kutoka *European Union* licha ya nchi ya Ugiriki ambayo inapata matatizo ya kiuchumi na Serikali za Umoja wa Ulaya zinailsaidia. (*Makofi*)

Kwa hiyo, suala la kusaidiana katika nchi siyo tatizo, mimi naona tatizo ni unapeleka wapi zile fedha unazozipata. Unajenga nguvu ili ujitegemee baadaye au

unazitumia hovyo, sasa hili la kutumia hovyo ndiyo suala tunaweza tukalizungumza lakini siyo la kupata misaada wala suala la utegemezi, mimi pia halinipi shida kwa sababu Tanzania sisi tuna historia Wajerumani mwaka 1960 walitutisha tisha, tukawaambia ondokeni na misaada yenu ondokeni nayo, baada ya pale wakawa na nidhamu. Wakati wa Mwalimu Nyerere *IMF* na *World Bank* walitutisha hapa tukasema mkitutisha ondokeni na misaada yenu. Kwa hiyo, nchi yetu ina sifa ya kujitegemea na kuwa na msimamo thabiti kama mtu anatukera tunamkatalia pamoja na pesa zake. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi sina tatizo hilo lakini mimi tatizo langu ni la matumizi ya fedha hizo zinakwenda wapi na sasa hivi mimi naona tunafanya vizuri kwa sababu hata watu wangesemaje, kuna rafiki yangu mmoja anasema hapa ni katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma hakikuwepo katika Ilani ya Chama chetu, siyo kweli kwa sababu katika Ilani kuna mambo tunazungumza matatu kuhusu elimu. Tunazungumza juu ya kupanua na kuboresha elimu ya msingi, tunazungumza juu ya kupanua na kuboresha elimu ya sekondari lakini vilevile tunazungumza juu ya kupanua na kuboresha elimu ya juu. Sasa ni mkakati tu, unaweza kusema tujenge Chuo Kikuu kingine Dodoma, unaweza kusema kijengwe chuo kingine Arusha au Kigoma lakini sisi tumeamua tujenge Dodoma. Kwa hiyo, kusema hiyo siyo *credit* ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yake ni jambo la ajabu kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nataka vilevile nizungumzie suala la kilimo. Kilimo kama tunavyokubaliana Kilimo Kwanza ni lazima sasa tuangalie suala la *incentives* yaani motisha kwa kilimo. Pale kwenye kilimo motisha kubwa kabisa ni bei ya mkulima yaani *producer price*. Bei ya mkulima ndiyo inamuondolea shida maana ni pesa zake za mfukoni, ukiwa na gunia la mpunga ukaliuza kwa shilingi 20,000/= halafu ikafika wakati ukauza kwa shilingi 40,000/= maana yake umepata shilingi 20,000/= *extra* kutohana na gunia lile lile moja kwa hiyo bei ya mkulima ni muhimu kabisa na hili Serikali ilitazame kwani tusipolitazama kilimo kitaendelea kuwa duni, bei ndiyo *incentive* ya kwanza. Hivi vingine kwa mfano mikopo ya bei nafuu kwa mkulima ni jambo zuri vilevile ingawa leo asubuhi mdogo wangu pale Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee alipokuwa anataja masharti ya *TIB* kuhusu mikopo alisahau sharti moja kubwa sana, sharti la *down payment* ya 20%, hii *down payment* ya 20% mbaya maana trekta la shilingi milioni 40 lazima aweke shilingi milioni 8 mpaka shilingi milioni 10, hela hizi ni nyangi kwa mkulima kwa wakati mmoja, kwa hiyo, hapa unapunguza watu kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki moja ya kibinagsi ya kibashara inaweka *down payment* ya 10%, sasa hapa mnaona mnavyofanya *contradiction*, ninyi mmefungua hili mnaita dirisha la kilimo katika *TIB* halafu tena mnaweka masharti magumu kwa kweli *it is a contradiction* mimi naona hili jambo mlifikirie, mimi nimelisema mara mbili au tatu sasa hapa Bungeni na sasa naomba niseme mara ya mwisho kwa sababu sitalirudia tena kulisema na mimi naamini Serikali wanalisikia hili. Hili tulikalie kitako, tulimalize, tusiliendeleze hili kwa sababu halina tena motisha kwa mkulima.

Mimi kwangu nina uzoefu, sisi tumeshakopa matrekta karibu kumi kwa kupitia benki hii ya *FBME Bank* lakini sasa tutakopa kupitia *TIB* matrekta sita, lakini matrekta

sita yale ni *more expensive* kuliko yale matrekta kumi tuliyopata mwanzo kwa kupitia *FBME Bank*. Kwa hiyo, lazima Serikali ilitazame hili kwa sababu tutapata matrekta mengi zaidi kama tukiwa na msimamo mzuri kuhimiza kilimo. Lakini vilevile mimi nimefurahi sana katika ukurasa wa 75 nadhani tunazungumzia kwamba tunatoa motisha kwa matrekta na kwa ma-*harvester*, hili suala la *harvester* limetajwa kwa mara ya kwanza katika maandishi ya Serikali, hili jambo zuri. Kwa mfano, sisi jimboni kwangu kule tulipata sana Mpunga lakini umeharibika, kwa nini? Kwa sababu tumechelewa kuvuna *of course* kuna mvua ambayo imesababisha hivyo lakini vilevile mazao mengi tu kwamba bila kutumika *harvester* hutumie kufye ka mkono na kupiga kazi hiyo ni kubwa sana. Kwa hiyo, Serikali kufanya maamuzi haya mimi nayaunga mkonona tuendelee kufanya vizuri. Kwa hiyo, hili naomba lieleweke hivi ili Serikali ilitazame na iendelee kulitilia mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka kulizungumzia, mimi nimevutiwa sana na Serikali kuanza kuunda sasa Tume ya Mipango. Tume ya Mipango moja ya majukumu yake itakuwa ni kupanga mipango ya muda wa kati na muda mrefu, hii ndiyo njia nzuri kwa nchi yetu. Kwanza tunaji-*contradict* MKUKUTA ni mpango wa miaka mitano lakini tukija kufanya Bajeti hapa tunapanga mpango wa mwaka mmoja mpaka miaka mitatu *actually* ni wa mwaka mmoja miaka ile mitatu mingine ni *indicative* tu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi nadhani sasa ni wakati muafaka kuanzia mwaka kesho wa fedha basi tuendelee na mpango wa miaka mitano kama tulivyopanga katika mpango wa MKUKUTA I na MKUKUTA II na hili ni jambo muhimu la kupanga kwa sababu watu maskini kama sisi huwezi kupanga mambo yako vizuri, huwezi kufikia malengo unayotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika vipaumbele hivi tunapta matatizo kwa sababu ya hilo tu kwamba kwa mfano leo tumepanga hapa tangu mwaka 2006 elimu ndiyo tunaiweka namba moja ikifuatiwa na miundombinu, sasa katikati hapa unataka kuibadilisha utapata matatizo kwa sababu hata ufanyeje umeshajenga tayari Chuo Kikuu cha Dodoma, umepanua Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mzumbe, ni lazima uendelee kuwapa Bajeti ya kutosha ili vyuo hivi viendelee kutoa wanafunzi kwa kiwango kinachotakiwa, huwezi kusema utakata Bajeti hapa, haiwezekani na suala la kutoa kipaumbele kwa elimu ni la kihistoria pia wenzetu wanaofanya maendeleo mazuri *South Korea*, China na Japan huko ndiko walikotilia mkazo elimu, ukitalia mkazo elimu ndiyo unaweza kupata wataalamu wanaotakiwa hata mambo haya ya afya unaweza kuyazuia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na sasa nitamuita Mheshimiwa Mnyaa na atafuatiwa na Mheshimiwa Ania Chaurembo.

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi hii ya kuchangia Bajeti hii. (*Makofî*)

Kwanza napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mkanyageni kwa kunipa kura za kutosha katika uchaguzi wa kura za maoni. (*Makofî*)

Pili, napenda kumpongeza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa hotuba yake ya Bajeti ambayo imeonyesha kasoro nyingi za Serikali na ninategemea badala ya kuchukia au badala ya kukasirika itakuwa ni kigezo kizuri cha Serikali kupokea yale maoni na kurekebisha katika miaka ijayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo napenda nianze kwa kukumbusha kwamba nchi hii tangu Uhuru kama kuna mafanikio yoyote yaliyopatikana yamepatikana kwa mujibu wa Sera za Chama cha *TANU*, *ASP* na hatimaye *CCM* na kama kuna upungufu basi vilevile umefanywa na Sera za *CCM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, upungufu ambao tutaukosoa au umekosolewa ni changamoto kwa Sera za *CCM* na wananchi wanasikia na wanaona na kwa hiyo ni wao kujirekebisha kama wanataka Bajeti hii isiwe ndiyo kilio chao katika uchaguzi unaokuja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda niseme kwamba katika kipindi chote kabla mimi kuingiza Bungeni hapa miaka mitano iliyopita na hii miaka mitano ambayo inaishia, katika kipindi si chini ya miaka 10 katika Bajeti zote hutanguliwa na Bajeti ya mipango na uchumi na baadaye Bajeti ya fedha. Katika Bajeti zote hizo, basi kitu kikubwa kinachozungumziwa ni mipango na mipango yoyote ya uchumi haiwezi kukamilika bila ya kuwa na nishati ya kutosha, tutakuwa tunajidanganyana. (*Makofî*)

Lakini mipango hiyo ya kuwa na nishati ya kutosha hapa mpaka leo imekuwa inafeli, timesikia katika Bajeti zote za miaka yote mitano iliyopita *story* au hadithi za Mchuchuma, Liganga, *Stigler's George*, Rusumo, Kinyerezi, Kiwira na kadhalika lakini katika kipindi cha miaka mitano ni mradi miwili tu ya *Ubungo Power Plant* na Tegeta ndiyo iliyoweza kukamilika. Hiki ni kitendo cha aibu! Tunasema sana lakini utekelezaji hakuna na bahati mbaya jirani zetu kila tukisema wao wanatekeleza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo nchi nyingi sana duniani hazina vyanzo vya nishati lakini hazina ukosefu wa umeme, ziko nchi nyingi duniani hazina ardhi ya kulima lakini husikii kuna njaa, Tanzania yenye vyanzo vingi vya nishati havina idadi, leo hatuna umeme wa kutosha mpaka ni hadithi na maneno tu. Tanzania ambayo tuna ardhi ya kutosha ya kilimo bado tunategemea kila siku na sababu ni ukame tu, hatuna sababu za kusingizia ukame, hizo nchi ambazo hazina ardhi kwa nini wasisingizie ukame? Inafaa tujirekebishe, maneno yasiwe mengi lakini sasa tubadilike vitendo viwe vingi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa sana linalokabili nchi hii ni mipango kabambe ambayo ipo kwa msingi wa kujua Tanzania tunatoka wapi na tunakwenda wapi,

mipango hiyo ambayo ilikuwepo tangu wakati wa enzi wa Baba wa Taifa ndiyo aliyefanya mipango hata mwaka 1969 likawepo Shirika la *TPDC* na leo ndiyo tunajivunia Shirika la *TPDC* na ndiyo tunajua tunaeleleka wapi, lakini baada ya kuondoka mipango mingi sana imefutika, hakuna *coordination* katika Serikali. Ile *coordination* tu baina ya Wizara na Wizara inakosekana na nitatoa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Wizara ya Fedha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha, Mipango na Uchumi iliyotolewa ilionyesha takwimu za gharama zinazopatikana kwa *IPTL* wakaonyesha mafuta mazito, gharama na vipuri, gharama za *capacity yard*, *Tin percent VAT* wakaonyesha na *exchange rate* na ikawa kila mwaka Tanzania tunapoteza shilingi bilioni 20 kwa *IPTL* ni sawa na dola milioni 180.7. Lakini Wizara ya Nishati na Madini ilipoeleza taarifa kama hiyo kwa Kamati ya Nishati na Madini imetoa takwimu tofauti, wametoa kiwango cha mafuta *HA4*, wametoa vipuri vilainishi, gharama za *capacity charge*, *18% VAT* na wao wamefikia shilingi bilioni 24 au dola za Marekeni milioni 190. Sasa ikiwa Serikali hii hii moja Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Fedha ina viwango tofauti kwa kitu kinacholipiwa *IPTL* hilo ni tatizo kubwa sana yaani *lack of coordination*, hakuna uwiano baina ya Wizara hizi kupima matatizo nchini. Huo ni udhaifu mkubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa katika Ilani ya CCM walisema na nitanukuu; “Kuweka mkakati wa uzalishaji umeme wa kutosha na wa gharama nafuu zaidi kwa lengo la kuongeza ufanisi viwandani.“ Ukurasa wa 51.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa leo tunalipa bilioni 20 au bilioni 24 which ever current kwa sababu ilitolewa na Wizara mbili tofauti kwa kulipia gharama za kuendesha *IPTL* na katika takwimu za mitambo duniani kitabu hiki kwa ruhusa ya Mwenyekiti wangu wa Kamati nataka hata Waziri wa Fedha akione ambacho kina mitambo na makampuni yote ya umeme duniani na *indicative prices* bilioni 24 au dola 180 au 190 unanunua mtambo wa *megawatt 100* kila mwaka lakini leo tunakula hasara pale *IPTL*. Huu ni udhaifu ikiwa hata Wizara zinazohusika *indicative prices* hazioni na bado tunaingia katika mipango ile ya zimamoto ya mitambo hii, hii ni hatari na ni lazima Serikali ijirekebishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hiyo tu kuna mipango mingi sana mibovu, kule Mwanza ulipelekwa mtambo wa *power rental* na ukakaa mwaka mmoja na ukafika wakati wa kuondoka hakuna umeme wowote uliozalishwa na pesa nyingi sana tumepoteza. Lakini leo katika Bajeti hii Mheshimiwa Waziri mbali ya misahama ya kodi unayoifanya, ukurasa huu wa 61 unakwenda kwa mfano katika hii Sheria ya Usalama Barabarani sura ya 168, unakwenda kuongeza kiwango katika ada za leseni kwa 66.7% kwa gari zenye ujazo wa CC 500, 100% kwa gari zenye CC 1500, kwa 50% kwa gari zenye CC 2500 unaifanya hii kada ya hapa katikati kwamba wazidi kudhoofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda pale Dar es Salaam *Taxi* zinakaa hazina kazi, *Taxi* moja inakodi zaidi ya nane wanazolipia sasa tunawabana hawa wa *cadre* ya katikati kunyanyuka, tunawaacha matajiri na wawekezaji wakubwa kwa *PSA*, huu ni

udhaifu mkubwa. Kwa hiyo, hii mipango ya kupunguza umaskini haiwezi kuisha kwa Bajeti za namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ninayoyasema yanadhihirika pale ambapo tunapata kulinganisha wakati matumizi ya Bajeti ya kawaida inakuwa shilingi bilioni 3.8 kwa mfano mwaka 2007/2008 wakati matumizi ya maendeleo ni shilingi bilioni 2.2, mwaka 2008/2009 Bajeti ya kawaida shilingi trilioni 4.7 wakati ya maendeleo ni shilingi trilioni 2.4 halafu tunategemea kupata maendeleo, wapi? Tumeona na tunashuhudia na takwimu zipo nchi za jirani hawa ambao tunataka hii Jumuiya ya Afrika Mashariki wenzetu wao Bajeti ya Maendeleo ni kubwa kuliko Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kwa Bajeti za namna hii hivi kweli Tanzania tunategemea kupata maendeleo? Haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maduka Dar es Salaam ya Wachina, kweli wana *TIN number* na wanalipa kodi kwa asilimia ndogo, lakini utakuta duka kubwa lina uwezo mkubwa halikuwa *VAT registered* na mimi *research* hii nimefanya juzi hapa Dar es Salaam. Ndugu zetu Watanzania nafasi wanazikosa lakini Wachina wamemiminika, hivi kweli *TRA* hawaoni? Hivi kweli bidhaa hizi zinazoingizwa nchini *TRA* hawazioni? Hivi kweli wale wengine wana kiwango cha *TIN* bila kuwa *VAT registered*?

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Ahsante!

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Ya ngapi hiyo?

NAIBU SPIKA: Ya pili!

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Hatuwezi kuunga mkono hoja Bajeti hii isipokuwa labda itategemea Mheshimiwa Waziri atakavyojieleza. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Tunashukuru na sasa ni Mheshimiwa Ania Chaurembo atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya.

MHE. ANIA S. CHAUREMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo ili nichangie. (*Makofii*)

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya njema na kusimama hapa leo katika Bunge lako hili la mwisho na kuchangia katika hoja iliyokuwepo mbele yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kuhusu manunuzi ya umma. Kumekuwa na upotevu mkubwa wa pesa katika manunuzi ya umma na Sheria inayohusu manunuzi ya umma inahitaji marekebisho na hata ile iliyokuwepo bado watendaji wa Serikali hawaifanyii kazi ipasavyo na matokeo yake ndiyo haya sasa hivi Serikali inapoteza pesa nyingi sana kwa manunuzi ya umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile nizungumzie habari ya MKUKUTA. MKUKUTA I tayari umeshafanyiwa kazi na sasa tunatakiwa kwenda katika MKUKUTA II. Ni vyema basi tukaambiwa na Watanzania wakaelezwa manufaa yaliyopatikana katika MKUKUTA I kabla hatujaendelea na MKUKUTA II.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuzungumzia suala zima juu ya fedha nyingi zinazotolewa na Serikali kupelekwa kwenye Halmashauri. Nimepata bahati ya kutembelea Halmashauri nyingi hapa nchini nikiwa katika Kamati ya *LAAC*, mambo nimeyaona mwenyewe na wala siyo ya kusoma katika vitabu. Fedha nyingi zinazopelekwa katika Halmashauri kuna baadhi ya watendaji wasiokuwa waaminifu wanazitumia sivyo inavyopangwa na Serikali Kuu na matokeo yake baadhi ya Madiwani wa eneo lile kulalamika au kwa Kamati hizi yule mtu ambaye tayari pale ameharibu na anaonekana kabisa kwamba ni fisadi anaondolewa katika eneo lile kupelekwa eneo lingine ili akafanye uharibifu vilevile, hawa watu wapo na wanajulikana na ushahidi upo. Hatuwezi kuendelea katika hali hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia Bajeti ya mwaka 2010/2011 pesa zimeongezwa tena katika Halmashauri, sasa mimi nataka kidogo Waziri anieleze, je, wale watu ambao tayari nimewataja hapo wa aina hiyo wataendelea kweli kuwa katika Halmashauri ambapo bado wanaendelea na ufisadi wa kuharibu fedha za Serikali na tukienda wananchi wanalamika wanasema huyu kaharibu huko tunaletewa sisi, ina maana kuna *chain* kutoka katika Halmashauri mpaka Wizarani. Naomba Serikali ichunguze hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu jiji la Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam hivi sasa lina matatizo makubwa ya huduma ya afya na Mbunge wa Ilala amesema kwamba huduma ya afya sasa hivi inatakiwa kuboreshwa na kupewa hadhi ya Mkoa, lakini je, tunaipa hadhi ya Mkoa kwa mazingira yapi? Kama ya Wilaya haikukidhi haja na bado hatujaboresha miundombinu ya majengo wala hakuna madaktari wa kutosha sasa hivyo sasa hiyo hadhi tu ya kubadilisha jina itasaidia kweli wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wapatao milioni nne? Bado hapa mimi naona kuna tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekeso langu ni kwamba Jiji la Dar es Salaam pamoja na kuwa kuna Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili na *CCBRT* vilevile inapewa hadhi ya Mkoa, lakini bado ile haifanyi kazi kama Mkoa, ifuatiliwe sasa ili ianze kazi kama Mkoa na hizo Wilaya tatu ambazo zinataki kupandishwa hadhi basi kwanza tujenge majengo ya uhakika kwani akina mama wanazalia chini sasa hivi, wazazi wanalala chini hakuna mtu asiyejua katika ukumbi huu, *television* zinaonyesha hali mbaya, tunapiga kelele ya UKIMWI, wakati watu wakishajifungua wanalala kitanda kimoja wawili mpaka watatu, tunafanya nini? Hili ni tatizo!

Kwa hiyo, Dar es Salaam ni lazima ieleweke kwamba sasa hivi kila mtu aliyekuwa Mkoani au Wilayani anatamani kuja katika jiji la Dar es Salaam na wala hatamani kuja Dodoma, Dodoma wanakuja wasomi kwa ajili ya kufanya kazi. Sasa jiji

hili liangaliwe, ijengwe hasa hospitali maalum ambayo itakuwa kubwa inayofanana na Muhimbili, Watanzania wote sasa hivi wenyewe matatizo wanakwenda Dar es Salaam, jamani hebu nendeni Muhimbili mkaangalie watu wanavyoteseka, mtu anakuja na ugonjwa mkubwa anaambiwa arudi baada ya miezi nane ndiyo aonane na daktari. Hili ni tatizo naomba litatuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia suala lingine kuhusu uvuvi. Wenzangu hapa wamezungumzia lakini kwa kweli tunahitaji kutilia mkazo suala hili. Wavuvi hivi karibuni wamepata msukosuko wa ajabu kabisa wamechomewa, wanasukumwa, wamenyang'anywa. Sasa tulitegemea baada ya mambo yote hayo kufanyika wavuvi watapewa somo jipya, wataelekezwa vitendea kazi, watapewa boti zenye hadhi ya kuvua ili wasiharibu mazingira ya bahari na maelekezo, mikopo pia ya kuwasaidia katika kazi yao. Sisi watu wa Pwani tumezoea kula samaki sasa hivi samaki unanunua shilingi 40,000/= samaki mmoja tu aina ya Kolekole anauzwa mpaka shilingi 40,000/= kwa hiyo, watu wanaumia sana katika suala hili. Naomba wavuvi waangaliwe kwa jicho la huruma. (*Makofi*)

Lakini mimi sasa hivi nilikuwa nazungumzia suala la elimu, nawapongeza sana na watu wamesema hapa shule zimejengwa mwenye hamsini au thelathini. Lakini napenda kuchangia kwamba baadhi ya shule hizo hazina hadhi ya shule na pesa hizi zimechukuliwa kama mkopo ambao watalipa Watanzania. Tumetembelea shule tumeukuta ukishika tofali linatoka mchanga, kwa hiyo, hili nalo liangaliwe vile viwango ambavyo Serikali imetoa viwango vizuri tu kabisa lakini watendaji wetu hawataki kufuata viwango nya Serikali na Serikali ifuatilie suala hili karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisema habari ya elimu tunasema habari ya walimu, vitabu, vitendea kazi na nyumba za walimu. Ni mambo ya aibu sana, juzi kama wiki mbili tu nimetoka ziara, walimu watano akiwemo mwalimu mkuu katika Mkoa wa Tanga wanakaa nyumba moja, walimu wanasikitika wanasesma tuna familia zetu lakini hatuwezi kuzileta ndiyo maana walimu wanashawishika kutembea na wanafunzi na kuwatia mimba kwa sababu wanakosa haki yao ya kibinadamu. Kwa hiyo, naomba walimu pesa inayotolewa ilekezwe katika suala la walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na sasa nimuite Mheshimiwa Suleiman Kumchaya.

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kumchaya samahani sana, unajua mimi nilikuwa naona kama ni saa kumi na mbili na robo kumbe ni saa mbili kasoro robo, kwa hiyo naomba radhi kesho utakuwa wa kwanza na niwataje wengine watakaofuatia watakuwa ni hawa wafuatao Mheshimiwa Charles Keenja kwa sababu nimeshamtaja na

Mheshimiwa Manju Msambya na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na wengine watafuatia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, sina matangazo mengine naahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

(*Saa 1.42 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumamosi,
Tarehe 12 Juni, 2010 saa tatu asubuhi*)